


Ufunuo wa Yesu Kuhusu Kuzimu

na **Mary K Baxter** Ministry

www.DivineRevelations.info/SWAHILI

Translated to Swahili by Ambakisye Mtawa, ambamtawa@gmail.com



Sikiliza ushuhuda wa moja kwa moja juu ya uwepo Halisi wa Kuzimu. Mary Katherine Baxter alichaguliwa na Mungu ili kuujulisha ulimwengu juu wa UHALISI wa Kuzimu. Yesu Kristo alimtokea Mary Baxter wakati wa usiku siku 40 mfululizo na kumtembeza kuzimu na Mbinguni. Alitembea, na Yesu, na kuona mambo ya kutisha ya Kuzimu na alizungumza na watu wengi. Yesu alimwonyesha ni kitu gani kinatokea roho zinapokufa na mambo gani yanatokea kwa wasioamini na watumishi wa Mungu ambao hawatii wito walioitiwa.



Neno la Awali Wakfu	Sura ya 9 – Vitisho vya Kuzimu	Sura ya 19 – Mdomo wa Kuzimu
Utangulizi	Sura ya 10 – Moyo wa Kuzimu	Sura ya 20 - Mbinguni
Sura ya 1-Kwenda Kuzimu	Sura ya 11 – Giza la Nje	Sura ya 21 – Dini ya Uongo
Sura ya 2 - Mguu wa Kushoto wa Kuzimu	Sura ya 12 - Pembe	Sura ya 22 – Alama ya Mnyama
Sura ya 3 - Mguu wa Kulia wa Kuzimu	Sura ya 13 – Mkono wa Kulia wa Kuzimu	Sura ya 23 – Kurudi kwa Kristo
Sura ya 4 - Mashimo Zaidi	Sura ya 14 – Mkono wa Kushoto wa Kuzimu	Sura ya 24 – Ombi la Mwisho la Mungu
Sura ya 5 – Pango la Hofu	Sura ya 15 – Siku za Yoeli	Sura ya 25 – Maono ya Mbingu
Sura ya 6 - Matendo Katika Kuzimu	Sura ya 16 – Kitovu cha Kuzimu	Sura ya 26 –Unabii Kutoka kwa Yesu
Sura ya 7 – Tumbo la Kuzimu	Sura ya 17 – Vita Katika Mbingu	Maneno ya Kufungia
Sura ya 8 – Selo za Kuzimu	Sura ya 18 – Maono ya Wazi Kutoka Kuzimu	Kuhusu Mwandishi Mwaliko wa huduma

Neno la Awali

Marcus Bach alisema kwamba mara nyingi vitabu ni kama watoto wa akili, wala hakukosea. Sio kama watoto wa nyama na damu, watoto hawa, wanaozaliwa kwa kupanga au kwa bahati wamepangiwa maisha yao wenyewe. Kuishi kwao katika ulimwengu huu kunafanana na watoto wengine. Hisia zote za kibinadamu ni zao. Si ajabu hofu yao ya siri ni kwamba siku moja watawekwa kando na kusaulika moja kwa moja.

Tofauti na vitabu vingine, ninaamini kwamba Roho Mtakatifu amefanya maandishi haya kuwepo kwa muda na milele. Ushuhuda na ujumbe huu ni wa muhimu sana kwa mwili wa Kristo. Ninaamini kwamba upako wa Mungu utakuwa juu ya kitabu hiki na kumhudumia kila mtu asomaye yaliyomo.

Wakfu

Kazi hii imewekwa wakfu kwa utukufu wa Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu, bila Yeye kitabu hiki kisingewezekana kuwepo.

Utangulizi

Ninatambua kwamba bila nguvu za Bwana Yesu Kristo, kitabu hiki au kingine kinachoshughulikia na maisha baada ya kifo kisingeandikwa. Yesu peke yake ndiye aliye na funguo za Kuzimu na amelipa gharama za kutuingiza mbinguni.

Niligundua kwamba kuandika kitabu hiki ilikuwa ni kazi ndefu, ya upweke, na ngumu. Kwa kweli kitabu hiki kimesubiri miaka mingi kufunuliwa. Ufunuo kutoka kwa Bwana ulinijia mwaka 1976. Ilinichukua miezi minane kuuandika katika karatasi. Uandikaji wa rasimu ulichukua miaka mingi na uwekaji wa vifungu vya Maandiko hatua kwa hatua ilinichukua mwaka mwingine zaidi. Kukamilisha kitabu kulichukua msimu wa baridi wa 1982 na mwaka 1983. Vile vile kwa muda wa siku thelathini, Yesu alinichukua hadi Kuzimu wakati wa usiku, zikafuata siku kumi za kutembelea mbinguni wakati wa usiku.

Sasa naona kwamba Bwana alikuwa ananiandaa kuandika kitabu hiki tangu nilipokuwa mtoto mdogo nilipokuwa naota mambo ya Mungu. Baada ya kuzaliwa mara ya pili, nilikuwa na mapenzi sana kwa waliopotea na nilikuwa natamani kuona roho zikiokolewa.

Baadaye Bwana alinitokea mwaka 1976 na kuniambia kwamba nilikuwa nimechaguliwa kwa ajili ya kazi maalum, Aliniambia,

“Mwanangu, nitajithibitisha kwako na kuwatoa watu kutoka gizani na kuwaleta nuruni. Kwa maana Bwana Mungu amekuchagua kwa kusudi, kuandika na kuweka kumbukumbu ya mambo nitakayokuonyesha na kukuambia.

"Nitakufunulia uhalisi wa kuzimu, ili wengi waokolewe, wengi watatubu njia zao mbaya kabla hawajachelewa.

"Roho yako itachukuliwa kutoka kwenye mwili wako, na mimi, Bwana Yesu Kristo, na kupelekwa kuzimu na sehemu nyingine nitakazopenda kukuonyesha. Vile vile nitakuonyesha maono ya mbinguni na mahali pengine na kukupa mafunuo mengi."

Mary Kathryn Baxter

Kwa Kathryn kutoka kwa Yesu

Kwa kusudi hili ulizaliwa, kuandika na kueleza mambo niliyokuonyesha na kukuambia. Maana mambo haya ni uaminifu na kweli. Wito wako ni kuufanya ulimwengu ujue kwamba kuna kuzimu, na kwamba Mimi, Yesu, nilitumwa na Baba ili kuwaokoa kwenye mateso haya.

Sura ya 1

Kwenda Kuzimu

Mwezi Machi 1976 nilipokuwa naomba nyumbani, nilitembelewa na Bwana Yesu. Nilikuwa nikiomba katika Roho kwa siku kadhaa ambapo mara nilihisi uwepo halisi wa Mungu. Nguvu yake na utukufu wake ulijaza nyumba. Mwanga mkali ulikijaza chumba nilimokuwa naomba, na hali ya kujisikia vizuri ilinijia.

Mwanga ulikuja kama mvuke, ukiviringika na kujikunja na kujikunjura tena. Lilikuwa jambo la ajabu. Ndipo sauti ya Bwana ikaanza kuzungumza nami.

Alisema, "***Mimi ni Yesu Kristo, Bwana wako, nataka kukupa ufunuo wa kuwaandaa watakatifu kwa ajili ya kurudi kwangu na kuwageuza wengi kuelekea kwenye haki. Nguvu za giza ni halisi na hukumu zangu ni halisi.***

"Mwanangu, nitakupeleka kuzimu kwa Roho Yangu, na nitakuonyesha mambo mengi ambayo nataka ulimwengu uyajue. Nitaonekana kwako mara nyingi; nitaichukua roho yako nje ya mwili wako na nitakupeleka kuzimu kihalisi.

"Nataka uandike kitabu na ueleze maono yote na mambo yote nitakayofunulia. Mimi na wewe tutatembea kuzimu pamoja. Andika mambo haya yaliyopo na yatakayokuja. Maneno yangu ni hakika, kweli, aminifu. Mimi Ndimi, wala hakuna mwingine badala yangu."

"Bwana wangu," nililia, "Unataka nifanye ninii?" Kila kitu ndani yangu kilitaka kumlilia Yesu, kukiri uwepo wake. Nikijitahidi sana kueleza niseme kwamba upendo ulinifunika. Ulikuwa ni upendo mzuri, wa amani, wa furaha, wenye nguvu, kuliko nilivyowahi kuhisi wakati wowote.

Sifa za Mungu zilianza kunimiminika. Pale pale nilitamani kumpa maisha yangu yote ayatumie, kusaidia kuwakoa watu katika dhambi. Nilijua, kwa Roho wake, kwamba alikuwa Yesu Mwana wa Mungu aliyekuwa chumbani pamoja nami. Sipati maneno ya kuelezea uwepo wake. Lakini najua kwamba najua kwamba alikuwa ni Bwana.

"Angalia , mwanangu," Yesu alisema, "**Ninakuchukua kwa roho wangu hadi kuzimu ili uweze kuelezea uhalisi wake, kuiambia dunia nzima kwamba kuzimu ni halisi, na kuwatoa waliopotea kutoka gizani kuingia kwenye nuru ya injili ya Yesu Kristo.**"

Mara ile ile, roho yangu ilitolewa ndani ya mwili. Nilitoka na Yesu kutoka ndani ya chumba changu tukaingia hewani. Nilikuwa na ufahamu wa mambo yote yaliyokuwa yananzunguka. Nilimuona mume wangu na watoto wamelala pale chini nyumbani.

Ilikuwa kama nimekufa na mwili wangu umeachwa nyuma kwenye kitanda wakati roho yangu inapanda juu na Yesu kuitia paa la nyumba. Ilikuwa kama paa lote limeezuliwa, na niliona familia yangu imelala vitandani.

Niliona Yesu akinigusa na kuniambia, "**Usiogope. Watakuwa salama.**" Alitambua mawazo yangu.

Nitajihidi kwa kadri ya uwezo wangu kueleza hatua kwa hatua niliyoyaona na nilivyojisikia. Mambo mengine sikuelewa. Bwana Yesu alinieleza maana ya mambo mengi, lakini mambo mengine hakuniambia.

Nilifahamu wakati ule, na sasa nafahamu, kwamba mambo haya yalikuwa yanatokea kihalisi na Mungu mwenyewe ndiye angeweza kunionyesha. Litukuzwe Jina lake. Jamani, niamini, kuzimu ni halisi.Nilipelekwa kule na Roho mara nyingi wakati wa kuandaa taarifa hii.

Mara tulikuwa katika anga za juu. Niligeuka na kumtazama Yesu. Alikuwa amejaa utukufu na nguvu, na amani ya ajabu ilifurika kutoka kwake. Alichukua mkono wangu na kusema, "**Nakupenda. Usiogope, maana niko pamoja nawe.**"

Baada ya hayo, tulianza kupaa juu zaidi mawinguni, na sasa niliweza kuiona dunia kwa chini. Katika sehemu nyingi kulikuwa na mashimo (faneli) yaliyokuwa yanajizungusha kueleka mahali fulani, na kurudi tena yalikotoka.. Haya yalikuwa yanatembea juu sana ya dunia na yalikuwa kama kitu fulani kikubwa, kichafu na kinachoteleza kinazunguka wakati

wote. Vilikuwa vinajitokeza duniani pote. “*Vitu gani hivi?*” Nilimuuliza Bwana Yesu tulipokuwa tunakikaribia kimojawapo.

“Haya ni malango ya kuzimu, Aliniambia. ***Tutaingia kwenye mojawapo.***”

Mara tuliiingia mojawapo ya mashimo haya. Ndani lilioneekana kama tanuru, likizunguka na kuzunguka kama pia.

Giza nene ilituangukia, na pamoja na giza hilo ilikuja harufu mbaya sana kiasi cha kwamba ilikausha pumzi yangu. Kwenye kuta za shimo hili kulikuwa na viumbe vimeganda kwenye kuta. Vilikuwa na rangi ya zambarau, viumbe hivi vilitembea na kupiga kelele tulipopita. Nilijua bila kuambiwa kwamba vilikuwa viovu.

Viumbe hivi vingeweza kutembea lakini viliganda kwenye kuta. Vilitoa harufu mbaya sana, na vilitupigia kelele zenyе kukera kweli. Nilihisi nguvu fulani ya giza, isiyooonekana, ikitembea ndani ya mapango.

Wakati fulani, katika giza, niliweza kuona maumbile. Chura mchafu alijaza kuta za pango. “*Bwana vitu gani hivi?*” Niliuliza huku nikishika mkono wa Yesu kwa nguvu.

Alisema, “***Hizi ni roho chafu ambazo ziko tayari kumwagwa duniani pindi Shetani atakapotoa amri.***”

Tulipokuwa tunashuka kwenye pango, viumbe hivyo viovu vilicheka na kutuita. Vilijaribu kutugusa, lakini havikuweza kwa sababu ya nguvu ya Yesu. Hewa yenewe ilikuwa chafu, ni uwepo wa Yesu tu ulionizuia kupiga kelele kwa utisho mkubwa uliokuwepo.

Oh, ndio, nilikuwa na fahamu zangu zote – niliweza kusikia, kunusa, kuona, kugusa na hata kuonja uovu wa mahali hapa. Zaidi ya hapo fahamu zangu ziliikuwa makini zaidi, harufu na uchafu vilinitia kichefuchefu.

Mayowe yalijaza hewa tulipokaribia mwanzo wa shimo. Vilio vikali vilipanda juu na kutulaki. Sauti za kila namna zilijaza hewa. Nilisikia hofu, mauti na dhambi vikinizunguka.

Harufu mbaya ambayo sijawahi kunusa ilijaza hewa. Ilikuwa harufu ya mzoga unaooza, na ilielekea kutoka kila upande. Kamwe hapa duniani nilikuwa sijawahi kuhisi kiasi hiki cha ouvu au kusikia sauti za namna hii za kukata tamaa. Muda si muda ningeligundua kwamba mayowe haya yalikuwa ya wafu na kwamba kuzimu kulijaa mayowe yao.

Nilisikia mvumo wa upepo mbaya na mvuto mdogo mbele yetu. Mwanga kama wa radi ulipenyeza kwenye giza nene na kutupa vivuli vyeusi vyeusi kwenye kuta. Niliweza kuona umbile la kitu fulani mbele yangu. Nililishtuka nilipotambua kwamba joka kubwa lilikuwa linatambaa mbele yetu. Nilipoendelea kutazama niliona nyoka wengi wabaya wanatambaa kila mahali.

Yesu aliniambia "***Muda si mrefu tutaingia kwenye mguu wa kushoto wa kuzimu. Huko mbele utaona huzuni kubwa, masikitiko ya kutisha na vitisho visivyoelezeka. Kaa karibu na Mimi, nami nitakupa nguvu na ulinzi tunapopita kuzimu. Mambo ambayo utayaona ni tahadhari, Aliniambia.*** " ***Kitabu utakachokiandika kitaziokoa roho nyngi zisiende kuzimu. Unayoyaona ni halisi. Usiogope, kwa maana nitakuwa pamoja nawe***"

Hatimaye, Bwana Yesu namimi tulifika chini ya shimo. Tuliingia kuzimu. Nitajitahidi kwa uwezo wangu wote kukueleza niliyoyaona, na nitasimulia kwa ule mpangilio amba Mungu alinipa.

Mbele yetu, kwa kadri nilivyoweza kuona, kulikuwa na vitu vinaruka huku na kule. Sauti za kukoroma na vilio vya huzuni vilijaza hewa. Juu niliona mwanga hafifu, na tulianza kuufuata. Njia ilikuwa kavu na yeny mavumbi. Mara tulifika kwenye mlango wa kuelekea kwenye shimo dogo lenye giza.

Mambo mengine siwezi kuyaandika kwenye karatasi; yalikuwa yanatisha mno kuyaeleza. Kuzimu hofu unaisikia hasa, na nilijua kwamba kama nisingelikuwa na Yesu nisingeweza kurudi. Katika kuandika haya, baadhi ya mambo niliyoyaona sikuyaelewa, lakini Bwana anajua yote, na alinisaidia kuelewa mambo mengi niliyoyona.

Nakuonya, usiende mahali kule. Ni mahali penye mateso ya ajabu, maumivu makubwa, na huzuni ya milele. Roho yako itakuwa hai wakati wote. Roho inaishi milele. Roho ndio wewe, na roho yako itakwenda mbinguni au kuzimu.

Kwa wale mnaodhani kwamba kuzimu ipo hapa duniani – sawa, ipo hapa. Kuzimu ipo katikati ya dunia, na kule kuna roho ziko kwenye mateso usiku na mchana. Kuzimu hakuna sherehe. Hakuna upendo, hakuna kuhurumiana. Hakuna kupumzika. Ila ni mahali penye masikitiko zaidi ya unavyoweza kudhani.

Sura ya 2

Mguu wa Kushoto wa Kuzimu

Harufu chafu ilijaza hewa. Yesu aliniambia, " *Katika mguu wa kushoto wa kuzimu kuna mashimo mengi. Shimo hili limegawanyika kwenda sehemu nyingine za kuzimu, lakini tutatumia muda kadhaa katika mguu wa kushoto kwanza. Mambo unayokwenda kuyaona yatakuwa nawewe daima. Ulimwengu lazima ujue juu ya uhalisi wa kuzimu. Wenyewe dhambi wengi na hata baadhi ya watu Wangu hawaamini kuwa kuzimu ni halisi. Umeteuliwa na Mimi kufunua ukweli huu kwao. Mambo yote nitakayokueleza kuhusu kuzimu na mambo mengine nitakayokueleza ni ya kweli.*"

Yesu alijihirisha kwangu kama mwanga mkali, mwangavu kuliko juu. Umbile la mtu ilikuwa katikati ya mwanga ule. Wakati mwingine nilimuona Yesu kama mwanadamu, lakini wakati mwingine alikuwa katika hali ya roho.

Alizungumza tena, " *Mwanangu, ninaposema ni Baba amesema. Baba na Mimi ni wamoja. Muhimu kuliko yote kumbuka upendo na kusameheana. Sasa njoo, nifuate.*"

Tulipokuwa tukitembea, pepo wachafu walikuwa wanakimbia kutoka kwenye uwepo wa Bwana. "O Mungu, O Mungu", Nililia. "Nini zaidi?"

Kama nilivyosema awali, kuzimu nilikuwa na uelewa wangu wote. Wote walioko kuzimu wana uelewa wao wote. Wa kwangu ulikuwa unafanya kazi kwa nguvu zote. Hofu ilitanda kila upande, na hatari zisizoelezeka zilijificha kila mahali. Kila hatua niliyosogea ilikuwa ilikuwa hatari zaidi kuliko iliyotangulia.

Kulikuwa na milango mfano wa madirisha madogo, ikifunguka na kufunga haraka sana juu ya shimo. Mayowe yalijaza hewa viumbe viovu viliporuka karibu nasi, vikienda nje na juu ya malango ya kuzimu. Mara tulikuwa mwisho wa shimo. Nilikuwa nikitetemeka kwa woga kwa sababu ya hatari na hofu iliyotuzunguka.

Nilishukuru sana kwa ulinzi wa Yesu. Namshukuru Mungu kwa nguvu za uweza wake za kutulinda, hata katika mashimo ya kuzimu. Hata katika ulinzi huo, nilikuwa nawaza, Sio kwa mapenzi yangu, Baba, bali mapenzi yako yafanyike.

Niliutazama mwili wangu. Kwa mara ya kwanza niligundua kwamba nilikuwa katika hali ya roho, na taswira yangu ilikuwa kama nilivyo.

Yesu na mimi tulichepuka kutoka kenyepo kwenda kwenye njia iliyokuwa na vipande vyatya ardhi kila upande. Kulikuwa na mashimo ya moto kila mahali mpaka upeo wa macho.

Mashimo yalikuwa na upana wa futi nne na urefu wa futi tatu na umbo lake lilikuwa kama bakuli. Yesu alisema, "**Kuna mashimo mengi ya aina hii katika mguu wa kushoto. Njoo, nitakuonyesha baadhi yake.**"

Nilisimama na Yesu kwenye njia na kuchungulia kwenye mojawapo ya mashimo. Kiberiti kilisiribwa kwenye kuta za shimo na kiliwaka kama makaa makali ya moto. Katikati ya shimo kulikuwa na roho iliyopotea iliyokufa na kwenda kuzimu. Moto ulianzia chini ya shimo, ukapanda juu na kuifunika roho ile katika ndimi za moto. Mara moto hufifia, halafu tena kwa mvumo wa sauti huenda tena kwenye roho inayoteseka katika shimo.

Nilipotazamaniliona roho iliyopotea iliyokuwa katika shimo ilikuwa imefungiwa katika mifupa. "*Bwana wangu,*" nililia kwa kuona hali ile, "*Huwezi kuwafungulia wakatoka?*" *Lo, hali hii inasikitisha! Niliwaza, ningeliweza kuwa ndio mimi.* Nilisema, "*Bwana, angalia inavyosikitisha kuona kwamba mle ndani kuna roho inayoishi.*"

Nilisikia sauti ikitoka katikati ya shimo la kwanza. Niliona umbo kwa mfano wa mifupa (skeleton) ikilia, "*Yesu, nihurumie!*"

"*O, Bwana!*" Nilisema. Ilikuwa ni sauti ya mwanamke. Nilimwangalia na kutaka kumvuta kutoka kwenye shimo la moto. Hali yake iliniumba sana moyo.

Mifupa ya mwanamke iliyokuwa na na rangi ya zambarau na ukungu ndani ilikuwa inazungumza na Yesu. Nilimsilikiza kwa mshangao. Nyama iliyooza ilining'inia kwa vipande vipande kwenye mifupa yake, na ilipokuwa inaungua ilianguka chini ya shimo. Mahali ambapo awali palikuwa na macho palikuwa mashimo matupu. Hapakuwa na nywele.

Moto ulianza kwenye miguu yake kama moto mdogo na ukaendelea kukua ulipokuwa unapanda kwenye mwili. Ilionekana kama mwanamke Yule aliendelea kuungua tu, hata wakati moto umepungua sana. Kutoka ndani yake kabisa yalitoka mayowe na vilio vyatua kukata tamaa. "*Bwana, Bwana, nataka kutoka humu!*"

Alijaribu mara nyingi kumfikia Yesu. Nilimtazama Yesu, alikuwa na huzuni kubwa katika sura yake. Yesu aliniambia, "***Mwanangu, upo hapa pamoja nami ili kuujulisha ulimwengu kwamba malipo ya dhambi ni mauti, kwamba kuzimu ni halisi.***"

Nilimwangalia tena yule mwanamke, na mafunza yalikuwa yanatoka kwenye mifupa ya skeleton yake. Hayakudhurika na moto. Yesu aliniambia, "***Anafahamu na anayasikia mafunza hayo katika mwili wake.***"

"*Mungu mhurumie!*" Nililia moto ulipofikia kilele chake na ule uchomaji ulianza kwa mara nyingine. Kilio kikubwa na kwikwi kilitigisha mwanamke-roho. Alikuwa amepotea.

Hapakuwa na njia ya kutokea. “Yesu, kwanini yupo hapa?” Niliuliza kwa sauti ndogo, maana nilikuwa naogopa kwelli kweli.

Yesu aliniambia, “**Njoo.**”

Njia tuliyokuwa tunapita ilikuwa na mizunguko, ikizunguka kwenye mashimo haya kwa kadri ya upeo wa macho. Vilio vya wafu waishio, vikichanganyikana na mayowe, vilikuja kwenye masikio yangu kutoka kila upande. Hakukuwa na wakati wa utulivu kuzimu. Harufu nzito ya ya uozo wa nyama ilitapakaa hewani.

Tulifika kwenye shimo lingine. Ndani ya shimo hili, ambalo ukubwa wake ulikuwa sawa na lile lingine, kulikuwa na skeleton nyingine. Sauti ya mwanaume ililia kutoka shimoni, ikitisema, “*Bwana, nihurumie.*” Ni pale tu walipozungumza ndipo nilipoweza kujuu kama ni mwanaamke au mwanaume.

Vilio vikubwa vya mayowe vilitoka kwa mwanaume huyu. “*Nimekosa, Yesu, nisamehe. Nitoe humu. Nimekuwa mahali hapa pa mateso miaka mingi. Ninakusihu, nitoe.*” Kilio cha kwikwi kilitisa skeleton hii. “*Tafadhali Yesu, nitoe.*” Nilimtaza Yesu nikaona kwamba naye alikuwa analia.

“*Bwana Yesu,*” mtu huyo alilia kutoka shimo la moto, “*sijateseka vya kutosha kwa dhambi zangu? Imepita miaka arobaini tangu nilipokufa.*”

Yesu alisema, “**Imeandikwa, Wenye haki wataishi kwa imani!’ Wenye dhara wote na wote wasioamini watakuwa na fungu lao katika ziwa la moto. Hukutaka kuamini kweli. Mara nyingi watu wangu walitumwa kwako kukuonyesha njia, lakini hukuwasikiliza. Uliwacheka na uliikataa injili. Ingawaje nilikufa msalabani kwa ajili yako, ulinikebehi na hukutaka kutubu dhambi zako. Baba yangu alikupa fursa nyingi za kuokolewa. Heri ungelisikiliza.**” Yesu alilia.

“*Najua Bwana, Najua Bwana!*” Yule mtu alilia. “*Lakini sasa natubu.*”

“**Umechelewa,**” Yesu alisema. “**Hukumu imetolewa.**”

Yule mtu aliendelea, “*Bwana, baadhi ya watu wangu watakuja huku, kwa maana nao hawatatu. Tafadhali, Bwana, niruhusu niende nikawaambie kwamba ni lazima watubu dhambi zao wangali duniani. Sitaki waje huku.*”

Yesu alisema, “**Wanao wahubiri, waalimu, wazee wa kanisa-wote hao wanahubiri injili. Vile vile wana bahati ya kuwa na njia za kisasa za mawasiliano na njia nyingine nyingi za kujifunza kuhusu Mimi. Niliwapelekea watumishi ili waweze kuhubiriwa na kuokoka. Kama hawaamini wanaposikia injili, basi hawatasikia hata mtu akifufuka katika wafu.**”

Aliposikia hivi mtu yule alighadhabika sana akaanza kutukana. Maneno machafu, ya kufuru yakatoka kwake. Nilitazama kwa mshangao nilipoona moto ukipanda kwenye skeletoni na nyama iliyoza ikaanza kuungua na kudondoka. Ndani ya mifupa hii ya mtu, niliona roho yake. Ilikuwa kama ukungu wa zambarau, na ulijaza mifupa yake.

Yesu alisema, "**Kuzimu ni halisi, na hukumu ni halisi. Nawapenda sana , mwanangu. Huu ni mwanzo tu wa mambo ya kutisha nitakayokuonyesha. Kuna mambo mengi zaidi yanakuja. Uambie ulimwengu kwa niaba yangu kwamba kuzimu ni halisi, kwamba wanaume na wanawake lazima watubu dhambi zao. Njoo, nifuate. Lazima tusonge mbele.**"

Katika shimo lingine kulikuwa na mwanamke mdogo sana aliyejkuwa na umri wa labda miaka themanini. Siwezi kueleza namna nilivyojua umri wake lakini nilijua tu. Ngozi ilitolewa kwenye mwili wake kwa moto endelevu, ilibaki mifupa tu ikiwa na roho kama mvuke mchafu ndani yake. Niliangalia moto ulivyokuwa unamuunguza. Mara ilibaki mifupa tu na mafunza yakizunguka ndani, ambayo moto haukuweza kuyaunguza.

"*Bwana, inatisha!*" Nililia. " *Sijui kama naweza kuendelea, maana inavyotisha vigumu kuamini.*" Kwa kadri ya upeo wa macho yangu roho zilikuwa zinaungua kwenye mashimo ya moto.

" **Mwanangu, ndio maana upo hapa.**" Yesu alijibu. "**Nilazima ujue na uelezee ukweli wa kuzimu. Mbingu ni hakisi! Kuzimu ni halisi! Twende, hatuna budi kusonga mbele.**"

Niligeuka na kumtazama yule mwanamke. Vilio vyake vilikuwa vinasikitisha sana. Nilipomwangalia, aliiweka mifupa ya mikono yake kama kwamba anasali. Nilishindwa kujizuia kulia. Nilikuwa katika hali ya roho, na nilikuwa nalia. Nilijua kwamba watu wa kuzimu walikuwa na ufahamu wa aina hii pia.

Yesu aliyajua mawazo yangu. "**Ndio, mtoto,**" alisema, "**Wanafahamu. Watu wajopo hapa, wana ufahamu ule ule na mawazo kama walipokuwa duniani. Wanazikumbuka familia na marafiki wao na nyakati zote walipokuwa na nafasi ya kutubu lakini hawakutubu. Kumbukumbu iko pamoja nao wakati wote. Heri wangeliamini injili na kutubu bila kuchelewa.**"

Nilimwangalia yule mwanamke kwa mara nyingine, na safari hii nilligundua kwamba ana mguu mmoja tu. Na ilionekana kama mashimo yamechimbwa kwenye mifupa ya kiuno. "Hii ni kitu gani, Yesu?" Niliuliza.

Alisema "**Mtoto, alipokuwa duniani alikuwa na kansa na alikuwa katika maumivu makali. Upasuaji ulifanyika ili kuokoa maisha yake. Alilala akiwa mwanamke mwenye uchungu kwa miaka mingi. Watu wangu wengi walikwenda kumuombea na**

kumwambia kwamba naweza kumponya. Alisema, ‘Mungu ndiye amenifanya hivi’ na hakuweza kutubu na kuamini injili. Aliwahi hata kunijua wakati mmoja, lakini baadaye alikuja kunichukia. Alisema kwamba hamuhitaji Mungu na hakutaka mimi nimponye. Bado niliendelea kumbembeleza, nikitaka kumsaidia, nikitaka kumponya na kumbariki. Alinipa kisogo na kunilaani. Alisema alikuwa hanihitaji. Roho yangu ilimbembeleza. Hata baada ya kunipa kisogo, niliendelea kumvuta kwangu kwa Roho wangu, lakini hakutaka kusikia. Mwishoni alikufa na kuja hapa.

Yule mwanamke alimlilia Yesu, “Bwana Yesu, tafadhali nisamehe sasa. Nasikitika kwamba sikutubu nilipokuwa duniani. Kwa uchungu alimlilia Yesu, “Laiti ningelitubu bila kuchelewa. Bwana, nisadie, nitoe hapa. Nitakutumikia. Nitakuwa mtu mwema. Sijateseka vya kutosha? Kwanini nilisubiri mpaka nikachelewa? Oh, Kwanini nilisubiri mpaka Roho wako alipochoka kushindana nami?”

Yesu alimwambia, “**Ulikuwa na nafasi ya kutubu na kunitumikia.**”

Huzuni ilidhihirika kwenye uso wa Yesu alipoondoka mahali pale.

Yule mwanamke alivyokuwa analia, niliuliza, “*Bwana kinafuata nin?*”

Nilihisi hofu kila upande. Huzuni, vilio vya uchungu, na umauti vilitanda mahali pote. Yesu na mimi tulitembea kwa huzuni hadi shimo lingine. Niliweza kosogea mbele kwa sababu ya nguvu zake tu. Hata baada ya kitambo kirefu niliendelea kusikia vilio vya toba na msamaha vya yule mama. Nilitamani kuwa na namna ya kumsaidia. Mkosaji, usisubiri mpaka Roho wa Mungu anaacha kushindana na wewe.

Kwenye shimo lingine kulikuwa na mwanamke amepiga magoti, kama kwamba anatafuta kitu. Skeletoni yake ilikuwa na matundu mengi. Mifupa yake ilikuwa inaonekana, na nguo yake iliyokuwa imechanika ilikuwa imeshika moto. Kichwa chake hakikuwa na nywele, na kulikuwa na mashimo tu mahali ambapo palistahili kuwa na macho. Moto mdogo ulikuwa unawaka kuzunguka pale alipokuwa amepiga magoti, na aliparua kwa makucha pembe za kiberiti. Moto ulishikilia kwenye mikono yake, na nyama mfu iliendelea kudondoka kama mavi ya ng’ombe.

Kilio kikubwa kilimtikisa. “O Bwana, O Bwana,” alilia, “Nataka kutoka” Tulipozidi kuangalia hatimaye alifika mwisho wa shimo kwa miguu yake. Nilidhani angetoka ndipo pepo kubwa lenye mabawa makubwa yaliyoonekana kuvunjika juu na kuning’inia kwenye mabega llimkimbilia. Rangi yake ilikuwa zambarau nyeusi na alikuwa na minywele mwili mzima. Macho yake yalibonyea ndani ya kichwa, na umbo lake lilikuwa kama mbweha mkubwa. Yule pepo alimkimbilia yule mwanamke na kumsukumia kwenye shimo la moto kwa nguvu. Niliangalia kwa mshangao alipotumbukia. Nilimsitikikia. Nilitamani kumchukua katika mikono yangu na kumkumbatia, kumwomba Mungu amponye na kumtoa mle.

Yesu alitambua mawazo yangu na akasema, "**Mwanangu, hukumu imekwisha kutolewa. Mungu amesema. Hata alipokuwa mtoto nilimwita na kumuita ili anitumikie. Alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, nilimwendea na kusema, 'Nakupenda, nipe maisha yako na nifuate, kwa maana nimekuita kwa kusudi maalum: nilimwita maisha yake yote, lakini hakutaka kusikiliza. Alisema, 'Siku moja nitakutumikia. Kwa sasa sina muda na wewe. Sina muda, sina muda, nina maisha yangu ya starehe. Sina muda, sina muda wa kukutumikia Yesu. Kesho nitakutumikia.', Kesho haikufika, alichelewa'**"

Yule mwanamke alimlilia Yesu, "Roho yangu iko kwenye mateso hasa. Hakuna njia ya kutokea. Najua kwamba niliupenda ulimwengu badala ya kukupenda wewe, Bwana. Nilitaka utajiri, sifa, na mali, na nilivipata. Niliweza kununua chochote nilichokihitaji; nilikuwa bwana wangu mwenyewe. Wakati wangu nilikuwa mwanamke mzuri kupita wote, mwenye kujua kuva kuliko wote. Nilikuwa na utajiri, sifa na mali, lakini niligundua kwamba nisingweza kwenda navyo kaburini. O Bwana kuzimu kunatisha. Sina kupumzika mchana na usiku. Kila wakati niko kwenye mateso na maumivu. Nisaidie Bwana," alilia

Mwanamke alimwangalia Yesu kwa shauku na kusema, *Bwana wangu mwema, laiti ningekusikiliza. Nitajuta milele. Nilipanga kuja kukutumikia siku moja-nitakapokuwa tayari. Nilidhani ungelikuwapo kwa ajili yangu wakati wote. Kumbe nilikosea! Nilikuwa mmojawapo wa wanawake walikokuwa wanapendwa sana wakati wangu kwa sababu ya urembo wangu. Najua kwamba Mungu alikuwa ananiita ili nitibu. Wakati wa maisha yangu yote alinivuta kwa kamba za upendo, na nilidhani ningeweza kumtumia Mungu kamanilivyokuwa nawatumia wengine. Nilidhani angekuwapo wakati wote. Ndio, nilimtumia Mungu! Alijaribu sana kunifanya nimtumikie, ambapo wakati wote nilidhani simuhitaji. Kumbe nilikosea! Shetani alitumia urembo wangu na fedha zangu, na mawazo yangu yote yaligeukia kwenye nguvu ambazo angenipa. Hata hivyo Mungu aliendelea kunivuta. Lakini niliwaza, ipo kesho na kesho kutwa. Ndipo siku moja nilipokuwa kwenye gari dereva wangu aligonga nyumba, nikafa. Bwana, tafadhalii nitoe.*" Alipokuwa anazungumza mikono yake iliyokuwa mifupa mitupu ilijaribu kumshika Yesu wakati moto unaendelea kumchoma.

Yesu alisema, "**Hukumu imetolewa.**"

Machozi yalimdondoka tuliposogea kwenye shimo lingine. Nilikuwa nalia ndani kwa ndani juu ya uchungu wa kuzimu. "Bwana Mpandwa," nililia, "mateso haya ni halisi mno. Roho ikija huku hakuna matumaini, hakuna maisha, hakuna upendo. Kuzimu ni halisi mno." Hakuna namna ya kutoka, niliwaza. Lazima aungue milele kwenye moto huu.

"**Muda umekwisha,** "Yesu alisema. "**Tutakuja tena kesho.**"

Rafiki, kama unaishi katika dhambi tafadhali tubu. Kama umezaliwa mara ya pili lakini umempa Mungu kisogo, tubu na mrudie mara moja. Ishi vizuri na simamia kweli. Amka kabla hujachelewa, na unaweza kuwa na Bwana milele mbinguni.

Yesu alisema tena, "*Kuzimu ina mwili* (kama mwili wa mwanadamu) ***umelala chali katikati ya dunia. Kuzimu ina umbo kama la mwanadamu, kubwa sana na lenye vyumba vya mateso vingi sana. Kumbuka kuwaambia watu wa dunia kwamba kuzimu ni halisi. Mamilioni ya roho zilizopotea ziko huko, na nyingine zinakwenda huko kila siku. Siku ya Hukumu, kifo na kuzimu vitatupwa katika ziwa la moto, hiyo itakuwa mauti ya pili*"**

Sura ya 3

Mguu wa Kulia wa Kuzimu

Sikuweza kulala wala kula tangu nilipotoka kuzimu usiku uliopita. Kila siku kumbukumbu za kuzimu zilinijia. Nilipofumba macho; nilichokiona ni kuzimu tu. Masikio yangu hayakuweza kuzuia nisisikie kelele za waliolaaniwa. Mambo niliyoyaona kuzimu yalinijia mara kwa mara kama kwamba nilikuwa naangalia kipindi cha televisheni. Kila siku nilikuwa kuzimu, na kila siku nilikuwa natafuta namna ya kuueleza ulimwengu juu ya mambo haya ya kutisha.

Yesu alinitokea tena na kusema, "***Leo tunakwenda ndani ya mguu wa kushoto wa kuzimu, mwanangu. Usiogope, maana nakupenda na nipo pamoja nawe.***"

Uso wa Bwana ulikuwa na masikitiko, na macho yake yalijaa upole na upendo. Ingawaje waliokuwa kuzimu walikuwa wamepotea milele, nilijua kwamba bado alikuwa anawapenda na angewapenda milele.

"Mwanangu," Alisema, ***"Mungu, Baba yetu, alimpa kila mmoja wetu utashi ili kuchagua kumtumikia Yeye au Shetani. Unajua, Mungu hakuumba kuzimu kwa ajili ya watu wake. Shetani anawadanganya watu wengi wamfuate, lakini kuzimu kulitengenezwa kwa ajili ya Shetani na malaika zake. Sio mapenzi yangu, wala mapenzi ya Baba yangu, kwamba mtu yeyote apotee"*** Machozi ya huruma yalitiririka kwenye uso wa Yesu.

Alianza kusema tena, ***"Kumbuka maneno yangu katika siku za mbele nitakapokuonyesha kuzimu. Ninayo mamlaka yote mbinguni na duniani. Sasa, mara nyingine itakuwa kama nimekuacha, lakini sitakuacha. Kuna wakati tutaonekana na***

nguvu za giza, na wakati mwingine hazitatuona. Kokote tutakakokwenda, uwe na amani na usiogope kunifuata."

Tulikwenda pamoja. Nilimfuata kwa karibu nikilia. Kwa siku kadhaa nilikuwa nalia, na sikuweza kabisa kuuondoa uwepo wa kuzimu ambao wakati wote ulikuwa mbele yangu. Zaidi nililia ndani kwa ndani. Roho yangu ilikuwa na majonzi sana.

Tulifika kwenye mguu wa kulia wa kuzimu. Nilipotazama mbele niliona njia iliyokuwa kavu na imeungua. Vilio vilijaza hewa chafu, na harufu ya mauti ilikuwa kila mahali. Mara nyininge harufu ilikuwa mbaya kiasi cha kunifanya nijisikie kutapika. Kila mahali palikuwa giza isipokuwa mwanga uliokuwa unatoka kwa Kristo na mashimo ya moto, ambayo yalijaa kila mahali kwa kadri ya upeo wa macho.

Mara, mapepo ya kila aina yalianza kutupita. Vipepo vilitumulika vilipotupita. Mapepo ya kila ukubwa na umbile yalianza kusemezana. Mbele yetu, pepo kubwa lilikuwa linatoa amri kwa mapepo madogo. Tulisimama kusikiliza, na Yesu alisema, "**Vile vile kuna jeshi lisiloonekana hapa la nguvu za giza- kama vile mapepo ya magonjwa.**"

"*Nenda!*" Pepo kubwa liliviagiza vipepo vidogo. "*Kafanye mambo mengi maovu. Vunja familia. Washawishi Wakrsto dhaifu, na fundisha uongo na wapotoshe watu wengi kadri mtakavyoweza. Mtapata dhawabu yenu mtakaporejea. Kumbuka, jihadharini na wale waliompokea Yesu kuwa Mwokozi wao. Wana uwezo wa kuwafukuza. Nendeni sasa ulimwenguni pote. Ninao wengi kule na bado nitawapeleka na wengine. Kumbuka, sisi ni watumishi wa mfalme wa giza na nguvu za anga.*"

Baada ya hapo, nguvu za giza zilianza kutoka chini na kuruka juu hadi nje ya kuzimu. Milango juu ya mguu wa kulia wa kuzimu ilifunguka na kufungwa kwa kasi sana kuziruhusu hizo nguvu za giza kutoka nje. Zingine zilipanda juu na kutokea kwenye pango tuliloingilia.

Nitajitahidi kuelezea maumbile ya viumbe hivi. Aliyekuwa anazungumza alikuwa na umbo kubwa sana dubu mkubwa, rangi ya kikahawia, alikuwa na kichwa kama popo na macho yaliingia ndani sana ya uso wenyewe minywele. Mikono yenye minywele ilining'inia pembeni, na meno yalijitokeza kwenye nywele za uso wake.

Mwingine alikuwa mdogo kama nyani akiwa na mikono mirefu sana na nywele mwili mzima. Uso wake ulikuwa mdogo, na alikuwa na pua iliyochongoka. Sikuona macho juu ya mwili wake mahali popote.

Mwingine tena alikuwa na kichwa kikubwa, masikio makubwa na mkia mrefu, na mwingine alikuwa mkubwa kama farasi na ngozi laini. Maumbile ya mapepo haya mabaya yalinitia kichefuchefu. Kila nilikotazama kulikuwa na mapepo.

Kubwa kushinda yote ya mapepo haya yalikuwa yanapokea amri moja kwa moja kutoka kwa Shetani, ndivyo Bwana alivyoniambia.

Yesu na mimi tulitembea kwenye njia hadi tulipofika kwenye shimo lingine. Vilio vyatamaumivu, sauti za masikitiko zisizosahaulika, zilisikika kila mahali. Bwana wangu, nini zaidi? Niliwaza.

Tulitembea kuvipita baadhi ya viumbi hivi vibaya, ambavyo havikuelekea kutuona, na kusimama kwenye shimo lingine la moto na kiberiti. Katika shimo hili kulikuwa na mtu mwenye umbile kubwa. Nilimsikia akihubiri injili. Nilimtazama Yesu kwa mshangao nikisubiri jibu, maana wakati wote aliyajua mawazo yangu.. Alisema, "**Alipokuwa duniani mtu huyu alikuwa mhubiri wa injili. Wakati fulani alisema kweli na kunitumikia.**"

Nilishangaa, mtu huyu alikuwa anatafuta nini kuzimu? Alikuwa na kimo cha futi sita, na mifupa yake ilikuwa michafu, kijivu, kama jiwe la kaburi. Vipande vyatamaumivu na nguo vilimnin'ginia bado. Nilishangaa kwanini moto haukuunguza vipande hivi vyatamaumivu na nguo. Nyama iliyokuwa inaungua ilikuwa inamning'inia, na kichwa kilionekana kuwaka moto. Harufu mbaya ilitoka kwake.

Nilimwona amenyosha mikono yake kama kwamba ameshika kitabu na alianza kusoma Maandiko kutoka kitabu kisochokuwepo. Nilikumbuka tena Yesu alivyokuwa ameniambia.

Yesu alisema, "**Kuzimu unakuwa na ufaamu wako wote, na unakuwa mkubwa zaidi.**" Yule mtu alisoma Andiko hadi Andiko, na nilidhani ilikuwa vizuri. Yesu alimwambia yule mtu kwa upendo mwingi katika sauti yake, "**Amani, tulia.**" Mara moja mtu yule aliacha kusema, aligeuka taratibu kumwangalia Yesu.

Niliona roho ya mtu ndani ya mifupa hii. Alimwambia Bwana, "Bwana, sasa nitahubiri kweli kwa watu. Sasa, Bwana, niko tayari kwenda na kuwaambia wengine kuhusu mahali hapa. Najua kwamba nilipokuwa duniani nilikuwa siamini kwamba kuna kuzimu, wala sikuamini kwamba ungerudi tena. Ndivyo watu walivyotaka kusikia, sikutetea kweli. Najua kwamba sikumpenda yejote wa rangi au asili tofauti na mimi, na nilisababisha watu wengi kujitenga nawe. Nalitengeneza taratibu zangu mwenyewe kuhusu mbingu na kuhusu jambo gani ni sahihi na lipi si sahihi. Najua kwamba niliwapotosha wengi, na nilisababisha wengi kujikwaa kwa Neno lako Takatifu, na nilichukua fedha kutoka watu fukara. Lakini, Bwana, nitoe humu nami nitajirekebisha. Sitachukua tena fedha za kanisa. Nimetubu tayari. Nitawapenda watu wa kila aina na kila rangi."

Yesu alisema, "**Sio tu kwamba ulipindisha na kutoa tafsiri ya uongo ya Neno la Mungu, Bali ulidanganya kwamba hujui ukweli. Mimi mwenyewe nilikutembelea na kujaribu kukugeuza, lakini hukutaka kusikia. Ulikwenda njia yako mwenyewe, na ubaya ulikuwa ndio bwana wako. Uliiua kweli, lakini hukutaka, lakini hukutaka**

kutubu na kunigeukia. Nilikuwepo pale wakati wote. Nilikusubiri. Nilitaka utubu lakini hukutaka.”

Masikitiko yalikuwa kwenye sura ya Yesu. Nilijua kwamba mtu huyu angelisikia wito wa Mwokozi, asingekuwa hapa sasa. O nyie watu, tafadhali sikilizeni.

Yesu alisema tena na mkosaji “**Ulipaswa kusema kweli, na ungewageuza wengi kwenye haki kwa Neno la Mungu, ambalo linasema kwamba wote wasioamini sehemu yao ni katika ziwa linalowaka kwa moto na kiberiti. Ulijua njia ya msalaba. Ulijua njia ya haki. Ulijua kusema kweli. Lakini Shetani alijaza uongo kwenye moyo wako, na ukaingia katika dhambi. Ulistahili kutubu kwa moyo wa kweeli, sio nusu nusu. Neno langu ni kweli. Halisemi uongo.**” Baada ya kusikia hayo, mtu yule alinyosha mkono kwa Yesu kwa hasira, akaanza kumlaani.

Kwa huzuni, mimi na Yesu tuliondo kuelekea shimo lingine. Mhubiri aliyeanguka aliendelea kulaani na kumkasirikia Yesu. Tulipokuwa tunapita kwenye mashimo ya moto, mikono ya wapotevu ilinyooshwa kutka kumfikia Yesu, na kwa sauti ya kubembeleza waliita na kuomba rehema.

Mifupa ya mikono yao na miguu yao ilikuwa na rangi ya majivu meusi kutokana na kuungua- hakuna nyama yenyenye damu, hakuna viungo, ni mauti tu na kifo. Nilikuwa nalia ndani kwa ndani, *O dunia, tubu. Usipotubu utakuja hapa. Acha kabla hujachelewa.*

Tulisimama tena kwenye shimo lingine. Nilisikia huzuni mno kwa ajili yao wote kiasi cha kwamba nilijiona dhaifu katika mwili hata kusimama wima ilikuwa vigumu. Kilio cha kwikwi kilinitisa. “*Yesu, naumia sana ndani.*” Nilisema.

Kutoka ndani ya shimo sauti ya mwanamke ilisema na Yesu. Alisimama katikati ya moto, na ulimfunika mwili mzima. Mwili wake ulijaa mafunza na nyama mfu. Moto ulipokuwa unawaka kumzunguka, alinyosha mikono yake kwa Yesu akilia. “*Nitoe humu. Sasa nitakupa moyo wangu, Yesu. Nitawaeleza wengine habari za msamaha wako. Nitakushuhudia. Nakusihii, tafadhali nitoe*”

Yesu alisema, “**Neno langu ni kweli linasema kwamba watu wote lazima watubu na kuziacha dhambi zao na kuniomba niingie katika maisha yao kama wanataka kukwepa kuja hapa. Katika damu yangu kuna ondoleo la dhambi. Mimi ni mwaminifu na wa kweli ni nitawasamehe wote wanaokuja kwangu. Sitawatupa nje.**”

Aligeuka, alimwangalia mwanamke na kusema, “**Ungelinisikiliza na kuja kwangu na kutubu, ningelikusamehe.**”

Yule mwanamke aliuliza, Bwana, hakuna njia nyingine ya kutoka hapa?”

Yesu alimjibu kwa upole sana. “**Mwanamke,**” alisema, ***ulipewa nafasi nyingi za kutubu, lakini roho yako sugu haikutaka. Ulilija Neno langu kwamba waongo sehemu yao ni katika ziwa la moto***”

Yesu alinigeukia na kusema, “**Mwanamke huyu alikuwa na matendo ya dhambi na wanaume wengi, na alisababisha nyumba nyingi kuvunjika. Pamoja na hayo yote niliendelea kumpenda. Nilikwenda kwake sio kwa kumhukumu bali kwa ukombozi. Niliwatuma kwake watumishi wangu wengi ili atubu na kuacha njia zake mbaya, lakini hakutaka. Alipokuwa mwanamama kijana, nilimwita, lakini aliendelea kufanya maovu. Alifanya maovu mengi, bado ningelimsamehe kama angelikuja kwangu. Shetani alimwingia, akawa na uchungu na hakuweza kuwasamehe wengine. Alikwenda kanisani ili tu kuwatafuta wanaume. Aliwapata na kuwanasa. Angelinijia, dhambi zake zingelitakaswa zote kwa damu yangu. Upande mmoja alitaka kunitumikia, lakini huwezi kumtumikia Mungu na Shetani kwa wakati mmoja. Kila mmoja lazima aamue nani atakayemtumikia.**”

“Bwana,” Nililia, “*nipe nguvu za kuendelea*” Nilikuwa natetemeka tangu kichwa hadi miguu kwa sababu ya mateso ya kuzimu.

Yesu aliniambia, “**Amani, tulia**”

“*Nisaidie, Bwana*” Nililia. *Shetani hataki tujue ukweli kuhusu kuzimu. Nilikuwa sijawahi kufikiria kwamba kuzimu kungekuwa namna hii. Mpendwa Yesu, haya yataisha lini?*”

“Mwanangu,” Yesu alijibu, “**Baba peke yake ndiye anayejua mwisho utakavyokuwa.**” Alisema nami tena na kuniambia, “**Amani, tulia.**” Nguvu nyingi zilinijia.

Yesu na mimi tulitembelea mashimo mbalimbali. Nilitamani kumvuta kutoka kwenye shimo la moto kila mtu tuliyemkuta na kumkimbiza kwenye miguu ya Yesu. Nililia ndani kwa ndani. Niliwaza: sitaki watoto wangu waje huku.

Hatimaye, Yesu alinigeukia na kuniambia, “**Mwanangu, tutakwenda nyumbani kwako sasa. Kesho usiku tutarudi tena kwenye sehemu hii ya kuzimu.**”

Niliporudi nyumbani nililia na kulia. Wakati wa mchana picha ya kuzimu na mateso ya watu wa kule ilinijia. Nilimwambia kila mtu niliyekutana naye mchana habari za kuzimu. Niliwaambia kwamba mateso ya kuzimu hatasimuliki, ni vigumu kuamini.

Mnaosoma kitabu hiki, nawasihi, tafadhali, tubu dhambi zenu. Mwite Yesu na mwambie akuokoe. Mwite leo. Usingoje mpaka kesho. Kesho huenda isifike. Muda unakwisha haraka. Piga magoti usamehewe dhambi zako. Mpandane. Kwa ajili ya Yesu, iweni wapole na msameheane.

Kama umemkasirikia mtu msamehe. Hakuna hasira iliyio na uzito wa kutosha kukupeleka kuzimu. Uwe mtu wa kusamehe kama Kristo alivytousamehe dhambi zetu. Yesu ana uwezo wa kuvumiliana nasi tukiwa na moyo wa toba na atafanya damu yake isafishe dhambi zote. Wapende watoto wako, na wapende jirani zako kama unavyojipenda mwenyewe.

Bwana wa makanisa anasema, "**Tubu nawe utaokolewa!**"

Sura ya 4

Mashimo Zaidi

Usiku uliofufata mimi na Yesu tulikwenda tena ndani ya mguu wa kulia wa kuzimu. Niliona kama mwanzo upendo wa Yesu kwa roho zilizopotea zilizoko kuzimu. Na nilihisi upendo wake Yesu kwangu mimi na kwa wote walioko duniani.

"**Mtoto,**" Aliniambia, "**sio mapenzi ya Baba kwamba mtu yeyote apote. Shetani anawadanganya wengi, na wanamfuata. Lakini Mungu anasamehe. Ni Mungu wa upendo. Wangelimjia Baba kwa moyo wa kweli na kutubu, angeliwasamehe.**" Upole mwingi ulijaa uso wa Yesu alipokuwa anasema.

Tulipita tena kwenye mashimo ya moto na kuwaona watu wengi katika mateso kama nilivyoeleza mapema. "**Bwana wangu, Bwana wangu, mateso yalivyo makubwa!**" Niliwaza

Njia nzima mikono iliyokuwa inaungua ilitaka kumfikia Yesu. Kulikuwa na mifupa tu mahali ambapo nyama ingelikuwapo-nyama iliyooza ikining'inia katika vipande vipande. Ndani ya kila skeletoni kulikuwa na kitu kama roho ya moshi wa kikahawia imefungiwa ndani ya mifupa hii mikavu milele. Nilitambua kutokana na vilio vyao kwamba walikuwa wanausikia moto, mafunza, maumivu na hali ya kukata tamaa iliyowakabili. Na vilio vyao viliujaza moyo wangu masikitiko yasiyoelezeka. Laiti kama wangelisikiliza, niliwaza, wasingekuwa hapa.

Nilijua kwamba waliopotea kuzimu walikuwa na fahamu zao zote. Walikumbuka mambo yote ambayo waliwahi kuambiwa. Walijua kwamba hakukuwa na njia ya kutoka kuzimu na kwamba walikuwa wamepotea milele. Hata hivyo, bila matumaini bado walitumaini kwamba walipomwita Yesu kuomba awahurumie.

Tulisimama kwenye shimo lilioluata. Lilikuwa sawa kabisa na yale mengine. Ndani yake kulikuwa na umbo la mwanamke, nilitambua kwa sauti yake. Alimlilia Yesu amwokoe na moto.

Yesu alimwangalia yule mwanamke kwa upendo na kusema, “**Ulipokuwa duniani nilikuita uje kwangu. Nilikuomba uitengeneze roho yako usije ukachelewa. Nilikutembelea mara nyingi wakati wa usiku kukueleza juu ya upendo wangu. Nilikumbelea, nilikupenda, nilikuvuta kwangu kwa Roho wangu.**”

‘Ndio Bwana, ullisema, ‘nitakufuata. Kwa kinywa chako ulisema unanipenda, lakini moyo wako haukumainisha. Nilijua roho yako ilikokuwa. Mara nyingi niliwatuma watumishi wangu kwako kukuambia utubu dhambi zako na kunifuata, lakini hukutaka kunisikiliza. Nilitaka kukutumia wewe kuwashudumia wengine, kuwasaidia wengine kunifuata. Lakini uliitaka dunia sio mimi. Nilikuita, lakini hukutaka kunisikiliza, wala kutubu dhambi zako.’

Mwanamke yule alimwambia Yesu, “Unakumbuka, Bwana, namna nilivyokuwa nakwenda kanisani na nilivyokuwa mwanamke mzuri. Nilijiunga na kanisa. Nilikuwa msharika wa kanisa lako. Nilijua kwamba wito wako ulikuwa juu ya maisha yangu. Nilijua kwamba ilinipasa kutii wito kwa gharama yoyote ile, na nilitii.”

Yesu alisema, “**Mwanamke, bado umeja uongo na dhambi. Nilikuita, lakini hukutaka kusikia. Kweli, ulikuwa mshiriki wa kanisa, lakini kushiriki kanisani hakujafikisha mbinguni. Dhambi zako zilikuwa nyingi, hukutaka kutubu. Uliwasababisha wengine kukwazwa na Neno langu. Ulishindwa kuwasamehe wengine walipokuudhi. Ulijifanya kunipenda na kunitumikia ulipokuwa kati ya Wakristo, lakini ulipokuwa mbali na Wakristo ulilaghai, ulidanganya na kuiba. Ulizisikiliza roho zidanganyazo na ulifurahia maisha ya nduma kuwili. Uliijua njia pana na njia nyembamba.**

“Na” Yesu alisema, “**ulikuwa ndumila kuwili. Uliwasengenya dada zako na kaka zako katika Kristo. Uliwahukumu na kujifanya mtakatifu kuliko wao, wakati ulikuwa na dhambi kubwa ndani ya moyo wako. Hili najua, kwamba usingemsiliza Roho wangu wa upole. Uliwahukumu watu kwa kuwaangalia nje, bila kujali kwamba wengi walikuwa wachanga katika imani. Ulikuwa katili sana.**

“Ndio, ulisema unanipenda kwa midomo yako, lakini moyo wako ulikuwa mbali nami. Ulizifahamu njia za Bwana na ulizielewa. Ulicheza na Mungu na Mungu anajua mambo yote. Ungelimitumikia Mungu kwa uaminifu, usingelikuwa hapa leo. Huwezi kumtumikia Shetani na Mungu kwa wakati mmoja.”

Yesu alinigeukia na kusema, “**Katika siku za mwisho wengi wataiacha imani na kuzisikiliza roho danganyifu na kutumikia dhambi. Toka ndani yao, na jitenge.**

Usitembee njia moja na wao." Tulipoanza kuondoka, yule mwanamke alianza kumalaani Yesu. Alipiga kelele kwa hasira. Tuliendelea mbele. Nilikuwa dhaifu sana katika mwili.

Katika shimo lililofuata kulikuwa na skeletoni nyingine. Nilisikia harufu ya mauti hata kabla hatujafika. Mtu huyu alikuwa sawa na wengine.

Nilijiuliza roho hii imefanya nini hata kupotea na kutokuwa na tumaini, bila matumaini isipokwa umilele mahali hapa pa kutisha. Kuzimu ni milele. Niliposikia roho zikilia kwa mateso, nililia vile vile.

Nilisikiliza mwanamke mmoja alipokuwa anazungumza na Yesu kutoka kwenye shimo la moto. Alikuwa ananukuu Neno la Mungu. "Bwana Mpandwa, anafanya nini hapa?" Niliuliza.

"Sikiliza," Yesu alisema.

Mwanamke alisema, "Yesu ni Njia, Kweli na Uzima. Mtu haji kwa Baba bila kupitia kwake. Yesu ni nuru ya Ulimwengu. Njoo kwa Yesu naye atakuokoa."

Alipozungumza, roho nyingi zilizopotea zilimsikiliza. Nyingine ziliapa na kumlaani. Nyingine zilimwambia kunyamaza. Nyingine zilisema, "hivi kweli kuna tumaini?" au "Tusaidie Yesu." Vilio vya huzuni kubwa vilijaa hewani.

Sikuelewa kitu gani kilikuwa kinatokea. Sikujua kwanini mwanamke yule alikuwa akihubiri injili hapa.

Bwana aliyajua mawazo yangu. Alisema, "**Mtoto, nilimwita mwanamke huyu akiwa na umri wa miaka thelathini kuhubiri Neno langu na kuwa shahidi wa injili. Nawaita watu tofauti kwa ajili ya makusudi mbalimbali katika Mwili wangu. Lakini kama mwanaume au mwanamke, mvulana au msichana hamtaki Roho wangu, nitaondoka.**

"Ndio, alijibu wito wangu kwa miaka mingi, na alikuwa katika kumjua Bwana. Alikuja kuitambua sauti yangu, na alitenda mambo mengi mema kwa ajili yangu. Alijifunza Neno la Mungu. Aliomba mara nyingi, na maombi mengi yalijibowi. Aliwafundisha watu wengi njia ya utakatifu. Alikuwa mwaminifu katika nyumba yake

"Miaka ilikwenda hata siku moja aligundua kwamba mume wake alikuwa anatembea na mwanamke mwingine. Ingawaje alimwomba msamaha, alikuwa na hasira na hakutaka kumsamehe na kuokoa ndoa yao. Kweli, mume wake alikosea, na alifanya dhambi kubwa.

"Lakini mwanamke huyu alilifahamu Neno langu. Alijua kusamehe, na alijua kwamba kila jaribu lina njia ya kutokea. Mume wake alimwomba amsamehe.

Alikataa. Badala yake hasira iliota mizizi. Hakutaka kuileta kwangu. Hasira iliongezeka kila siku na alisema moyoni mwake, “Nipo hapa namtumikia Mungu kwa moyo wote, na mume wangu anatembea na mwanamke mwingine! ‘je hiyo ni sawa’ aliniuliza.

“Hapana sio sawa. Lakini alikuja na kuomba msamaha na kusema kwamba asingerudia tena.

“Nilimwambia, ‘Binti, jikague mwenyewe, uone kama sio wewe mwenyewe uliyesababisha haya’

“Sio mimi Bwana,” alisema, mimi ni mtakatifu, yeye ndiye mkosaji.’ Hakutaka kunisikiliza.

“Muda ulizidi kwenda. Hakuweza kuniomba au kusoma Biblia. Alikuwa na hasira si kwa muwe wake tu, bali na kwa wale waliomzunguka. Alinukuu Maandiko, lakini hakuweza kumsamehe.

“Hakutaka kunisikiliza. Moyo wake ullizidi kuwa na uchungu, na dhambi kubwa ilimwigia. Uuji uliingia katika moyo wake mahali ambapo zamani palikuwa na upendo. Na siku moja, katika hasira yake alimuua mume wake na yule mpenzi wa mume wake. Shetani alimwingia kabisa akajua.”

Niliitazama roho ile iliyokuwa imepotea na kumwacha Kristo na kuhukumiwa moto na mateso milele. Nilisikiliza alivyomjibu Yesu. “Sasa nitasamehe Bwana,” alisema. “Nitoe huku. Sasa nitakutii. Ona Bwana, sasa nahubiri Neno lako. Baada ya saa moja mapepo yatakuja na kunitesa zaidi. Yatanitesa kwa masaa mengi. Kwa sababu nilikuwa nahubiri Neno lako mateso yangu ni makubwa zaidi. Tafadhali, Bwana, nakuomba unitoe.”

Nililia pamoja na yule mwanamke aliyekuwa katika shimo na kumwomba Bwana aniepushe na machungu yote ya moyo. “Usiruhusu chuki iingie katika moyo wangu, Bwana Yesu.” Nilisema

“Haya, tuendelee mbele.” Yesu alisema.

Katika shimo lingine kulikuwa na mwili wa mwanaume, akilia, “Bwana,” alilia, “nisaidie kuelewa kwanini nipo hapa.”

Yesu alimwambia. **“Amani, tulia. Utaelewa kwa nini upo hapa.”**

“Nitoe, nami nitakuwa mtu mzuri.” Yule mtu aliomba.

Yesu alimjibu, **“Hata kuzimu bado unadanyanya.”**

Ndipo Yesu aliponigeukia na kusema, “**Mtu huyu alikuwa na miaka 23 alipokuja hapa. Hakutaka kusikiliza injili yangu. Alisikia Neno langu mara nyingi na mara nyingi alikuwa katika nyumba yangu. Nilimvuta kwa Roho wangu aingie katika wokovu, lakini aliipenda dunia na tama zake. Alipenda kunywa na hakutaka kusikia wito wangu. Alilelewa kikanisa lakini hakutaka kujitoa kwangu. Siku moja aliniambia, “siku moja nitatoa maisha yangu kwako, Yesu.” Siku hiyo haikufika. Usiku mmoja, baada ya sherehe, alipata ajali mbaya ya gari akafa. Shetani alimdanganya mpaka mwisho.**

“Aliuawa pale pale. Alipuuza wito wangu. Watu wengine vile vile walikufa kwenye ajali ile. Kazi ya Shetani ni kuua, kuiba na kuharibu. Laiti kama kijana huyu angelinisikiliza! Sio mapenzi ya Baba kwamba mtu ye yote apote. Shetani alikuwa anaitaka roho ya mtu huyu, na aliiharibu kupidia kutokujijali, dhambi na vinywaji vikali. Nyumba zinaharibiwa kila mwaka kwa sababu ya pombe.”

Laiti watu wangetambua kwamba tamaa za dunia ni zakitambo tu! Ukija kwa Yesu atakuokoa na vinywaji vikali. Mwite Yesu, atakusikia na kukusaidia. Atakuwa rafiki yako. Kumbuka kwamba anakupenda, na kwamba anao uwezo wa kusamehe dhambi zako.

Wakristo wenye ndoa, Yesu anawaonya kwamba msizini. Ukimtamani mtu wa jinsia tofauti na yako, hata kama hujakutana naye kimwili, ni uzinzi moyoni mwako.

Vijana, kaa mbali na madawa ya kulevyia na ngono. Ukitenda dhambi Mungu atakusamehe. Mwite sasa wakati nafasi ipo. Watafute Wakristo wakubwa, waulize kama mnaweza kujadiliana juu ya matatizo yako. Utashukuru kwamba ulipata muda sasa katika ulimwengu huu kabla hujachelewa.

Shetani anakuja kama malaika wa nuru kuudanganya ulimwengu. Ndio maana dhambi za ulimwengu huu zilionekana kuvutia kwa kijana huyu, ingawaje alilijua Neno Takatifu la Mungu. Sherehe moja zaidi, aliwaza, Yesu ataelewa bwana. Lakini kifo hakina huruma. Alingojea mno.

Niliitazama roho ya mtu yule, nilikumbushwa juu wa watoto wangu. “Oh Mungu, ebu waokoe.” Najua kwamba wengi mnaosoma haya mna watoto wenu, labda watoto, ambao hamtaki waende kuzimu. Waambie habari za Yesu wakati muda upo bado. Waambie watubu dhambi zao na Mungu atawasamehe na kuwatakasa.

Vilio vyia yule mtu vilinisumbua moyoni mwangu siku nyingi. Sitasahau kamwe vilio vyake vyia majuto. Nakumbuka nyama yamwili wake ikining’nia na kuungua katika moto. Sitasahau uozo, harufu ya mauti, mashimo mahali ambapo palikuwa na macho, roho chafu ya kijivu na mafunza yaliyokuwa yanapita kwenye mifupa. Mikono ya skeletoni ya yule mtu aliinyosha kwa Yesu akimsihi huku tukielekea kwenye shimo lingine.

"Bwana Mpendwa,' niliomba, "nipe nguvu za kuendelea."

Nilisikia sauti ya mwanamke ikilia kwa kutapatapa. Vilio vya wafu vilikuwa kila mahali.

Kisha tulifika kwenye shimo alimokuwemo yule mwanamke. Alikuwa anaomba kwa roho yake yote Yesu amtoe kule. *"Bwana,"* alisema, *"Sijakaa huku vya kutosha? Mateso yangu ni zaidi ya ninavyoweza kuvumilia. Nakuomba, Bwana, nitoe."* Kilio cha kwikwi kilitikisa mwili wake, na kulikuwa na maumivu hata katika sauti yake. Nilijua kwamba alikuwa anateseka kweli kweli.

Nilisema, *"Yesu, huwezi kufanya lolote?"*

Yesu alizungumza na yule mwanamke. *"Ulipokuwa duniani,"* alisema, *"nilikuita na kukuita uje kwangu. Nilikuhimiza urekebishe moyo wako, uwasamehe wengine, utende yaliyo sawa, kaa mbali na dhambi. Hata usiku wa manane nilikutembelea na kukuvuta kwangu kwa Roho wangu. Kwa midomo yako ulisema unanipenda, lakini moyo wako ulikuwa mbali nami. Hukujua kwamba hakuna kitu ambacho kimefichika kwa Mungu? Uliwadanganya wengine, lakini usingeweza kundanganya mimi. Bado niliwapeleka wengine wakwambie utubu, lakini hukusikia. Hukutaka kusikia, hukutaka kuona, na katika hasira uliwafukuza. Nilikuweka mahali ambapo ungeweza kusikia Neno langu, lakini hukutaka kutoa roho yako kwangu."*

"Hukusikitika, wala hukuona aibu kwa yale uliyokuwa unayafanya. Uliufanya moyo wako kuwa mgumu na ulinipa kisogo. Sasa umepotea milele. Ulipaswa kunisikiliza."

Kwa kusikia haya, alimtaza Yesu na kuanza kumlaani Mungu. Nilihisi uwepo wa roho chafu na nilijua kwamba ndizo zilizokuwa zinalaani na kuapa. Inasikitisha kweli kupotea milele kuzimu. Mpinge Sheatani wakati unaweza, na atakukimbia.

Yesu alisema, *"Dunia na vyote vilivyomo vitapita, lakini maneno yangu hayatapita."*

Sura ya 5

Pango la Hofu

Nilijaribu kukumbuka mahubiri niliyowahi kusikia kuhusu kuzimu. Lakini sikuwahi kusikia mambo ya kutisha kama ambayo Bwana alikuwa ananionyesha hapa. Kuzimu kulikuwa kubaya mno kuliko mtu yejote anavyoweza kudhani au kuwaza. Iliniumiza sana kujua kwamba roho zilizokuwa zinateseka kuzimu zitakuwa kule milele. Hakuna namna ya kutoka.

Nimedhamiria kwamba nitafanya kila linalowezekana lililo katika uwezo wangu kuziponya roho na mateso haya. Ni lazima nimhubirie kila ninayekutana naye, maana kuzimu ni mahali pa kutisha, na hii ni taarifa ya kweli. Unaelewa ninachosema? Kama wenye dhambi hawatatubu na kuiamini injili, kwa vyovoyote vile wataishia kuzimu.

Mwamini Bwana Yesu Kristo, na mwite akuokoe na dhambi. Soma sura ya 3 na ya 14 ya Injili ya Yohana. Halafu tafadhali soma kitabu hiki toka mwanzo hadi mwisho ili uelewe zaidi habari za kuzimu na maisha ya baadaye. Unapoendelea kusoma mwombe Yesu aingie katika moyo wako na asafishe dhambi zako usije ukachelewa.

Yesu alitembea kuelekea kuzimu. Njia ilikuwa umeungua, kavu, imepasukapasuka na yenye ukiwa. Niliona mistari ya mishimo mpaka mwisho wa upeo wa macho. Nilichoka sana. Moyo wangu, na roho yangu ilivunjika kutohana na yale niliyoyaona na kuyasikia, na hata hivyo nilijua kwamba mengi yalikuwa yananisubiri mbele.

“Yesu, nipe nguvu za kuendelea,” nililia.

Yesu alitangulia, nami nilimfuata nyuma kwa karibu. Nilijaa huzuni kwa ajili ya mambo ambayo nilikuwa nimeyaona. Nilikuwa najiuliza kimoyomoyo kama walimwengu watanisadiki. Nilitazama kulia kwangu na kushoto kwangu na nyuma yangu-kulikuwa na mashimo ya moto kwa kadri ya upeo wa macho yangu. Nilizungukwa na moto, na roho zinazoungua. Nililia kwa uchungu mwingi. Utisho na ukweli wa mambo ambayo nilikuwa nayaona yalikuwa makubwa mno kwangu kuyabeba.

“O dunia tubu,” nililia. Kwikwi za kilio zilitikisa mwili wangu nilipoendelea kutembea na Yesu. Nilikuwa najiuliza kitu gani kitafuata. Nilikuwa natakakari kwamba sijui familia yangu na ndugu zangu walikuwa wanafanya nini. Lo, nilikuwa nawapenda kwelikweli! Nilikumbuka jinsi nilivyokuwa nafanya dhambi kabla sijarejea kwa Bwana Yesu, na nilimshukuru Mungu kwamba nilirejea wakati muda ulikuwepo bado.

Yesu alisema, “**Sasa tunataka kuingia katika pango ambalo litatupeleka ndani ya tumbo la kuzimu. Umbo la kuzimu ni kama mwanadamu aliyelala katikati ya dunia.**

Mwili umelala chali, mikono na miguu imenyooka. Jinsi nilivyo na mwili wa waumini, ndivyo kuzimu kulivyo na mwili wa dhambi na mauti. Kama vile mwili wa Kristo unavyojengeka kila siku, ndivyo hivyo hivyo mwili wa kuzimu unavyojengeka kila siku.

Tulipokuwa tunakwenda kwenye pango, tulipita kwenye mashimo ya moto na vilio vya waliohukumiwa vilikuwa vinasikika. Wengi walimwita Yesu tulipokuwa tunapita. Wengine walijaribu kupanda kutoka kwenye mashimo ya moto ili kumfikia, lakini hawakuweza. Mmechelewa, mmechelewa, roho yangu ililia.

Uso wa Yesu ulijaa masikitiko tulipokuwa tunatembea. Nilipoyatazama mashimo ya moto nilikumbuka jinsi tulivyokuwa tunapika kutumia mkaa nyuma ya nyumba yetu na jinsi makaa yalivyokuwa yanawaka kwa masaa mengi kwa rangi nyekundu. Ndivyo nilivyoona kuzimu.

Nilishukuru tulipoingia kwenye pango. Niliwaza, pangoni hamuwezi kuwa pabaya kuliko mashimo ya moto. Kumbe!

Mara tulipoingia ndani nopianza kuona manyoka makubwa, panya wakubwa, na roho wachafu wengi, wote wakikimbia kutoka kwenye uwepo wa Mungu. Nyoka walitupigia mirusi na panya walipiga kelele. Kulikuwa na kelele nyingi mbaya. Nyoka wakali na vivuli vyeusi vilituzunguka. Yesu alikuwa ndio mwanga pekee ulioonekana katika pango. Nilikaa karibu sana na Yesu.

Mapepo yalikuwa pande zote za pango, na yalikuwa yanakwenda mahali fulani juu na nje ya pango. Baadaye nilitambua kwamba mapepo haya yalikuwa yanakwenda duniani kufuata maagizo ya Shetani.

Akihisi hofu yangu ya mahali hapa penye giza, unyevunyevu na uchafu, Yesu alisema, “***Tutafika mwisho wa pango hivi karibuni. Lazima nikuonyeshe mambo haya. Njoo, nifuate.***”

Majoka makubwa yalitambaa kuititia tulipokuwapo. Majoka mengine yalikuwa na ukubwa wa futi nne, na urefu wa futi ishirini na tano. Kulikuwa na hewa chafu, nzito, na pepo wachafu walikuwa kila mahali.

Yesu alisema, “***Tutafika sasa hivi kwenye tumbo la kuzimu. Sehemu hii ya kuzimu ina kimo cha maili kumi na saba na maili tatu kuzunguka, kama duara.***” Yesu alinipa vipimo kamili.

Nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuandika na kusimulia yote niliyoyaona na kusikia. Nitafanya kwa utukufu wa Baba, utukufu wa Mwana na utukufu wa Roho Mtakatifu. Mapenzi ya Mungu yafanyike.

Nilijua kwamba Yesu alikuwa ananionyesha mambo yote haya ili niwaonye wanaume na wanawake wa dunia kuiepuka kuzimu kwa gharama yoyote ile. Mpendwa, kama unasoma haya na bado humfahamu Yesu, acha kila kitu, tubu dhambi zako, na mwalike awe Mkombozi wako.

Sura ya 6

Matendo Katika Kuzimu

Mbele yetu niliona mwanga hafifu. Yesu na mimi tulitoka kwenye pango la kutisha na tulisimama kukabiliana na tumbo la kuzimu. Niliona, kwa kadri ya upeo wa macho, shughuli nyingi zikifanyika katikati mwa kuzimu.

Tulisimama, na Yesu alisema. “**Ninakwenda kukupitisha kwenye tumbo la kuzimu, na nitakufunulia mambo mengi. Njoo, nifuate.**” Sisi wawili tulitembea kuelekea mbele.

Yesu alisema, “**Mbele yetu kuna mambo mengi ya kuogofya. Sio hisia za mtu fulani, ni mambo ya kweli. Hakikisha unawajulisha wasomaji wako kwamba nguvu za mapepo ni halisi. Waambie kwamba Shetani ni halisi, na nguvu za giza ni halisi. Waambie wasikate tamaa, maana ikiwa watu wangu walioitwa kwa Jina langu watajinyenyewekeza na kuomba na kuacha njia zao mbaya, nitawasilikiliza kutoka mbinguni na kuiponya nchi yao na mili yao. Jinsi vile ambavyo mbinguni ni halisi , ndivyo kuzimu kulivyo halisi ”**

Mungu anataka ujue habari za kuzimu, na anataka akuokoe usiende kuzimu. Mungu anataka ujue kwamba kuna njia ya kutokea, na njia hiyo ni Yesu Kristo, Mwokozi wa roho yako. Kumbuka, ni wale tu amba majina yao yameandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana Kondoo ndio watakaoookoka.

Tulifika kwenye shughuli ya kwanza katika tumbo la kuzimu. Ilikuwa kulia kwa pale tulipoingilia na juu ya kilima kidogo kwenye kona ya giza ya kuzimu.

Nilikumbuka maneno ya Bwana aliponiambia, “**Mara nyingine nitakuwa kama nimekuacha, lakini sitakuacha. Kumbuka kwamba nina mamlaka yote mbinguni na duniani. Wakati mwingine mapepo na roho zilizopotea hazitatuona au kujua kwamba tupo hapa. Usiogope. Unachokwenda kuona ni halisi. Mambo haya yanatokea sasa hivi na yataendelea kutokea mpaka kifo na kuzimu vitakapotupwa katika ziwa la moto.”**

Msomaji, hakikisha kwamba jina lako limeandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana Kondoo.

Mbele yetu nilisikia sauti na vilio vya roho ikiwa kwenye mateso. Tulipanda kilima na kuangalia. Mwangaza ulikuwepo kwa hiyo niliweza kuona waziwazi, vilio ambavyo huwezi kudhania kuwa vinaweza kuwepo vilijaza anga. Vilikuwa vilio vya mwanaume.

“**Nisikilize**,” Yesu alisema. “**Unachokwenda kusikia ni kweli. Jihadharini enyi wahubiri wa injili, maana haya ni maneno ya uaminifu na kweli. Amkeni wainjilisti, wahubiri, na waalimu wa neno langu, nyie wote ambao mmeitwa kuhubiri injili ya Bwana Yesu Kristo. Kama unafanya dhambi tubu, la sivyo utaangamia vile vile.**”

Tulitembea hadi futi kumi na tano kutoka shughuli hii. Niliviona viumbe vidogo vimevaa nguo nyeusi vikittembea kuzunguka kitu kama sanduku. Baada ya kuchunguza zaidi niliona kwamba sanduku lile lilikuwa jeneza na viumbe vilivyokuwa vinazunguka vilikuwa mapepo. Lilikuwa jeneza la kweli, na kulikuwa na mapepo kumi na mawili yakitembea kulizunguka. Walikuwa wanalizunguka jeneza wakiimba na kucheka. Kila mmoja alikuwa na mkuki mkali mkononi mwake, ambao alikuwa akichoma kwenye jeneza kuitia vitundu vidogo.

Kulikuwa na hali ya hofu kuu hewani, na nilitetemeka nilipoona yaliyokuwa mbele yangu.

Yesu aliyatambua mawazo yangu, kwa maana alisema, “**Mtoto, kuna roho nyingi zikiwa kwenye mateso hapa, na kuna aina nyingi za mateso kwa ajili ya roho hizi. Kuna adhabu kubwa zaidi kwa wale ambao walikuwa wahubiri wa injili halafu wakaanguka katika dhambi, au ambao hawakuitikia wito wa Mungu katika maisha yao.**”

Nilisikia kilio kilichoujaza moyo wangu na hali ya kukata tamaa. “Hakuna tumaini, hakuna tumaini!” aliita. Kilio hiki cha kukata tamaa kilitoka kwenye jeneza. Ulikuwa mlion mfululizo wa kukata tamaa.

“Mungu, inasikitisha kweli!” Nilisema.

“**Njoo.**” Yesu alisema, “**Twende karibu zaidi.**” Baada ya kusema hayo alisogea karibu na jeneza na kutazama ndani. Nami nilifuata, nikatazama ndani. Ilionekana kwamba wale pepo wachafu walikuwa hawatuoni.

Ukungu mchafu wa kikahawia ulijaza jeneza. Ilikuwa roho ya mtu. Mapepo walichoma mikuki yao ndani ya jeneza huku nikiangalia.

Sitasahau kamwe kuteseka kwa roho hii. Nilimlilia Yesu, “**Mtoe Bwana, mtoe.**” Mateso ya roho yake yalikuwa ya kusikitisha. Laiti kama angelitoka. Nilimvuta mkono Yesu na kumwomba amtoe mtu yule kwenye jeneza.

Yesu alisema, “**Mwanangu, amani, tulia.**”

Yesu aliposema hivyo, yule mtu alituona. Alisema, “*Bwana, Bwana, nitoe. Nihurumie.*” Nilitazama ndani ya jeneza na kuona roho. Ndani ya roho kulikuwa na moyo wa mwanadamu, na damu ilibubujika kutoka kwenye moyo huo. Kule kuchomwa mikuki kulikuwa kunaichoma roho yake.

“*Sasa nitakutumikia Bwana.*” Alisihi, “*Nakuomba nitoe.*” Nilijua kwamba mtu huyu alisikia uchungu wa kila mkuki uliomchoma.

“**Anateswa usiku na mchana.**” Bwana alisema, “**Aliwekwa hapa na Shetani, na Shetani ndiye anayemtesa.**”

Yule bwana alilia, “Bwana, sasa nitahubiri injili ya kweli. Nitahubiri juu ya dhambi na kuzimu. Lakini nakuomba nitoe hapa.”

Yesu alisema, “**Mtu huyu alikuwa mhubiri wa Neno la Mungu. Kuna wakati alinitumikia kwa moyo wake wote na kuwaongoza wengi kwenye toba. Baadhi ya watu waliookolewa wanantumikia hadi leo, na miaka mingi imepita. Tamaa ya mwili na udanganyifu wa mali ulimpotosha. Alimruhusu Shetani amtawale. Alikuwa na kanisa kubwa, gari zuri na kipato kizuri. Alianza kuiba sadaka. Alizungumza zaidi nusu uongo na nusu kweli. Hakutaka nimsahihishe. Nilimpelekea wajumbe wangu kumwambia atubu na kuhubiri kweli, lakini alipenda zaidi anasa za dunia hii kuliko maisha ya Mungu. Alijua kutokufundisha au kuhubiri ukweli wowote isipokuwa ule uliuofunuliwa katika Biblia. Lakini kabla hajafa alisema kwamba ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa ni uongo na wale waliosema kuwa wanaye Roho Mtakatifu walikuwa wanafiki. Alihubiri kwamba unaweza kuwa mlevi na ukaenda mbinguni, hata bila kutubu.**

“**Alisema kwamba Mungu asingempeleka mtu ye yeyote kuzimu – kwamba Mungu alikuwa mwema sana asinge fanya hivyo. Alisababisha watu wengi kukosa neema ya Bwana. Hata alisema hanihitaji, kwa sababu alikuwa kama Mungu. Alikwenda hadi kiasi cha kuendesha semina kufundisha mafundisho haya ya uongo. Alilikanyaga Neno langu takatifu chini ya miguu yake. Hata hivyo, niliendelea kumpenda.**

“**Mwanangu, heri kutokunija kabisa kuliko kunijua halafu ukageuka na kuacha kunitumikia,**” Bwana alisema

“*Heri kama angelikusikiliza, Bwana!*” Nililia. “*Heri kama angejali roho yake na roho za watu wengine.*”

“Hakunisikiliza. Nilipokuwa namwita hakusikia. Alipenda maisha ya raha. Nilimwita na kumwambia atubu, lakini hakutaka kunirudia. Siku moja aliuawa na akaja hapa moja kwa moja. Sasa Shetani anamtesa kwa sababu aliwahi kuhubiri Neno langu na kuwaokoa watu wengi kwa ajili ya ufalme wangu. Haya ndio mateso yake.”

Niliangalia mapepo yalivyozidi kuzunguka jeneza. Moyo wa mtu yule ulidunda na damu ya kweli ilichirika. Sitasahau kamwe kilio chake cha maumivu na huzuni.

Yesu alimtazama yule mtu kwenye jeneza kwa huruma kubwa na kusema, “**Damu ya roho nyingi zilizopotea iko kwenye mikono ya mtu huyu. Wengi wao wamo katika mateso hivi sasa.**” Kwa mioyo ya huzuni mimi na Yesu tulisogea mbele.

Tulipokuwa tunaondoka, niliona kundi lingine la mapepo likienda kwenye jeneza. Yalikuwa na urefu wa kama futi tatu, yamevaa nguo nyeusi, na vitambaa vyeusi kuziba nyuso zao. Walikuwa wanabadilishana zamu kuitesa roho hii. Tunakataa kutubu na kujishusha, utadhani sisi tu ndio tuko sawa wakati wote. Lakini sikiliza, roho, kuzimu ni halisi. Tafadhalii sana usiende mahali kule.

Ndipo Yesu aliponionyesha saa kubwa, imeujaza ulimwengu wote. Niliisikia ikienda tik tak tik tak. Mshale wa saa ulikuwa unakaribia majira ya saa sita, na mshale wa dakika ulikwenda mbio na kusimama dakika tatu kabla ya saa sita. Taratibu mshale wa dakika ulisogelea saa sita kamili. Ulipokuwa unasogea mbele mlion wa saa uliongezeka mpaka ukaonekana kama unaijaza dunia nzima.

Mungu alizungumza kama tarumbeta, na sauti yake kama ya maji mengi. “**Sililiza ambayo Raho ayaambia makanisa,” alisema. “Iweni tayari, maana kwa wakati msiodhania, nitakuja tena. Nasikia saa ikilia. Ni saa sita. Bwana harusi amekuja kwa ajili ya bibi harusi wake”**

Je uko tayari kwa ajili ya kuja kwa Krsito, rafiki yangu? Au uko sawa na wale wanaosema, “*Sio leo, Bwana?*” Je unaweza kumwita ili uokolewe? Je unaweza kumpa roho yako leo? Kumbuka, Yesu anaweza kukuokoa kutoka maovu yote kama utamwita leo, na kutubu. Omba kwa ajili ya familia yako na wapendwa wako ili wamwendee Yesu wasije wakachelewa.

Sikiliza Yesu anavyosema, “**Nitakulinda na mabaya. Nitakuchunga katika njia zako zote. Nitakuokoa. Nitawakoa unaowapenda. Niite leo upate kuishi.**”

Kwa machozi mengi ninaomba kwamba nyie wote mnao soma kitabu hiki mtajua kweli bila kuchelewa. Kuzimu ni milele. Ninajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuyaeleza yote niliyoyaona na kusikia. Najua mambo haya ni kweli. Unapoendelea kusoma sehemu inayobaki ya kitabu hiki, ninaomba kwamba utatubu na kumchukua Yesu kuwa Mwokozi wako binafsi.

Nilisikia Bwana akisema, “**Ni wakati wa kuondoka. Tutarudi tena kesho.**”

Sura ya 7

Tumbo la Kuzimu

Usiku uliofuata Yesu na mimi tulikwenda kuzimu tena. Kwanza tuliingia kwenye sehemu kubwa ya wazi. Kwa kadri ya upeo wa macho yangu, vitendo viovu vilikuwa vikiendelea. Vingi ya vitendo hivi vilikuwa vinafanyika maeneo yaliyotuzunguka. Kama futi kumi hivi kutoka mahali tulipokuwa timesimama , niliona kitu cha pekee, cha pekee kwa sababu viumbe viovu na pepo wachafu waliingia na kutoka kwa haraka mahali pale.

Ilikuwa kama sinema ya kutisha. Kwa kadri ya upeo wa macho yangu, roho zilikuwa katika mateso, na ibilisi na malaika zake walikuwa kazini. Ile hali ya giza giza ilijaa kelele za uchungu na kukata tamaa.

Yesu alisema, “**Mtoto, Shetani ni mdanganyaji duniani na mtesi wa roho kuzimu. Nguvu za kipepo unazoziona hapa mara ingine huenda duniani kuumiza, kusababisha mateso na kudanganya. Nakwenda kukuonyesha mambo ambayo hayajawahi kuonekana kwa undani namna hii. Baadhi ya mambo utakayoyaona yatakuwa yanatokea hivi sasa, na baadhi ya mambo yatatokea baadaye.**”

Nilitazama mbele tena. Ardhii likuwa ya rangi ya kijivu, bila maisha , wala kitu chochote cha kijani. Kila kitu kilikuwa Kimekuwa au katika hali ya kufa. Sehemu nyingine zilikuwa baridi na nyevu nyevu, na nyingine zilikuwa moto na kavu. Na wakati wote kulikuwa na harufu nzito, mbaya, ya nyama inayochomwa na kuoza, ikichanganyikana na harufu ya mavi, na takataka zilizooza.

“**Shetani anatumia mitego mingi kuwadanganya watu wa Mungu,**” Yesu alisema.
“**Katika safari zetu za kuzimu nitakuonyesha ujanja na mbinu za ibilisi.**”

Tulikuwa tumetembea hatua chache nilipoona kitu cheusi mbele yetu. Kilionekana kushuka na kupanda, kubonyea na kuvimba. Kila kilipotembea kilitoa harufu mbaya ya kutisha, mbaya kuliko harufu nyingine mbaya za kuzimu.

Nitajaribu kueleza niliyoyaona kwa kadri ya uwezo wangu. Kitu hiki kikubwa, cheusi kilichokwuwa kinaning’inia kilipoendelea kujipanua na kujikunja na kutoa harufu mbaya sana, niliona vitu kama pembe, za rangi nyeusi, zikitoka kwenye kitu hiki na kwenda juu

duniani. Nilitambua kwamba ulikuwa ni moyo mkubwa, mweusi na kwamba ulikuwa na milango mingi. Hali ya wasiwasi ilinijia.

Yesu alitambua mawazo yangu na kusema, “***Usiogope. Huu ni moyo wa kuzimu. Baadaye tutakwenda ndani yake, lakini sasa tunakwenda sehemu ya kuzimu yenyehelo za jela.***”

Jengo la selo za jela lilikuwa katika duara katika tumbo la kuzimu. Selo zina urefu wa maili kumi na saba. Nilipoangalia juu niliona kuna mfereji mkubwa wa kijivu kati ya selo na tumbo la kuzimu, au chini. Nilihisi kwamba mfereji ulikuwa na kina cha futi sita, na nilikuwa najiuliza namna ya kuuvuka. Nikiwa katika kutafakari huku nilikuta tuko juu, kwenye ngazi ya kwanza ya selo. Ngazi hii ilizunguka selo na kwa hiyo ilikuwa mahali pazuri pa mtu kuchungulia ndani hadi katikati ya selo.

Yesu alisema, “***Mambo haya ni yamini na kweli. Mauti na kuzimu siku moja vitatupwa katika ziwa la moto. Hadi wakati huo, hapa ni mahali pa kutunzia roho zilizo kuzimu. Selo hizi zitaendelea kuwa hapa, zimejaa roho zenye dhambi, zikiteswa na kuumia.***

“Nilitoa maisha yangu ili msije mahali hapa. Nilijua kwamba mateso haya ni halisi, lakini neema ya Baba yangu ni halisi vile vile. Ukimruhusu, atakusamehe. Mwite leo katika Jina langu.”

Sura ya 8

Selo za Kuzimu

Yesu na mimi tulisimama kwenye ngazi ya kwanza ya selo. Ngazi hii ilikuwa na upana wa futi kama nne. Nilipotazama juu, kwa kadri ya upeo wa macho, niliziona ngazi zingine katika duara kubwa kuzunguka kitu kama shimo kubwa. Pembeni mwa ngazi, au njia ya kupita, kulikuwa na selo zimechimbwa ardhini. Kama selo za jela, selo hizi zilikuwa kwenye mstari, zikitenganishwa na futi mbili tu za udongo.

Yesu alisema, “*Jengo hili la selo lina urefu wa maili kumi na saba kwenda juu, kuanzia chini ya kuzimu. Katika selo hizi kuna roho nyngi ambazo zilikuwa katika uchawi na ulozi. Zingine zilikuwa na udanganyifu wa mazingaombwe, mizimu, wauzaji wa dawa za kulevyta, waabudu sanamu, au watu wabaya wenye roho za utambuzi. Hizi ni roho ambazo zilifanya machukizo makubwa kwa Mungu. Nyngi kati ya hizi zimekuwepo hapa kwa miaka mia nyngi. Hizi hazikutaka kutubu, hasa zile zilizowadanganya watu na kuwapeleka mbali na Mungu. Roho hizi zimefanya mabaya mengi dhidi ya Mungu na watu wake. Zilfurahia uovu na dhambi.*

Nilipoendelea kumfuata Yesu kwenye ile ngazi, nilitazama chini katikati ya kuzimu, ambapo palikuwa mahali penye shughuli nyngi. Mwanga hafifu ulikuwepo pale wakati wote, na niliona viumbi vingi vikiwa katika shughuli mbalimbali. Kwa kadri ya upeo wa macho mbele yangu kulikuwa na selo.

Niliwaza kimoyomoyo kwamba kwa vyovyote vile mateso ya kwenye selo yasingezidi yale ya kwenye mashimo. Kuzunguka pande zote nilisikia vilio. Nilianza kuugua. Majonzi mazito yalijaza roho yangu.

Yesu alisema, “*Sikuruhusu usikie vilio hivyo kabla mpaka sasa, mtoto. Lakini sasa nataka nikuonyeshe namna ambavyo Shetani anakuja kuiba, kuua na kuharibu. Kuzimu huku kuna mateso tofauti kwa roho tofauti. Shetani anatoa mateso haya mpaka siku ya hukumu, mpaka mauti na kifo vitakapotupwa katika ziwa la moto. Vile vile, mara nyngine ziwa la moto linakuja kuzimu.*

Tulipozidi kutembea kwenye ile ngazi, sauti zilizidi kukua. Vilio vikubwa vilitoka ndani ya selo. Nilitembea karibu na Yesu, tukafika kwenye selo ya tatu. Mwanga mkali uliimulika selo ile. Ndani yake kulikuwa na mwanamke amekaa kwenye kiti cha kubembea. Akibembea na kulia kama kwamba moyo wake ungepasuka. Sijui kwa nini, lakini nilishtuka kuona kwamba alikuwa binadamu kweli mwenye mwili.

Selo haikuwa na kitu chochote isipokuwa yule mwanamke kwenye kile kiti. Kuta za selo zilikuwa zimejengwa kwa udongo, zimesimama kwenye ardhi. Upande wake wa mbele

ulikuwa ni mlango. Ulitengenezwa kwa chuma cheusi na nondo za chuma na kutiwa kufuli. Kwa sababu nondo ziliwu zimebekwa mbalimbali mimi na Yesu tulikuwa na nafasi ya kuiona selo yote.

Ngozi ya yule mwanamke ilikuwa na rangi ya majivu na madoa meusi kiasi. Alikuwa anabembea mbele na nyuma. Huku akibembea, machozi yalichirizika kwenye shavu zake. Kutokana na mtazamo wake wa huzuni nilijua kwamba alikuwa katika mateso makubwa ya kimya kimya. Nilijiuliza kosa lake lililomfikisha hapa.

Ghafla, mbele ya macho yangu, yule mwanamke alianza kugeuka kuwa maumbo mbalimbali. Kwanza aligeuka kuwa mwanaume kikongwe, kisha kuwa msichana, halafu kuwa mwanamke wa makamu, kisha kuwa mwanamke mzee niliyemwona mwanzoni. Kwa mshangao mkumbwa nilimuona mwanamke huyu akifanya mabadiliko haya, moja baada ya jingine.

Alipomwona Yesu alilia, “Bwana, nihurumie. Nitoe mahali hapa pa mateso. Aliinama kwenye kiti chake ili amfikie Yesu, lakini hakuweza. Mabadiliko yaliendelea. Hata mavazi yake yalibadilika, alivaa kama mwanaume, halafu kama msichana, halafu kama mwanamke mzee. Mabadiliko haya yalionekana kuchukua muda mfupi tu.

Nilimuuliza Yesu, “*Kwa nini, Bwana?*”

Alipiga kelele tena, “*O Bwana nitoe kabla hawajarudi.*” Sasa alisimama mbele ya selo, akishikilia nondo za selo kwa nguvu. Alisema, “*Najua upendo wako ni kweli, najua upendo wako ni halisi. Nitoe!*” Mwanamke yule alipokuwa analia kwa uchungu, niliona kitu fulani kikianza kunyofoa nyama yake.

“**Hayuko kama anavyoonekana.**” Bwana alisema.

Mwanamke yule alikaa kwenye kiti na kuanza kubembea. Lakini sasa ni skeleton ndio ilikaa kwenye kiti cha kubembea, mifupa ikiwa na ukungu mchafu ndani yake. Mahali ambapo dakika chache zilizopita palikuwa na mwili uliovaa nguo, sasa palikuwa na mifupa mieusi iliyoungua na mashimo ya macho badala ya macho. Roho ya mwanamke yule ilugu na kumlilia Yesu katika toba. Lakini kilio hicho kilikuwa bure, alichelewa.

“**Alipokuwa duniani,**” Yesu alisema, “**mwanamke huyu alikuwa mchawi na akimwabudu Shetani. Alikuwa mchawi na aliwafundisha wengine uchawi. Tangu akiwa mtoto mdogo, familia yake ilishiriki vitendo vya kishirikina. Walipenda giza kuliko mwanga.**”

“**Mara nyingi,**” Bwana alisema, “**nilimwita atubu. Alinidharau na kuniambia, Napenda kumtukia Shetani. Nitaendelea kumtumikia.’ Alikataa kweli na alikataa kutubu uovu wake. Aliwafanya watu wengi kumwacha Bwana, baadhi yao wapo**

hapa kuzimu pamoja na huyu. Angelitubu ningemuokoa pamoja na watu wengi wa familia yake, lakini hakutaka kusikiliza.

“Shetani alimdanganya mwanamke huyu kwa kumwambia kwamba angepokea ufalme wake mwenyewe kama zawadi ya kumtumikia. Alimwambia kwamba asingekufa, lakini angeishi na Shetani milele. Alikufa akimtukuza Shetani na alikuja hapa na kudai apewe ufalme wake. Shetani, baba wa uongo, alimcheka ma kumwambia, ‘ulidhani ningekata ufalme wangu na kukugawia? Huu ni ufalme wako.’ Ndipo alipomfungia kweli selo hii na anamtesa usiku na mchana.

“Akiwa duniani mwanamke huyu aliwafundisha watu wengi uchawi, wachawi weupe na wachawi weusi. Mojawapo ya ushirikina wake ulikuwa kugeuka kutoka msichana, kuwa mwanamke wa makamo, kuwa bibi kizee, na hata kuwa mwanaume. Ilikuwa raha katika siku hizo kujibadilisha hivyo na kuwatishia wachawi wadogo. Lakini sasa anapata maumivu kuzimu, na nyama yake inanyofolewa kila badiliko linapotokea. Sasa hawezi kumudu hali hiyo, na anaendelea kugeuka kutoka umbo moja hadi lingine, lakini hali yake halisi ni ile roho ya ukungu ndani ya mifupa. Shetani anamtumia kwa makusudi yake maovu akimtania na kumdhihaki. Mara kwa mara hupelekwa mbele ya Shetani ili kuteswa na Shetani afurahi.

“Nilimwita mara nyingi, na ningemwokoa. Lakini hakunitaka. Sasa anabembeleza na kuomba msamaha, lakini amechelewa. Sasa amepotea pasipo matumaini.”

Nilimwangalia mwanamke huyu ambaye alikuwa amepotea milele katika mateso na kuugua, ingawaje alikwa mwanamke mwovu, nilimwonea huruma. “Bwana, angalia inavyosikitisha!” Nilisema kwa machozi.

Halafu, kama kwamba Yesu na mimi hatukuwa pale, pepo chafu, la kijivu lenye mabawa yaliyovunjika, lenye umbo na ukubwa wa dubu mkubwa alikuja na kufungua mlango wa selo kwa funguo. Alikuwa anapiga makelele kama kwamba kumtia hofu yule mwanamke. Mwanamke yule alipiga kelele za woga mkubwa yule pepo alipoanza kumshambulia na kumtoa kwenye selo.

Yesu alisema, “**Pepo hili huja kumtesa mara kwa mara.**” Niliona akivutwa kutoka kwenye selo na kupelekwa mahali.

“Bwana Mpandwa,” nilisema, “hatuwezi kufanya kitu chochote?” Nilimwonea huruma sana.

“**Amechelewa**” Yesu alijibu, “**Amechelewa**”

Sura ya 9

Vitisho vya Kuzimu

Nilielewa kwanini watu waliokuwa katika selo hizi ndani ya tumbo la kuzimu walikuwa tofauti na waliokuwa katika sehemu nyingine katika mateso. Kulikuwa na mambo mengi ambayo nilikuwa sielewi. Nilimsikiliza Yesu na kutunza kumbukumbu ya yote niliyoyaona na kuyasikia, kwa utukufu wa Mungu.

Kwa kuona kwangu, selo zilikuwa katika duara lisiloisha. Kulikuwa na roho moja tu katika kila selo. Kelele, vilio, na maombolezo yalitoka katika selo hizi kila tulipozipita.

Tulikuwa hatujakwenda mbali Yesu aliposimama mbele ya selo nyingine. Tulipochungulia ndani, mwanga ulikuja (Yesu alifanya nuru). Nilisimama na kuitazama roho ambayo nilijua ilikuwa katika mateso makubwa. Alikuwa mwanamke mwingine, na rangi yake ilikuwa samawia. Nyama yake ilikuwa imekufa, na sehemu za nyama ambazo zilikuwa zimeoza zilikuwa zikidondoka kutoka kwenye mifupa. Mifupa yake ilikuwa imeunguzwa na kuwa mieusi, na alikuwa na vipande vipande vya nguo. Funza walikuwa wakitambaa kwenye nyama na mifupa yake. Harufu mbaya ilijaza selo yake.

Sawa na yule mwanamke wa kwanza, huyu naye alikuwa amekaa kwenye kit cha kubembea. Alipokuwa anabembea, alilia na kukumbatia mdoli kifuani pake. Kilio cha kwikwi kilitikisa mwili wake, na kilio kilitoka kwenye selo.

Yesu aliniambia, “**Huyu naye alikuwa mtumishi wa Shetani. Alimuuzia roho yake, na ilipokuwa hai alifanya kila aina ya ubaya. Uchawi ni jambo halisi.**” Yesu alisema. “**Mwanamke huyu alitumia na kuwafundisha watu wangu uchawi na kuwageuza wengi kuelekea njia ya dhambi. Waalimu wa uchawi wanapewa upendeleo na nguvu zaidi kutoka kwa Shetani kuliko wachawi wa kawaida. Alikuwa mtabiri na alipewa pepo la utambuzi na bwana wake.**

“**Alipendwa sana na Shetani kwa maovu yote aliyoafanya. Alijua namna ya kutumia nguvu za giza kwa ajili yake na kwa ajili ya Shetani. Alikwenda kwenye ibada za wamwabuduo Shetani na kumtukuza Shetani. Alikuwa mwanamke mwenye nguvu kwa ajili ya Shetani.**”

Niliwaza kwamba sijui kazidanganya roho ngapi kwa ajili ya Shetani. Niliitazama roho hii ndani ya mifupa, ikililia mdoli-kipande kichafu cha nguo. Huzuni uliu jaza moyo wangu, na machozi macho yangu. Aliushikilia mdoli kama kwamba unaweza kumuokoa, au kwamba angeweza kuusaidia. Harufu ya mauti ilizagaa mahali pale.

Halafu nilimuona akianza kubadilika kama yule wa kwanza. Alikuwa mwanamke mzee wa miaka ya 1930 kisha kuwa msichana wa leo. Mara nyingi alifanya mabadiliko haya mbele ya macho yetu.

“Mwanamke huyu,” Yesu alisema, “*alikuwa kama mhubiri wa Shetani. Kama vile ambavyo injili ya kweli inahubiriwa kwetu na wachungaji wa kweli, Shetani naye ana wachungaji wake wa uongo. Alikuwa na nguvu za kishetani kubwa sana, ambazo ilibidi auze roho yake ili azipate. Vipawa viovu vya Shetani ni kama upande wa pili wa shilingi wa vipawa vya kiroho ambavyo Yesu anagawa kwa waumini. Hii ni nguvu ya giza.*

“Wafanyakazi hawa wa Shetani wanafanya katika ushirikina, maduka ya vitu vya kishirikina, waonaji kutumia viganja vya mikono, na njia nyingine nyingi. Msemaji wa Shetani ni mtumishi wa Shetani mwenye nguvu. Watu hawa wamedanganyika kabisa na wameuzwa moja kwa moja kwa Shetani. Wafanyakazi wengine wa giza hawawezi kusema na Shetani mpaka wasemaji waseme kwa ajili yao. Wanatoa kafara za wanadamu na wanyama kwa Shetani.

“Watu wengi wanatoa roho zao kwa Shetani. Wanachagua kumtumikia yeye kuliko Mimi. Chaguo lao ni mauti ila kama watatubu dhambi zao na kuniita, Mimi ni mwaminifu, nitawakoa na dhambi zao. Wengi wanauzwa roho zao kwa Shetani wakidhani kwamba wataishi milele, lakini watakuwa kifo kibaya.

“Shetani anadhani kwamba anaweza kumpindua Mungu na kuharibu mpango wa Mungu, lakini alishindwa msalabani. Nilichukua funguo kutoka kwa Shetani, na nina nguvu zote mbinguni na duniani.

“Baada ya mwanamke huyu kufa, alikwenda moja kwa moja kuzimu. Mapepo yalimleta mbele ya Shetani, ambapo kwa hasira aliuliza kwanini mapepo yalikuwa na uwezo juu yake, ambapo duniani alidhani ana uwezo juu yao. Duniani yalimtii. Vile vile alimwambia Shetani ampe ufalme aliokuwa amemwahidi.

“Shetani aliendelea kumdanganya hata baada ya kifo chake duniani. Alimwambia kwamba angelimfufua na kumtumia kwa makusudi yake tena. Kwa mbinu za uongo alimpatia roho nyingi, kwa hiyo uongo wake ulionekana kama kweli kwake.

“Ndipo mwishoni, Shetani alimcheka na kumdhihaki. Alimwambia, ‘Nilikudanganya na kukutumikisha miaka yote hiyo. Sitakupa kamwe ufalme wangu’”

Shetani alipunga mikono yake kwa yule mwanamke, na ilionekana kama nyama yake inanyofolewa kutoka kwenye mifupa yake. Alipiga kelele kwa uchungu huku kitabu kikubwa cheusi kikiletwa kwa Shetani. Alikifungua na kupitisha kidole chake kwenye kurasa mpaka alipoliona jina la huyu mwanamke.

"O, ndio, "Shetani alisema, "ulinitumikia vizuri duniani. Uliniletea zaidi ya roho 500." Alimdanganya na kusema, "Adhabu yako haitakuwa mbaya kama za wengine."

Kicheko cha hila kilisikika. Shetani alisimama na kumnyoshea kidole mwanamke, na upepo mkali ulivuma na kupajaza mahali pale. Sauti ya mvumo kama radi ilimtoka.

"Ha-ha," Shetani alisema, "chukua ufalme wako kama unaweza." Halafu nguvu fulani isiyonekana ilimbwaga chini.

"Hapa napo unakwenda kunitumikia." Shetani alicheka mwanamke alipojaribu kunyanyuka. Mwanamke alipiga kelele kwa uchungu nyama ilipokuwa inachanwa na mapepo kutoka kwenye mifupa yake. Aliburuzwa tena mpaka kwenye kifungo chake. Alikumbuka ahadi za Shetani. Alikuwa amemwambia kwamba angekuwa na nguvu zote. Alikuwa amemwambia kwamba asingekufa. Alimwambia kwamba alikuwa na mamlaka juu ya uzima na mauti, na alimwamini. Aliambiwa kwamba Shetani alikuwa na mamlaka ya kuzuia kitu chochote kisimuue. Shetani alimwambia uongo mwingi na kumuahidi mambo mengi.

Yesu alisema, "**Nilikuja kuwaokoa watu wengi. Nataka kwamba wote waliopotea watubu na kuliitia jina langu. Sio mapenzi yangu kwamba mtu ye yote apote, lakini kila mtu awe na uzima wa milele. Inasikitisha, wengi hawatatubu dhambi zao kabla ya kufa, na watakwenda kuzimu. Lakini njia ya kwenda mbinguni ni moja kwa watu wote. Ni lazima uzaliwe mara ya pili ili kuingia ufalme wa Mungu. Lazima uje kwa Baba kwa jina langu na kutubu dhambi zako. Lazima umpe Mungu moyo wako kwa dhati na kumtumikia.**

"**Mtoto,**" Yesu alisema, "**jambo ninalokwenda kukufunulia sasa ni baya zaidi. Najua litakusikitisha. Vile vile nataka ulimwengu usikie na kujua mambo ambayo Roho anayaambia makanisa.**

"**Katika selo hizi, kwa kadri ya upeo wa macho yako, kuna roho ziko kwenye mateso. Kila mara selo zinapojaa, kuzimu kunajipanua ili kupokea roho zaidi. Roho ikiwa kuzimu inakuwa na fahamu zake zote. Kama ulikuwa kipofu duniani, utakuwa kipofu kuzimu. Kama ulikuwa na mkono mmoja tu duniani, utakuwa na mkono mmoja tu kuzimu.**"

Lazima nikwambie tubu, kwa maana kuzimu ni mahali pabaya sana, mahali pa kutisha, mahali penye huzuni kubwa na vilio vyta vya milele vya masikitiko. Nakuomba, amini ninayosema, ni kweli tupu. Ilikuwa vigumu sana wakati wa kuandaa taarifa hii kiasi kwamba mara nyingi niliugua.

Kuzimu niliyaona mambo ambayo ni mabaya mno kuyasimulia-mabaya kuliko vilio vya mateso, harufu ya nyama inayooza, na utisho wa moto wa kuzimu ndani ya mashimo marefu. Niliona na mambo mengine ambayo Mungu hakuniruhusu kuyaandika.

Unapokufa duniani, kama umezaliwa upya na Roho wa Mungu, roho yako inakwenda mbinguni. Kama ni mwenye dhambi unapokufa, unakwenda moja kwa moja kuzimu kwenye moto. Mapepo yenye minyororo mikubwa yataiburuta roho yako kwenye malango ya kuzimu, na huko utatupwa kwenye mashimo ya kuzimu na kuteswa. Baadaye utapelekwa kwa Shetani. Ukiwa kuzimu unatumbua na kujua kila kitu kinachokutokea .

Yesu aliniambia kwamba kuna mahali kuzimu panaitwa “Kituo cha burudani.” Roho zilizofungungiwa kwenye mashimo haziwezi kwenda pale. Vile vile aliniambia kwamba ingawaje mateso ni tofouti kwa roho mbalimbali, lakini roho zote zinaunguzwa na moto.

Kituo cha burudani kina umbo la uwanja wa michezo. Watu mbalimbali ambao watakuwa waburudishaji wanaletwa katikati ya uwanja. Hawa ni watu ambao walikuwa wanamtumikia Shetani kwa kujitambua. Ni watu ambao, kwa hiari yao wenyewe waliamua kumtumikia Shetani badala ya kumtumikia Mungu. Pembeni mwa uwanja kuna roho nyingine, isipokuwa zile zilizo kwenye mashimo.

Walio katikati ya uwanja ni wale waliokuwa viranja wa uchawi duniani kabla ya kufa kwao. Walikuwa walozi, wachawi, wabashiri, na wote ambao kwa makusudi walichagua kumtumikia Shetani.

Walipokuwa duniani waliwadanganya wengi na kuwasababisha kumfuata Shetani na kutenda dhambi. Waliokuwa wamedanganywa na kusababishiwa kuanguka katika dhambi walikuja na kuwatesa wale waliowasababisha kuanguka. Mmoja baada ya mwingine waliruhusiwa kuwatesa.

Katika mojawapo ya mateso haya, mifupa ya kiroho ilisambaratishwa na kufichwa sehemu mbalimbali. Roho ilichanwa vipande vipande na vipande hivi kufichwa sehemu mbalimbali za kuzimu. Roho zilizosambatishwa hivi zilisikia maumivu makali. Watazamaji walikokuwa pembeni mwa uwanja wangeweza kuwatupia mawe wale waliokuwa katikati. Kila aina ya utesaji uliruhusiwa. Roho zilizokuwa zinateswa zililia kifo, lakini hicho kilikuwa kifo cha milele. Shetani ndiye aliyetao amri kwa mambo haya kufanyika. Hiki ni kituo chake cha burudani.

Yesu alisema, “***Nilimnyang'anya Shetani funguo za kuzimu miaka mingi iliyopita. Nilifungua selo hizi na kuwatoa watu wangu. Kwa maana wakati wa Agano la Kale kabla sijatoa maisha yangu msalabani, paradiso ilikuwa karibu na kuzimu. Selo hizi zamani zilikuwa paradiso; sasa Shetani anazitumia kwa makusudi yake mabaya na ametengeneza nyingi zaidi.***

"O msomaji, tubu kabla hujachelewa milele. Kwa maana wote watakuja kwangu kwa ajili ya hukumu. Paradiso iliondolewa mahali pake karibu na kuzimu nilipokufa na kufufuka tena kwa nguvu za Mungu, Baba yangu."

Nakwambia tena kwamba selo hizi, ambazo zina urefu wa maili kumi na saba kwenda juu, ni jela kwa wale waliokuwa watumishi wa giza wa Shetani, wote waliohusika na dhambi yoyote iliyohusu nguvu za kishetani, ushirikina na ibada ya Shetani

Yesu alisema, “**Njoo, nataka kukuonyesha kitu fulani.**”

Mara tulikuwa kama nusu maili hivi, angani, katikati ya tumbo la kuzimu. Nilikuwa kama nipo kwenye kisima ambacho mwanzo wake wala mwisho wake hauonekani kwa sababu ya giza. Rangi ya manjano ilianza kujaa mahali pale. Niliushikilia mkono wa Yesu kwa nguvu.

“*Bwana mpendwa, niliuliza, “kwanini tupo hapa?”*

Mara ile ulitokea upepo mkali na mvuno mkubwa. Mawimbi makubwa ya moto yalianza kupanda kwa kasi kwenye kuta za selo, yakiunguza kila kitu katika njia yake. Miali ya moto ilifika katika kila selo na kusababisha vilio vya uchungu na kukata tamaa. Ingawaje Yesu na mimi hatukuguswa na ule moto, hofu ilijaa ndani yangu nilipoona roho zilizopotea zikikimbilia nyuma ya selo hizo ndogo, zikijaribu kutafuta mahali pa kujificha.

Mlio wa uovu ulianza kusikika kushoto kwetu. Niliona, Shetani amesimama akitupa mgongo, na alikuwa anawaka moto. Lakini alikuwa haungui, ila, ye ye ndiye aliyesababisha moto. Sasa alikuwa amesimama amefunika na moto, akifurahia vilio vya roho hizi maskini zilizopotea. Shetani alipoinua mikono yake, mabonge makubwa ya moto yalimtoka.

Mayowe na vilio vikubwa vya maumivu vilitoka kwenye selo. Roho zilizokuwemo ndani zilikuwa zinaunguzwa zikiwa hai na moto huu wa ziwa la moto, lakini hazikuweza kufa. Mapepo nayo yaliungana na Shetani katika kicheko Shetani alipokwenda selo hadi selo, kuzitesa roho zilizopotea.

Yesu alisema, “**Shetani ananawiri kwenye uovu. Anaona sifa kwenye maumivu.**”

Nilimwangalia Shetani wakati moto wa rangi nyekundu na manjano ukiwa na ncha za kikahawia ukiongezeka kuwaka kumzunguka. Upepo ulipuliza mavazi yake ambayo hayakuungua. Harufu ya nyama inayoungua ilijaa angani, na nilitambua kwa mara ingine kwamba mateso ya kuzimu ni halisi. Shetani alitembea kwenye moto, lakini haukuweza kumuunguza. Ingawaje niliuona mgongo wake tu, nilisikia kicheko chake cha hila kila mahali.

Nilimwona Shetani akipanda ndani ya wingu la moshi, akichukua moto pamoja naye hadi juu ya tumbo la kuzimu. Nilimsikia alipogeu ka na kutangaza kwa sauti ya nguvu kwamba roho yoyote isiyomwabudu, ataipeleka kwenye kituo cha burudani.

“*Hapana Shetani, tutakuabudu.*” Walipiga kelele kwa pamoja na kuanza kumsujudia Shetani. Kwa kadri walivyomsujudia, ndivyo kadri kiu yake ya kuabudiwa ilivyoongezeka. Sauti za sifa ziliongezeka na kuongezeka mpaka paa za kuzimu zikatikisika.

Yesu alisema, “***Hawa wote walio kwenye selo hizi waliisikia injili walipokuwa hai duniani. Mara nyangi wokovu wangu ulifunguliwa kwao. Mara nyangi Roho wangu aliwavuta, lakini hawakutaka kuja kwangu kuokolewa.***”

Yesu alipokuwa anasema, Shetani alikuwa anawaambia watu wake, “*Ha-ha, huu ni ufalme wenu- ufalme pekee ambao mtakuwa nao. Ufame wangu umejaa duniani pote na ulimwengu wa chini.*” Nilimsikia akipaza sauti, “*Haya ni maisha yenu milele.*” Vilio vya majuto vilitoka kwenye selo zilizokuwa zinaungua.

Yesu alisema, “***Ukombozi wangu ni bure. Yeyote anayetaka, aje aokolewe na mahali hapa pa mateso ya milele. Sitamtupa. Kama ulikuwa mchawi au mlozi, hata kama umeandika agano na Ibilisi, nguvu yangu italivunja, na damu yangu iliyomwagika itakuokoa. Nitaondoa laana katika maisha yako na kukukomboa na kuzimu. Nipe moyo wako ili nikufungue minyororo na kukuweka huru.***”

Sura ya 10

Moyo wa Kuzimu

Usiku nilikwenda na Yesu kuzimu. Mchana kutwa kuzimu kulikuwa machoni pangu. Nilijaribu kuwaambia wengine nilichokiona, lakini hawakuamini. Nilijisikia mpweke sana, ni kwa neema ya Mungu tu niliweza kuendelea. Utukufu wote ni wa Bwana yesu Kristo.

Usiku uliofuata Yesu na mimi tulikwenda tena kuzimu. Tulitembea pembezoni mwa tumbo la kuzimu. Nilizzitambua baadhi ya sehemu kutokana na kwamba nilikuwa nimewahi kufika kule. Zile nyama za kuoza, ile harufu mbaya, ile hewa chafu, nzito ilikuwa kila mahali. Nilikuwa nimechoka tayari.

Yesu alitambua mawazo yangu na aliniambia, “**Sitakuacha kamwe au kukukana.ninajua umechoka, lakini nitakutia nguvu.**”

Yesu alinigusa na kunitia nguvu, na tukaendelea mbele. Mbele yangu niliona kitu kukibwa cheusi, kikubwa kama uwanja wa mpira na kilikuwa kama kinapumua. Nilikumbuika kwamba niliwahi kuambiwa kwamba huu ni “moyo wa kuzimu.”

Kutoka kwenye moyo huu mweusi vilijitokeza vitu kama mikono mikubwa au pembe. Vilikuwa vinatoka ndani nakwenda juu hadi nije ya kuzimu mpaka dduniani mpaka dunia yote. Nilijiuliza kama pembe hizi ni zile ambazo zinazungumzwa katika Biblia.

Sehemu zote kuzunguka moyo, udongo ulikuwa mkavu wenye rangi ya kikahawia. Kiasi cha futi thelathini ktika pande zote, udongo ulikuwa umeungua na kukauka na kuwa na rangi ya kikahawia. Moyo ulikuwa na rangi nyeusi tii, lakini rangi nyingine kama magamba ya nyoka ilichanganyikana na weusi ule. Harufu mbaya sana ilitokakwenye moyo kila ulipopumua. Ulipumua kama moyo wa kweli. Nguvu ya giza iliwazunguka.

Kwa mshangao niliutazama moyo huu mouvu na kujiliza makusudi yake. Yesu alisema, “**Matawi haya, ambayo yanakuwa kama ateri za moyo, ni mabomba ambayo yanajotokeza duniani kumwaga juu yake. Hizi ni pembe ambazo Danieli aliziona, na zinawakilisha falme mbaya duniani. Zingine zilishakwisha kuweko, zingine zitakuwako, na zingine zipo Falme mbaya zitajitokeza, na Mpanga Kristo atawatawala watu wengi, sehemu nyingi na vitu vingi. Ingewezekana hata wateiule wangedanganywa naye. Wengi wtakengeuka na kumwabudu mnyama na sanamu yake.**

“**Kutokana na haya matawi makubwa au pembe, matawi madogo yatatokea. Kutoka katika matawi madogo yatatokea mapepo, na kila aina ya nguvu za giza. Yataachiliwa juu ya dunia na kufanya mambo mengi mabaya kwa kuamriwa na Shetani. Falme hizi na nguvu za uovu zitamtii Shetani, na watu wengi watamfuata kwenye uharibifu. Ni hapa katika moyo wa kuzimu ambapo mambo haya yanaanzia.**

“**Haya ni maneno ambayo Yesu aliniambia. Aliniambia niandike na niyaweke kwenye kitabu na kuambia ulimwengu. Maneno haya ni ya kweli. Ufunuo huu nilipewa na Bwana Yesu Kristo ili watu wote wajue na waelewe kazi za Shetani ni mipango yak e mibaya kwa ajili ya siku za usoni.**

Yesu alisema, “**Nifuate.**” Tulipanda ngazi kwenda ndani ya moyo, na mlango ulifunguka mbele yetu. Ndani ya moyo kulikuwa na giza tololo. Nilisikia vilio, na kulikuwa na harufu mbaya mno nilishindwa hata kupumua. Kitu pekee ambacho nilikiona ktika gizaile ni Yesu. Nilitembea karibu naye sana.

Halafu, ghafla, Yesu alotoweka! Lisilifikirika lilitokea.nilikuwa peke yangu ndani ya moyo wa kuzimu. Utisho ulinishika. Hofu ilijaa rohoni mwangu na mauti ilinishika.

Nilimlilia Yesu, “*Uko wapi? Uko wapi? O tafadhali Bwana , njoo.*” Niliita, niliita, lakini hakuna aliyenijibu.

“*O Mungu wangu,*” nililia, “*lazima nitoke hapa.*” Nilianza kukimbia gizani. Nilipogusa kuta zilikuwa kama zinapumua, zikitekenya mikono yangu. Halau sikuwa peke yangu tena.

Nilisikia sauti ya kicheko wakati mapepo mawili, yakizungukwa na mwanga hafifu wa rangi ya chungwa, yaliposhika mikono yangu kwa nguvu. Waliweka minyororo kwenye mikono yangu haraka na kuniburuza kunipeleka chini ndani zaidi ya moyo. Nilimlilia YUesu, lakini hapakuwa na jibu. Nililia na kupigana kwa nguvu zangu zote, lakini waliniburura kama kwamba sikuwa napigana kabisa.

Tulipokuwa tunateremka ndani ya moyo, nilisikia mauvu makubwa kitu fulani kiliposuguana na mwili wangu. Ilikuwa kama nyama yangu ilikuwa inachanwa. Nilipiga mayowe kwa hofu.

Watesi wangu waliniburuza hadi kwenye selo na kunitupa ndani. Walipofunga mlango kwa kufuli nililia kwa nguvu zaidi. Walichekakwa dharau na kusema, “*Haitakusadia kulia. Muda ukifika utapelekwa mbele ya bwana wetu. Atakutesa kwa raha yake.*”

Harufu chafu ya moyo ilipenya kwenye mwili wangu. “*Kwanini nipo hapa? Kuna nini? Je nimerukwa akili? Nitoe! Nitoe!*” Nililia bilamafanikio.

Baada ya muda, nilianza kugusa kuta za selo nilimokuwemo. Ziliuwa laini na mviringo kama kitu chenye uhai. Kilikuwa kitu hai, na kilianza kutembea. “O Bwana!, nilipiga kelele. “*Kitu gani kinatokea?* Yesu, uko wapi? Lakini mwangwi tu wa sauti yangu ndio niliosikia.

Hofu, hofu kuu iliushika moyo wangu. Kwa mara ya kwanza tangu Yesu aliponiacha, nilianza kuona kwamba nilikuwa nimepotea bila tumaini lolote. Nililia na kumwita Yesu tena na tena. Halafu nilisikia sauti katika giza ikisema, “*Haitakusaidia kumwita Yesu, hayupo hapa.*”

Mwanga hafifu ulianza kujaa pale. Kwa mara ya kwanza, nilianza kupona selo nyingine kama yangu, zimejikita kwenye kuta za moyo. Utandu wa aina fulani ulikuwa mbele yetu, na ndani ya kila selo aina fulani ya kitu kama tope lenye gundi lilikuwa linatiririka kwenye selo.

Sauti ya mwanamke kutoka selo iliyokuwa karibu na mimi iliniambia, “*Umepotea katika mahali hapa pa mateso. Hakuna namna yoyote ya kutoka hapa.*”

Sikuweza kumuona vizuri kwenye ule mwanga hafifu. Alikuwa macho, kama mimi, lakini wengine kwenye selo nyingine walionekana kuwa wamelala au wako kwenye usingizi mzito. “*Hakuna tumaini*,” alilia, “*hakuna tumaini*.”

Hali ya upwke mzito na kuuta tamaa ilinijia. Maneno ya yule mwanamke hayakunisaidia. Alisema, “*Huu ni moyo wa kuzimu. Huku tunateswa lakini mateso yetu sio makubwa kama ya sehemu nyingine za kuzimu.*” Baadaye nilitambua kwamba alisma uongo aliposema kuwa mateso ya huku ni afadhali kuliko mateso ya sehemu nyingine za kuzimu.

“*Mara nyingine*,” aliendelea, “*tunapelekwa mbele ya Shetani na anatutesa kwa burudani yake. Shetani ananawiri kwenye mateso yetu na anazidi kupata nguvu kwenye vilio vyetu vya huzuni na kukata tamaa. Dhambi zetu ziko mbele yetu daima. Tunajua sio watakatifu. Vile vile tunajua kwamba tuliwahi kumfahamu Bwana Yesu lakini tulimkataa na kumpa Mungu kisogo. Tulifanya kama tulivyotaka. Kabla sijaja hapa nilikuwa kahaba. Niliwafuata wanaume na wanawake kwa kutafuta fedha zao na kuita ‘mapenzi’ mambo tuliyokuwa tunafanya. Niliharibu ndoa nyingi. Wasagaji na mashoga na wazinifu wamo kwenye selo hizi.*”

Nililia katika giza, “*Sisitahili kuwa hapa, nimeokoka. Mimi ni wa Mungu. kwanini nipo hapa?*” lakini hapakuwa na jibu lolote.

Halafu mapepo yalirudi tena na kufungua mlango wa selo yangu. Mmoja alinisukuma na mwingine alinivuta kwenye kinjia. Mguso wa mapepo ulikuwa kama moto unaounguza ngozi yangu. Walikuwa wananiumiza.

“*O Yesu uko wapi? Tafadhali nisaidie Yesu!*” Nililia

Moto mkubwa ulilipuka mbele yangu lakini ulisimama kabla haujanigusa. Sasa nyama yangu ilikuwa kama inanyofolewa kwa nguvu kutoka kwenye mwili wangu. Maumivu makali ambayo nilikuwa sijawahi kuyafikiria yalinifunika. Nilikuwa naumia kuzidi maelezo. Kitu fulani ambacho kilikuwa hakioneckani kilikuwa kkiuchana mwili wangu, na wakati huo huo mapepo machafu mfano wa popo walikuwa wananiuma mwili mzima.

“*Bwana Yesu Mpewda*,” nililia. “*Uko wapi? O, tafadhali, nitoe!*”

Nilisukumwa na kuvutwa mpaka nilipofika mahali pa wazi katika moyo wa kuzimu, ndipo nilipotupwa mbele ya madhabahu chafu. Juu ya madhabahu kulikuwa na kitabu kikubwa, kimefunguliwa. Nilisikia kicheko kiovu nandipo nilipogundua kwamba nilikuwa nimelala chini kwenye udongo mbele ya Shetani.

.Shetani alisema, “*Hatimaye nimekupata.*”

Nilijikunja kwa hofu lakini muda si muda niligundua kwamba hakuwa ananitazama mimi ila mtu mwingine mbele yangu. Shetani alisema, “*Ha ha, hatimaye ninaweza kukuangamiza*

katika dunia. Ngoja niangalie adhabu yako itakuwa nini." Alifungua kitabu na kuitisha vidole vyake kwenye kurasa. Jina la roho ile liliitwa na adhabu yake ilitolewa.

"*Bwana Mpendwa,*" Nililia, "*Je hii inaweza kuwa kweli?*"

Ilikuwa zamu yangu, na mapepo yalinisukuma mbele ni kunilazimisha kupiga magoti mbele ya Shetani. Kicheko kile kiovu kilitoka kwake. "*Nimekusubiri kwa muda mrefu, na sasa nimekupata,*" alisema kwa furaha yenyenye hila ndani yake. "*Ulijaribu kunitoroka, lakini sasa nimekupata.*"

Hofu ambayo sikuwahi kuwa nayo ilinipata. Nyama ya mwili wangu ilianza kuchanwa tena, mnyororo mkubwa ulikuwa unazungushwa kwenye mwili wangu. Nilijitazama nilipokuwa navalishwa mnyororo. Nilikuwa kama wengine. Nilikuwa skeleton nimejaa mifupa. Minyoo ilitembea ndani yangu, na moto ulianza kwenye miguu yangu na kunifunika katika moto.

Nililia tena, "*O Bwana Yesu, kitu gani kimetokea? Uko wapi, Yesu?*"

Shetani alicheka na kucheka. "*Hakuna Yesu hapa,*" alisema. "*Sasa mimi ndiye mfalme wako. Utakuwa na mimi hapa milele. Sasa wewe ni wangu.*"

Nilishikwa na hisia za kutisha. Sikuweza kuhisi uwepo wa Mungu, wala upendo, wala amani, wala faraja. Lakini nilihisi kwa hisia kali, woga, chuki, maumivu makali na huzuni kupita kiasi. Nilimwita Bwana Yesu aniokoe, lakini hapakuwa na majibu.

Shetani alisema, "*Sasa mimi ndiye bwana wako,*" na aliinua mikono yake ili kuita pepo lije pale. Mara pepo ovu, baya likuwa kwenye steji nilipokuwepo na kunishika kwa nguvu. Likuwa na mwili mkubwa, na sura kama ya popo, na makucha kama ya mwewe badala ya mkono, na harufu mbaya ilitoka kwake.

"*Nimtendee nini, Bwana Shetani?*" Pepo mbaya aliuliza, wakati pepo lingine lenye minywele mwili mzima na sura kama ya dubu aliponishika vile vile. "*Mchukue hadi sehemu ya chini kabisa ya moyo, ambapo vitisho vitakuwa mbale yake daima. Huko atajifunza kuniita Bwana*"

Niliburuzwa hadi kwenye sehemu ya giza, giza nene na kutupwa kwenye kitu baridi. O mtu anawezaje kujisikia baridi huku akiungua wakati huo huo? Sijui. Lakini moto uliunguza mwili wangu, na mafunza yalizunguka mwilini mwangu. Vilio vyta wafu villijaa hewani.

"*O Bwana Yesu,*" nililia kwa kukata tamaa, '*kwa nini nipo hapa? Mungu mpandwa, niruhusu kufa.*"

Mara nuru iliangaza mahali pale nilipokuwa nimekaa. Yesu alionekana na kunikumbatia katika mikono yake, na mara ile ile nilikuwa nyumbani kwangu.

"*Mpendwa Bwana Yesu, ulikuwa wapi?*" Nililia, machozi yakitiririka kwenye shavu zangu.

Kwa upole Yesu aliniambia na kusema, "***Mwanangu, hii ni kuzimu. Lakini usingejua kwa uhakika bila kupitia kuzimu mwenyewe. Sasa unajua ukweli na unajua maana ya kupotea kuzimu. Sasa unaweza kuwaeleza wengine habari zake. Ilinibidi nikuache upitie kuzimu ili ujue habari zake kwa uhakika.***

Nilikuwa na uchovu mwangi na huzuni nyingi. Nilijitupa kwenye mikono ya Yesu. Ingawaje alinihuisha kabisa, nilitaka kwenda mbali, mbali na Yesu, mbali na familia yangu, mbali na wote.

Katika siku zilizofuata nilikuwa mgonjwa sana. Roho yangu ilihuzunika sana, na vitisho vya kuzimu vilikuwa mbele yangu daima. Zilipita siku nyingi kabla ya kupona kabisa.

Sura ya 11

Giza la Nje

Usiku hadi usiku Yesu na mimi tulikwenda kuzimu ili niweze kuandika ukweli huu wa kutisha. Kila mara tulipopita karibu na moyo wa kuzimu, nilitembea karibu sana na Yesu. Hofu kubwa ilinishika kila nilipokumbuka yaliyonisibu kule. Nilijua ilinibidi niendelee ili kuokoa roho. Lakini ilikuwa ni kwa neema ya Mungu tu kwamba niliweza kwenda tena kuzimu.

Tulisimama kwenye kundi la mapepo waliokuwa wanaimba na kucheza wakimtukuza Shetani. Walionekana wakifurahia sana. Yesu alisema, '***Nitakuambia wanayoimba.***'

"Tutakwenda kwenda kwenye nyumba hii leo na kuwatesa wanaokaa mle. Tutapata nguvu zaidi kutoka kwa Bwana Shetani kama tutafanya hivi kwa usahihi. O ndio, tutasababisha maumivu mengi na magonjwa ya kuwasikitisha wote. Walianza kuimba na kucheza nyimbo mbaya za kumwabudu Shetani, wakiutkuza ubaya. Pepo lili sema, "***Ni lazima tuwe waangalifu sana kwa wale wanaomwamini Yesu, kwa sababu wanaweza kututoa.***"

"Ndio," mwangiye alisema, "***kwa Jina la Yesu lazima tukimbie***"

Halafu pepo lingine la mwisho lilisema, “*lakini hatuendi kwa wale wanaomjua Yesu na nguvu za jina lake.*”

“**Malaika wangu**,” Yesu alisema, “*wanawalinda watu wangu na pepo hawa wabaya, na kazi zao hazifanikiwi. Vile vile nawalinda wengi ambao hawajaokoka, hata kama hawajui kwamba nawalinda. Ninao malaika wengi waliowekwa kusimamisha mipango mibaya ya Shetani.*”

Yesu alisema, “*Kuna mapepo mengi duniani na katika anga. Nimeruhusu uyaone baadhi ya mapepo hayo, lakini mengine huwezi kuyaona. Ndio maana ukweli wa injili ni lazima uhubiriwe kwa kila mtu. Kweli itawaweka watu huru, na nitawalinda na mabaya. Katika jina langu kuna uponyaji na uhuru. Ninayo mamlaka yote mbinguni na duniani. Usimwogoge Shetani, ila mwogope Mungu.*”

Tulipokuwa tunatembea kuzimu, Yesu na mimi tulikuja kwenye mtu mmoja mkubwa sana na mweusi sana. Alikuwa amezungukwa na giza na alikuwa na umbo la malaika. Alikuwa anashika kitu fulani katika mkono wake wa kushoto. Yesu alisema, “**Sehemu hii inaitwa giza la nje**”

Nilisikia kulia na kusaga meno. Hapakuwa mahali pengine palipokuwa na hali ya kukata tamaa kama niliyoiona hapa. Malaika aliyesimama mbele yetu hakuwa na mabawa. Alikuwa na urefu wa kama futi thelathini, na alijua kwa uhakika kazi aliyokuwa anafanya. Katika mkono wake wa kushoto alikuwa na kitufe kikubwa cha mviringo na alikuwa anageuka taratibu na kitufe hiki akiwa amekiinua juu kama kwamba alikuwa anajiandaa kukitupa.

Kulikuwa na moto katikati ya kitufe, na weusi pembezoni. Malaika aliweka mkono wake chini ya kitufe na kuinama kwa nyuma ili apate nguvu zaidi.

Nilijiuliza malaika huyu mkubwa alikuwa nani na alikuwa anajiandaa kufanya nini.

Yesu aliyajua mawazo yangu na alisema tena, “**Hili ni giza la nje. Kumbuka Neno langu linasema, ‘Watoto wa ufalme watatupwa kwenye giza la nje, na huko kutakuwa na kulia na kusaga meno.’**”

“Bwana,” nilisema, “Una maana watumishi wako wako huku?”

“**Ndio**,” Yesu alijibu, “*watumishi ambao walikengeuka baada ya Mimi kuwaita. Watumishi ambao waliupenda ulimwengu kuliko Mimi na walirudi nyuma na kuogelea katika dhambi. Watumishio ambao hawakusimama katika kweli na katika utakatifu. Ni afadhali kama mtu asingeanza kabisa kuliko mtu kurudi nyuma, baada ya kuanza kunitumikia.*”

“Niamini,” Yesu alisema, “**ukitenda dhambi unaye wakili mbele za Mungu. Ukitubu dhambi zako, nitakuwa mwaminifu na kukusafisha uovu wote. Lakini kama hutubu, nitakuja kwa wakati usiotarajia, na utakatiliwa mbali pamoja na wasioamini na kutupwa katika giza la nje.”**

Nilimwangalia yule malaika mweusi alivyotupa mbali kile kitufe, mbali kwenye giza. “**maneno yangu yanamainisha yanayosema ‘watatupwa katika giza la nje.’**”

Halafu, ghafla, Yesu na mimi tulikuwa hewani, tukikifuata kile kitufe angani. Tulifika nje ya kitufe na kuchungulia ndani

Kulikuwa na moto katikati ya kitufe, na watu walikuwa wanaogelea nje na ndani, juu na chini kwenye miali ya moto. Huku hakukuwa na mapepo, ila roho zikiungua katika ziwa la moto.

Nje ya kitufe kulikuwa na weusi wa weusi. Mwanga kutoka moto wa kitufe ulimulika anga la usiku. Katika mwanga ule niliwaona watu wakijaribu kuogelea hadi pembezoni mwa kitufe. Wengine wangefika pembezoni wakati nguvu ya mvuto kutoka ndani ya kitufe ingewavutia kwenye moto. Niliangalia wakati maumbo yao yaligeuka kuwa skeletoni na roho ya ukungu wa kikahawia. Ndipo nilipojua kwamba hii ilikuwa sehemu nyingine ya kuzimu.

Halafu niliona, katika maono, malaika wakifungua mihuri. Mataifa na falme zilionekana kufungwa chini yake. Mihuri ilipofunguliwa, wanaume na wanawake, wavulana na wasichana, walitembea moja kwa moja kuingia kwenye moto.

Nilitazama kwa mshangao, nikijiuliza kama nilimjua mtumishi yeote wa Bwana aliyeanguka akitupita. Sikuweza kugeuza macho yangu nisizitazame roho hizi ambazo ziliikuwa zinatembea kuelekea kwenye moto, na hakukuwa na mtu wa kuzisimamisha. Nililia, “**Bwana, tafadhali wasimamishe kabla hawajafika kwenye moto!**”

Lakini Yesu alisema, “**Aliye na masikio na asikie. Aliye na macho na aone. Mwanangu, kemea dhambi na uovu. Waambie watumishi wangu kuwa waaminifu na kuliitia Jina la Bwana. Ninakupeleka kwenye sehemu hii ya kutisha ili uweze kuwaeleza habari za kuzimu.**”

Yesu aliendelea, “**Wengine hawatakuamini. Wengine watasema Mungu ni mwema mno hawezi kuwapeleka watu kuzimu. Lakini waambie kwamba maneno yangu ni kweli. Waambie kwamba waoga na wasioamini watakuwa na sehemu yao katika ziwa la moto.**”

Sura ya 12

Pembe

Yesu alisema, “***Leo, mwanangu, nitakuonyesha sehemu tofauti ya kuzimu. Nataka kukueleza habari za pembe na jinsi zitakavyotumika kupeleka mapepo machafu na nguvu za giza kwenye uso wa dunia.***”

Yesu alipokuwa anazungumza nilianza kuona maono ya wazi. Katika maono niliona, nyumba kuu kuu ya shamba, miti ya kikahawia iliyokufa, ikizungukwa na miti mingi iliyokufa, na majani marefu yaliyokufa. Kwenye uwanja kuzunguka nyumba vilitapaka vitu vingi vilivyokufa. Hapakuwa na uhai kule. Nyumba ilikuwa kama imetulia kwenye kona na ilikuwa inazima katikati ya uwanja. Hakukuwa na majengo mengine karibu.

Mauti ilikuwa kila mahali. Nilijua kwamba nyumba hii ya shamba ilikuwa kuzimu, ila sikuelewa nilichokuwa nakiona. Ndani, nyuma ya madirisha, vilionekana vivuli vikubwa vyenye umbo la binadamu. Kulikuwa na kitu fulani kiovu katika kuonekana kwake. Mojawapo ya viumbe hivi kilisogea kwenye mlango na kuufungua.

Nilimwona mtu mkubwa akiwa na misuli mikubwa sana akitoka kwenye nyumba hadi kwenye kibaraza. Nilimuona waziwazi. Alikuwa na urefu wa futi sita, mwenye umbo lililovimba la mnyanya vyuma. Rangi yake ilikuwa ile ile ya kikahawia sawa na ya mazingira. Alivaa kaptura. Rangi ya kaptura yake ilikuwa ya kikahawia kama ya ngozi yake sehemu ya juu. Badala ya ngozi ya nyama alikuwa na mabaka, na kichwa chake kilikuwa kikubwa sana. Yaani, kichwa chake kilikuwa kikubwa mno kiasi cha kwamba miguu yake ilipinda kutokana na kubeba mzigo huo mzito. Nyayo zake zilikuwa na kwato kama za nguruwe. Uso wake ulikuwa mkali na mwovu, na alionekana kuwa mzee sana. Macho yake yalikuwa yamekufa na uso wake ulikuwa mpana sana.

Kwenye maono niliona kiumbe huyu akiteremka kwenye kibaraza. Ardhi ilitikisika alipotembea, na pembe zilikuwa zinaota juu ya kichwa chake-pembe kubwa zilikua kuelekea juu, juu hadi zisionekane tena. Alipokuwa anatembea, niliona kuwa pembe zilikuwa zinakua, taratibu sana. Pembe nyingine zilianza kuota kwenye kichwa chake. Pembe ndogo zilichomoza kwenye pembe kubwa. Niliona kwamba kichwa chake kilikuwa kama mnyama-mnyama mwenye nguvu, mwenye uharibifu mwingi. Kila hatua aliyochukua ilitikisa ardhi.

Yesu alisema, “***Angalia.***”

Niliona zile pembe zikienda juu na kuishia kwenye nyumba za watu, kwenye makanisa, kwenye mahospitali, kwenye maofisi na kwenye majengo ya aina zote duniani pote. Pembe hizi zilifanya uharibifu mkubwa kila mahali. Nilimwona mnyama akisema na pepo wabaya wakitoka mdomoni mwake kwenda duniani. Niliwaona watu wengi wakishawishiwa na roho hizo chafu na wakinaswa na mitego ya Shetani.

Tuko vitani: wema dhidi ya ubaya, niliwaza

“Tuko vitani” nilimsikia Roho wa Bwana akisema, “**wema dhidi ya ubaya.**”

Mawingu meusi yalitoka kwenye pembe na kuficha aina nyingi za ubaya zilizokuwa zinapelekwa duniani. Machukizo yote ambayo Mungu anayachukia yalikuwa pale. Niliona falme zikiinuka katika nchi, na mamilioni ya watu walianza kuzifuata hizo roho chafu. Niliona pembe za zamani ziking’olewa na pembe mpya zikiota badala yake.

Nilimsikia Yesu akisema, “**Haya yameanza kutokea sasa! Haya mambo yapo, na yalikuwepo na yatakuwepo. Watu watajipenda wenyewe kuliko kumpenda Mungu. Uovu utakuwa mwingi sana katika siku za mwisho. Wanaume na wanawake watapenda nyumba zao, magari, viwanja na mashamba, majengo, biashara, fedha zao na dhahabu zao kuliko kunipenda Mimi.**

“Tubu”. Alisema, “**kwa maana mimi ni Mungu wenyewe vivu. Hakuna kitu chochote ambacho kinatakiwa kutangulizwa mbele mnaponiabudu Mimi – sio watoto wenu au binti zenu, sio mke wala mume. Kwa maana Mungu ni Roho, na budi kuniakumwabudu katika Roho na kweli.**”

Niliona pembe zikitembea ulimwenguni kote, zikiinuka juu katika mbingu. Falme mpya ziliinuka, na kulikuwa na vita na uharibifu kila mahali. Waliomwabudu mnyama walikuwa wengi.

Yule mnyama mwovu mwenye pembe alitembea tembea kama kwamba anawaza, na ardhi ilitikisika kwa uzito wake. Baada ya dakika kadhaa alirudi kwenye nyumba ya shamba. Mawingu meusi yaliinuka, na wengi katika nchi walikufa.

Niliiona dunia ikiwa katika dhiki kuu, na nilianza kusali kwa moyo wangu wote. “O Bwana, tusaidie,” nililia. Halafu wanyama wawili wakubwa katika hali ya roho waliinuka kutoka katika ardhi na kuanza kupigana. Nilijua walitoka kuzimu.

Umati wa watu ulisimama ukishuhudia vita kati ya maovu haya mawili. Halafu nioliona kitu kikiinuka kutoka ardhini katikati yao. Waliacha kupigana na walismama mmoja upande huu na mwingine upande ule wa meli kubwa. Wanyama wote wawili walijaribu kuiharibu meli ile, lakini hawakuweza. Waliisukumia chini ya ardhi, na kuizika katikati yao. Walisimama wakikabiliana tena, tayari kuanza vita vyao.

Nilisikia sauti ikisema, “**Tazama**.”

Nilipokuwa nikitazama, mwanga ulionekana penye ardhi ambapo meli ilikuwa imefukiwa. Meli ilionekana tena juu ya ardhi ikawa tufe kubwa. Wale wanyama walianza kuchukua maumbo mengine na wakawa wakubwa na weusi. Mlango ulifunguka pembedi mwa tufe, na mwanga mkali ulionyesha ngazi. Ngazi hii ilikuwa inakwenda chini, chini kuzimu, na nilisikia sauti ikisema, “*hadi kuzimu!*”

Kulikuwa na hali ya uwepo mkubwa wa nguvu za uovu katika anga, na nilijiona nimepotea na bila matumaini. Nguvu fulani ya kutisha ilitokea kwenye tufe nami sikuwa na mahali pa kukimbilia. Nilijiona nimenaswa, ingawaje nilikuwa katka Roho.

Mara moja, Yesu aliniinua juu na juu zaidi mpaka nikawa nayaona maono yale kwa chini. Mara zile ngazi ziligeuka na kuwa ngazi zinaoendeshwa kwa mashine, zikitembea kutoka chini kwenye moyo wa dunia. Nilipokuwa karibu na Yesu nilijiona salama na chini ya ulinzi. “*itapanda kutoka kuzimu,*” nilisikia sauti ikisema.

Yesu alisema, “**Haya yatakuwa, haya hayajatokea bado. Andika ili watu wote wajue.**”

Katika maono yangu ile ngazi iliyokuwa inatembea ilikuwa inaleta kutoka chini mapepo na nguvu za giza. Wale wanyama wawili walismama, mmoja upande huu na mwingine upande ule wa meli, na niliwaona wakianza kubadilika tena. Niilsikia muungurumo mkubwa, muungurumo wa injili ikizunguka kwa kasi kubwa. Vichwa vya wanyama vikawa vikubwa, namwanga ulianza kujaza mikono yao. Niliona wal wanyama wawili na meli hivi vitatu vikiunganishwa pamoja.

Roho nyingi, kama kwamba zinatembea katika usingizi, zikiingia kwenye mnyama mmojawapo. Nilitazama hali hii ya kushangaza kwa masaa mengi, mpaka mwishoni, mojawapo ya mnyama alijaa watu. Nilisikiliza mlilo mkubwa kama wa ndege inayotaka kupaa ikitoka kwenye mnyama wa kwanza. Mnyawa alipata nguvu zake kutoka kwenye meli. Alipoanza kuruka alikuwa tena kwenye umbo la binadamu. Alipokuwa anaruka kichwa chake kilionekana kujaa taa na nguvu nyingi zilitoka kwake.

Alipokuwa akitoweka kwenye mawingu ,kichwa chakwe kilikuwa meli tena.

Nilikuwa bado nasikia mvumo wa mnyama wa kwanza wakati nilpoona mnyama wa pili akijaa roho. Baada ya kujaa nilimwona mnyawa wa pili akipaa kama roketi. Aliungana na mnyama mwingine, na waliondoka taratibu kuingia kwenye anga la kijivu. Huyu mnyama wa pili naye alichukua umbo la mwanadamu. Nilisikia mvumo wao wa nguvu wakitoweka angani.

Nilijuliza maana ya mambo haya. Niliona meli, au tufe, ikitulia ardhini. Ardhi ilijifunga mpaka meli isionekane tena. Maono yakiwa yanafifia, niliona chumba kikubwa cha mahakama, na niliwaza juu ya kiti kikubwa cheupe cha enzi cha hukumu.

Sura ya 13

Mkono wa Kulia wa Kuzimu

Baada ya maono ya kwanza Yesu na mimi tulikwenda kwenye sehemu ya pili ya kuzimu. Yesu alisema, “**Mambo unayoyaona ni kwa ajili ya siku za mwisho.**” Maono mengine yalioneckana mbele yangu.

Yesu alisema, “**Tupo mkono wa kuume wa kuzimu.**”

Tulitembea kupanda mlima mrefu, mkavu. Tukiwa juu ya mlima tulitazama chini na kuona mto ukitembea. Hakukuwa na mashimo ya moto wala mapepo wabaya, ila mto tu ukitembea kati ya kingo ambazo zilikuwa hazionekani. Kingo za mto zilifichwa katika giza. Yesu na mimi tulitembea karibu na mto, na niliona kuwa ulijaa damu na moto.

Nilipochunguza zaidi, niliona roho nyingi, zimefungwa pamoja. Uzito wa minyororo ulizizamisha hadi chini ya ziwa la moto.

Roho za kuzimu zilikuwa katika moto wa kuzimu. Niliona pia kuwa zilikuwa skeleton zikiwa na roho ya ukungu wa kikahawia.

“*Hiki ni kitu gan?*” Nilimuliza Bwana.

“Hizi ni roho za wasioamini na wasioishi maisha ya utakatifu, hawa waliipenda miili yao wenye kule kumpenda Mungu. Walikuwa ni wanaume waliokuwa wanawapenda wanaume, na wanawake waliokuwa wanawapenda wanawake, ambao hawakutaka kutubu na kuokolewa kwenye dhambi zao. Waliyafurahia maisha yao ya dhambi nu kuudharau wokovu wangu.”

Nilisimama karibu na Yesu na kutazama kwenye moto. Moto ulianza kuunguruma kama tanuru kubwa, ukienda na kuharibu kila kitu katika njia yake. Muda si muda ulijaza karibu mkono mzima wa kuume wa kuzimu.

Moto ulisogea hadi futi moja kutoka pale tuliposimama, lakini haukutugusa. Moto ulikuwa unaunguza kila kitu katika njia yake. Niliutazama uso wa Yesu, ulikuwa na huzuni na

mwororo. Upendo na huruma kwa roho zilizopotea bado ulikuwa unasomeka kwenye sura yake. Nilianza kulia na kutamani kutoka kwenye sehemu ile ya mateso, kuendelea kukaa pale ilikuwa haivumiliki.

Nilizitazama tena roho zilizokuwa katika moto. Zilikuwa zinawaka kwa wekundu, na mifupa yao ilikuwa mieusi na imechomeka. Nilizisikia roho zao zikilia kwa uchungu na masikitiko.

Bwana alisema, “**Haya ni mateso yao. Mnyororo baada ya mnyororo, zimeunganishwa pamoja. Hawa walipenda jinsia moja, waume kwa waume, wake kwa wake, wakifanya mambo yasiyo ya kawaida. Walivuta wasichana na wavulana wengi kwenye vitendo vya dhambi. Walisema ni mapenzi, hatima yake ni dhambi na mauti.**

“**Najua kwamba wavulana wengi na wasichana wengi, wanaume na wanawake, walifanya vitendo hivi vya aibu kwa kulazimishwa bila kupenda. Najua na sitawahukumu kwa dhambi hii. Lakini kumbuka.**”

Yesu alisema, “**Nayajua mambo yote, na watu waliosababisha vijana hawa kufanya dhambi wana adhabu kubwa zaidi. Nitahukumu kwa haki. ‘kwa mwenye dhambi nasema, ‘tubu, nami nitakuwa na rehema. Niite, nami nitakusikia.’**

“**Mara nyingi nimeziita roho hizi zitubu na zije kwangu. Ningezisamehe na kuzitakasa, na katika Jina langu zingekuwa huru. Lakini hawakutaka kunisikiliza. Walipenda raha za mwili zaidi kuliko kumpenda Mungu aishiye. Kwa sababu mimi ni mtakatifu, ni lazima muwe watakatifu. ‘usiguse kitu kichafu, nami nitakupokea.’**” Alisema Bwana.

Nilijisikia vibaya nilipokuwa nazitazama roho kwenye ziwa la moto.

“**Kama tu wangenigeukia bila kucheleta,**” Yesu aliendelea, “**damu yangu ingeliwaosha ili kila mtu aje kwangu. Nilitoa maisha yangu ili hata mwenye dhambi mbaya kuliko wote apate kuishi.**”

Roho nyingi zilikwenda kwenye mto wa miali ya moto. Juu na chini ya mawimbi ya moto walikwenda, bila njia ya kutokea wakiungua na kuogelea kwenye ziwa la moto. Nilisikia vilio vya kujuta mto wa damu ulipokuwa ukipita kando yetu.

Tulitembea kwenye kijia pembeni mwa mto. Mbele yetu, akiwa amekaa kwenye kimlima, alikuwepo mwanamke mnene. Alikuwa anayumba mbele na nyuma kama mtu aliyelewa. Aliandikwa maneno haya, “*Babeli ya Siri*”

Sasa nilijua kwamba mama wa machukizo ya duniani alikuwa anatoka kuzimu. Nguvu kubwa ya uovu ilikuwa inatoka kwake. Niliona kundi kubwa la watu na ndimi chini yake.

Alikuwa na vichwa saba na pembe kumi. Ndani yake ilipatikana damu ya manabii, watakatifu na wote waliochinjwa juu ya uso wa nchi.

"**Toka ndani yake na jitenge**," Bwana alisema, "**katika wakati wake ataharibiwa.**"

Tulitembea kumpita yule mwanamke mwovu mwenye pembe juu ya kichwa chake. Giza lilianza kuingia kila mahali. Sasa Yesu alikuwa ndiye mwanga pekee. Tulitembea mpaka tulipofika kwenye kilima kingine. Kwa mbali niliona miali ya moto katika anga. Hali ya hewa ikaanza kuwa na joto la kukera.

Tuliuzunguka mlima na kuja kwenye mlango mkubwa uliotobolewa matundu. Ulikuwa umewekwe kwenye upande wa mlima. Mnyororo mkubwa ulikuwa kwenye mlango na moto mkubwa ulikuwa unawaka nyuma yake. Mlango ulikuwa umefungwa na makufuli makubwa. Nilijuiliza maana ya mambo haya.

Mara umbo jeusi la mtu, akiwa amevaa kofia ndefu nyeusi, alionekana mbele ya mlango. Alionekana mzee sana na mchovu sana. Ngozi ya uso wake ilikuwa imeshikamana na mifupa ya kichwa chake. Alionekana kama ana miaka elfu moja.

Yesu aliniambia, "**Nyuma ya mlango kuna shimo la kuzimu. Neno langu ni hakika.**"

Moto nyuma ya mlango uliongezeka mpaka mlango ulivimba kutokana na msukumo wa joto la moto.

"*Mpendwa Bwana, " nilisema, "nitafurahi Shetani atakapotupwa kwenye shimo la kuzimu na mambo yote haya maovu yakasimama kwa muda."*

Ajibu, "**Njoo, usikie mambo ambayo Roho ayaambia makanisa. Mwisho umekaaribia, na niwaita watenda dhambi kutubu na kuokoka. Tazama sasa.**"

Tulikuwa tumesimama mahali pa wazi, na nilikuwa na Bwana katika Roho. Nilitazama na kuona maono ya wazi. Katika maono niliona joka kali likianza kupiga hewa na mkia wake mkubwa. Niliangalia namna ambavyo joka hili la kiroho lilivyoenenda kwa nguvu za kutisha.

Halafu niliona likiingia kwenye mkono wa kulia wa kuzimu na kusubiri. Nilijua kwamba haliwezi kuipiga dunia mpaka neno la Mungu litimie.

Niliona moto na moshi ukipanda kutoka ardhini, na niliona ukungu wa ajabu ukionekana juu ya dunia. Niliona giza ikionekana hapa na pale. Pembe zilianza kuota kwenye kichwa

cha joka kali. Zilienea mpaka zikaijaza dunia nzima. Shetani alitoa amri kwa lile joka. Kulikuwa na mapepo na roho chafu pale. Halafu niliona lile pepo kali likitoka kwenye mkono wa kulia wa kuzimu na kuipiga dunia kwa nguvu kubwa, watu wengi wakiumizwa na kuangamizwa.

Yesu alisema, “**Haya yatatokea siku za mwisho. Twende juu zaidi.**”,

Msomaji, kama unatenda moja wapo ya dhambi ambazo nimeziandika hapa, tafadhali acha kutenda dhambi, ita Jina la Yesu atakuokoa. Huna sababu ya kwenda kuzimu.mtafute Bwana maadam yupo karibu. Atakusikia na kukuokoa. Yeyote anayeliita jina la Bwana ataokolewa.

Sura ya 14

Mkono wa Kushoto wa Kuzimu

Unabii Kutoka kwa Yesu kwa Watu Wote.

Yesu alisema, “**Mambo haya sasa yameanza kutokea duniani, bado hayajatokea, na yatakuja hivi karibuni kwa dunia nzima. Joka kali ni sehemu ya mnyama. Nabii unazokwenda kusoma ni za kweli. Mafunuo ni ya kweli. Kesha**

“**Wanaume, wapendeni wake zenu kama Kristo alivyolipenda kanisa. Waume na wake pendaneni kama nilivyowapenda. Niliagiza ndoa na kuibariki kwa Neno langu. Kitanda cha ndoa kiwe kitakatifu. Jitakaseni na uchafu wote na iweni watakatifu, kama mimi nilivyo Mtakatifu.**

“**Watakatifu wa Mungu wamedanganywa na wadanganyaji. Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Uelewa utawajieni kama mtafungua masikio yenu na kunisikiliza. Huu ni ujumbe wa Bwana kwa makanisa. Jihadharini na manabii wa uongo wanaosimama patakatifu pangu na kuwadanganya kwa maneno matamu. O dunia, watakatifu wangu wamelazwa na mafundisho potofu. Amka, Amka! Nawaambia kwamba uchafu wote ni dhambi. Jitakaseni na dhambi zote za mwili na roho.**

“**Manabii wangu watakatifu waliishi maisha ya utakatifu, lakini mmeasi dhidi yangu Mimi na utakatifu wangu. Mmeasi na kuingia kwenye utumwa wa magonjwa na kifo. Mmetenda maovu na mmaniasi. Mmeziacha amri zangu na hukumu zangu. Hamkuyasikiliza maneno ya watumishi wangu, manabii wa kiume na wa kike. Laana**

badala ya baraka zimewajieni, na bado mnakataa kunigeukia na kutubu dhambi zenu.

“Kama mtarejea na kutubu, na kama mtaniheshimu na tunda la toba, nitabariki nyumba zenu na kuheshimu vitanda vyenu vya ndoa. Kama mtajinyenyekesha na kuniita, nitawasikia na kuwabariki.

“Sikilizeni, Enyi watumishi wa Neno langu takatifu. Msiwafundishe watu wangu kumtendea Mungu wao dhambi. Kumbuka kwamba hukumu inaanza kwenye nyumba ya Mungu. Msipotubu, nitawaondoa kwa sababu ya dhambi mliyowafundisha watu wangu. Mnadhani Mimi ni kipofu siwezi kuona na kiziwi siwezi kusikia?

“Nyie amba mnapotosha ukweli na mnajaza mifuko yenu na fedha na dhahabu kwa migongo ya maskini - tubu, nasema mapema kabla hamjachelewa. Siku ya hukumu utasimama peke yako mbele yangu na kutoa hesabu ya vile ulivyofanya na Neno langu takatifu. Ukinii ta kwa toba, nitaondoa laana kutoka katika nchi zenu na kuwabariki kwa baraka nyingi. Kama mtatubu na kuona aibu kwa ajili ya dhambi zenu, nitakuwa na huruma na kuwahurumia, na sitazikumbuka dhambi zenu tena. Ombo kwamba uwe mshindi.

“Amkia uhai na uishi. Tubu kwa watu uliowapotosha na kuwafundisha yasiyo sahihi. Waambie kwamba umetenda dhambi na kwamba umewatawanya kondoo wangu. Tubu kwao.

“Angalia, naandaa jeshi takatifu. Watafanya makuu kwa ajili yangu na kuharibu mahali penu pa juu. Ni jeshi la wanaume na wanawake watakatifu, wavulana na wasichana. Wamepakwa mafuta kuhubiri injili ya kweli, kuwawekea mikono wagonjwa na kuwaita wakosaji waje kwenye toba.

“Hili ni jeshi la wanaume wafanyakazi, akina mama wa nyumbani, wanawake wasioolewa, na watoto wa shule. Ni watu wa kawaida, maana si wengi mionganii mwa waheshimiwa walioitikia mwito wangu. Nyakati zilizopita hawakueleweka na walifanyiwa jeuri na kukataliwa. Lakini nimewabariki kwa ujasiri wa utakatifu na katika roho. Wataanza kutimiza unabii wangu, na kufanya mapenzi yangu. Nitatembea ndani yao, nitazungumza ndani yao, na nitafanya ndani yao.

“Hawa ni wale walionigeukia kwa mioyo yao yote, roho, akili na nguvu. Jeshi hili litawaamsha, litawazindua wengi kuwa watakatifu na wenye mioyo safi. Hivi karibuni nitaanza kutembea kati yao, kuwachagua wale nitakaopenda wawe katika jeshi langu. Nitawatafuta katika majiji na katika miji. Wengi watawashangaa niliowachagua. Mtawaona wakianza kutembea juu ya uso wa nchi kufanya makuu kwa ajili ya jina langu. Tazama na angalia nguvu zangu zikiwa kazini.

“Nawaambia tena, msikinajisi kitanda cha ndoa. Msiunajisi mwili ambamo Roho Mtakatifu anakaa. Dhambi za mwili zinapelekea dhambi za roho. Kitanda cha ndoa kiwe kitakatifu. Nilimuumba mwanaume kwa ajili ya mwanamke na mwanamke kwa ajili ya mwanaume na kuagiza kwamba wawili hawa waunganishwe kwa ndoa takatifu. Nasema tena, zinduka.”

Niliona maono mengine mengi katika mkono wa kushoto wa kuzimu. Niliagizwa na Bwana kwamba nisiyafunue sasa. Mengi kati ya hayo yalikuwa ni maono ya dunia katika siku za mwisho, wakati watu wa Mungu wengi wataanguka na kupotea.

Katika maono, nilipewa ufunuo juu ya mwili wa Kristo, huduma ya watoto wa Mungu, watoto wa mnyama na kurudi kwa Yesu. “**Baadaye unaweza kuyafunua,**” alisema, “**sio sasa.**”

“**Jeshi hili,**” Bwana alisema, “**ambalo lilizungumzwa na nabii Yoeli, litainuka kutoka katika nchi na kufanya makuu kwa ajili ya Mungu. Mwana wa Haki atainuka na nguvu za uponyaji katika mabawa yake. Atawakanyaga waovu, na watakuwa majivu chini ya miguu yake.**

“**wataitwa jeshi la Bwana. Nitawapa vipawa, na watatenda matendo yangu makuu. Watafanya makuu kwa ajili ya Bwana wa utukufu. Nitamwaga Roho yangu juu ya viumbe vyote, na wana wenu na binti zenu watatabiri.**

“**Jeshi hili litapigana na nguvu za uovu na kuharibu kazi nyingi za Shetani. Litawaleta wengi kwa Yesu kabla siku ya mnyama mwovu haijatokea**”, Bwana alisema

Yesu alisema, “**Njoo, wakati wa kuondoka umefika.**”

Hatimaye tulikuwa tunayaacha maono na mkono wa kushoto wa kuzimu. Nilifurahi sana.

Tulipokuwa tunaagana, Yesu alisema, “**Ziambie familia zenu kwamba nazipenda na kuzirudi kwa upendo. Waambie kwamba nitawalinda na ubaya kama wataweka imani yao kwangu.**”

Sura ya 15

Siku za Yoeli

Nilisikia sauti ikitumika, “**Andika, mambo haya ni aminifu na kweli.**” Nilikuwa na Bwana tena katika roho. Alikuwa juu na ameinuliwa, sauti yake ilikuwa kama ya radi.

“Angalia, O dunia, mambo haya yapo, yalikuwepo na yatakuja. Mimi ni wa Kwanza na wa Mwisho. Nitumikieni, Muumbaji, kwa maana natoa uhai, sio mauti. Inuka kutoka katika maovu yenu na niite Mimi, na nitakuponya na kukuokoa. Mambo unayosoma katika kitabu hiki ni yakweli, na muda si mrefu yatatokea.

“Tubu, kwa maana wakati umewadia, na utukufu wa Bwana utaonekana hivi karibuni. Muwe tayari, kwa maana hamuijui siku wala saa. Itakuwa kubwa thawabu ya wanaosubiri kuja kwangu. Nitawabariki wadogo wangu, wale walioitunza imani na wamenitumikia katika kweli na haki. Kabla hawajafahamu, itawafikia. Nimeandaa baraka kwa wale ambao watakuwa waaminifu kwa wito wao na wale ambao hawakulikana Jina langu. Ninasema. ‘Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa Jina langu, watajinyenyekeza na kuomba, nitawasamehe na kuwaponya na kurejeshea walivyopoteza. Ninapenda kusikia, kuponya na kuokoa wote wanaoamini na kuliita Jina langu.

“Takasa mfungo, ita kusanyiko takatifu. Wakusanye wazee na wenyeji wote wa nchi katika nyumba yangu, na nililieni. Angalia, siku ya Bwana inakuja kama mwizi wakati wa usiku- siku imefika.

“Niamini Mimi, nami nitarejesha miaka iliyoliwa na nzige, parare na madumadu.

“Jeshi langu kubwa ambalo nimeliita halitalegea, litafanya mambo mengi ya ajabu, wala halitashindwa, kwa maana Mimi ndiye nguvu yao. Sauti zao zitakuwa kama tarumbeta, watasema kama ngurumo, na wote watasikia na kujua kwamba Mimi ni Bwana Mungu wenu.”

Mpendwa Bwana Yesu, ni maombi yangu kwamba nihesabike kufaa kuwa katika jeshi hili. Ninataka kuwa katika jeshi hili lakini najua kwamba natakiwa kuwa msafi kama Yesu alivyo msafi na mtakatifu. Kwa damu ya Yesu iliyomwagika, nitakase uchafu wote. Nisaidie niwe na moyo wenye toba, usio na chuki wala uchungu wowote.

Baba, ninajua kwamba watu wako wengi wamelala. Ninaogopa kwamba itabidi uvunje vyombo vyetu vyta udongo na kutajinyenyekeza kama unataka tuwe na matunda ya haki.

Bwana, sitaki kwenda kuzimu tena na kubaki kule. O Bwana, nisaidie kuwaonya watu. Nipe uwezo wa kufanya kuzimu kusijipanue. Nisaidie mimi na watu wako kuwa wema, wenyе moyo wa upole, wenyе kusamehe na wanaopendana. Tusaidie kusema kweli wakati wote.

Najua kwamba Yesu Kristo anakuja hivi karibuni, na zawadi zake zipo pamoja naye. Najua kwamba ujumbe wangu kwa ulimwengu ni: Tubuni, maana Siku ya Bwana i karibu. “*Baba, sitaki damu ya watu hawa kuwa mikononi mwangu.*”

Sura ya 16

Kitovu cha Kuzimu

Bwana na mimi tulienda kuzimu tena. Yesu aliniambia, “*Mwanangu, kwa kusudi hili ulizaliwa, kuandika na kueleza niliyokuambia na kukuonyesha. Kwa maana mambo haya ni amini na kweli. Nimekuita ili kuuambia ulimwengu kupitia wewe kwamba kuna kuzimu, lakini nimetengeneza njia ya kukwepa. Sitakuonyesha sehemu zote za kuzimu. Na kuna mambo ambayo yamefichika ambayo siwezi kukufunulia. Lakini nitakuomyesha mambo mengi. Sasa njoo uone nguvu za giza na mwisho wake.*

Tulikwenda tena kwenye tumbo la kuzimu na tulianza kutembea kuelekea upenyo mdogo. Niligeuka kuangalia tulikokuwa tunakwenda na nikaona tulikuwa kwenye ngazi pembeni mwa selo katikati ya kuzimu. Tulisimama kwenye selo mlimokuwa na mwanamke mrembo. Juu ya selo yaliandidkwa maneno “B.C.” (yaani Kabla ya Kristo)

Nilimsikia yule mwanamke akisema, “*Bwana, nilijua siku moja utakuja. Tafadhalii nitoe kwenye sehemu hii ya mateso.*” Alivaa nguo za zama za kale, na alikuwa mrembo sana. Nilijua kwamba alikuwapo hapa kwa karne nyingi lakini hakuweza kufa. Roho yake ilikuwa katika mateso. Alianza kuvuta nondo na kulia.

Kwa sauti ya upole Yesu alisema, “*Amani, tulia.*” Alizungumza na huzuni katika sauti yake. “*Mwanamke, unajua kwa nini upo hapa?*”

“Ndio,” alisema, “lakini naweza kubadilika. Nakumbuka, ulipowatoa wengine wote paradise. Nakumbuka maneno yako ya ukombozi. Sasa nitakuwa mtu mzuri,” alilia, “na nitakutumikia.” Alishika nondo za selo katika mikono yake midogo na alianza kupiga kelele, “Nitoe, nitoe!”

Baada ya hayo alianza kubadilika mbele ya macho yetu. Nguo zake zilianza kuungua. Nyama ilidondoka, na kilichobakia ni mifupa mieusi na mashimo ya macho yaliyoungua badala ya macho na roho ndani yake. Niliangalia kwa hofu mwanamke yule alipoanguka kwenye sakafu. Uzuri wake wote ilitoweka mara moja. Ilisumbua akili yangu kuwaza kuwa alikuwapo hapa kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Yesu alimwambia, “**Ulijua ukiwa duniani mwisho wako ungekuwaje. Musa aliwapa torati, na uliisikia. Lakini badala ya kutii sheria yangu, uliamua kuwa chombo katika mikono ya Shetani, mnajimu na mchawi. Uliweza hata kufundisha uchawi. Ulipenda giza kuliko nuru, na matendo yako yalikiwa maovu. Ungelitubu kwa moyo wako, Baba yangu angelikusamehe. Lakini sasa, umechelewa.**”

Kwa huzuni na masikitiko katika mioyo yetu, tuliondoka. Hakutakuwa na kikomo cha mateso na kuumia kwake. Mikono yake iliyokuwa mifupa mitupu ilinyooshwa kwetu tulipokuwa tunaendelea mbele.

“**Mwanangu,**” Bwana alisema, “**Shetani anatumia njia nyingi kuwaharibu wanaume na wanawake wazuri. Anafanya kazi mchana na usiku, akijaribu kutafuta watu wa kumtumikia. Ukishindwa kuchagua kumtumikia Mungu, umechagua kumtumikia Shetani. Chagua uhai, na kweli itakuweka huru.**”

Baada ya kutembea kwa muda mfupi, tulisimama mbele ya selo nyingine. Nilisikia sauti ya mwanaume ikiita, “Nani yupo hapo? Nani yupo hapo?” Nilishangaa kwanini alikuwa anaita.

Yesu alisema, “**Ni kipofu.**”

Nilisikiliza sauti na kuangalia. Mbele yetu kulikuwa na pepo kubwa ambalo mabawa yake yalionekana kama yamevunjika. Alitazama bila kutuona. Nilisogea karibu na Yesu.

Pamoja, tuligeuka na kumtazama mtu aliyezungumza. Nayeye alikuwa katika selo, alikuwa ametupa mgongo – alikuwa skeletoni amezungukwa na moto na harufu ya mauti. Alikuwa anapunga mikono katika hewa na kusema, “*Nisaidie, nisaidieni!*”

Kwa upole, Yesu alimwambia, “**Bwana, amani, tulia.**”

Mtu yule aligeuka na kusema, “*Bwana, nilijua kwamba ungekuja kwa ajili yangu. Natubu sasa. Tafadhali nitoe. Nilijua kwamba nilikuwa mtu mbaya na nilitumia ulemavu wangu kujinufaisha. Najua nilikuwa mfanya mazingaombwe na niliwapeleka wengi kwa Shetani.*

Lakini Bwana, sasa natubu. Tafadhali nitoe. Usiku na mchana nateseka katika moto huu, hakuna maji. Nina kiu sana.” Alilia. “Huwezi kunipa maji kidogo ninywe?”

Tulipotoka pale mtu yule bado alikuwa anamwita Yesu. Nilitazama chini kwa huzuni.

Yesu alisema, “**Wachawi na watenda maovu wote watakuwa na sehemu katika ziwa linalowaka moto na kiberiti, ambayo ni mauti ya pili.**”

Tulifika kwenye selo nyingine ambamo mlikuwa na mwanaume mwingine. Alisema, “Bwana, nilijua kwamba ungekuja na kunitoa. Nimetubu kwa muda mrefu.” Naye huyu alikuwa skeletoni, amejaa moto na funza.

“**O mwanadamu, bado umeja uongo na dhambi. Unajua kwamba ulikuwa mfuasi wa Shetani, mwongo uliyewadanganya wengi. Ukweli haukuwahi kuwa katika kinywa chako, na daima mauti ilikuwa ndio ujira wako. Uliyasikia maneno yangu mara kwa mara ukaufanyia mzaha wokovu wangu na Roho wangu Mtakatifu. Ulidanganya maisha yako yote na hukutaka kunisikiliza. Wewe ni wa baba yako Ibilisi. Waongo wote watakuwa na sehemu yao katika ziwa la moto. Umekufuru Roho Mtakatifu.**”

Mtu yule alianza kulaani na kusema mambo mengi mabaya juu ya Bwana. Tuliendelea. Roho hii ilipotea milele kuzimu.

Yesu alisema, “**Mtu ye yote akitaka aje kwangu, na anayepotea maisha yake kwa ajili yangu atapata maisha, naam, kwa wingi zaidi. Lakini watenda dhambi lazima watubu wangali hai duniani. Watakuwa wamechelewa wakitaka kutubu wakifika hapa. Wakosaji wengi wanataka kumtumikia Mungu na Shetani, au wanadhani kwamba wana muda usio kikomo wa kukubali neema ambayo Mungu anatoa. Wenye hekima hasa watachagua leo nani wa kumtumikia.**”

Mara tulifika kwenye selo nyingine. Kilio cha huzuni kubwa kilitoka mle ndani. Tilitazama na kuona mtu akiwa skeletoni amekaa kwenye sakafu na kujikunja. Mifupa yake ilikuwa mieusi kutokana na kuungua, na roho yake ilikuwa chafu – mvuke wa kikahawia ndani. Niligundua kwamba baadhi ya viungo vyake vilikuwa havipo. Moshi na moto vilimzunguka. Funza walikuwa wanatembea ndani yake.

Yesu alisema, “**Mtu huyu alikuwa na dhambi nyingi. Alikuwa muuaji na chuki ilikuwa ndani ya moyo wake. Hakutaka kutubu wala kuamini kwamba ningeweza kumsamehe. Laiti kama angelikuja kwangu!**”

“Una maana, Bwana,” niliuliza, “alidhani kwamba usingeweza kumsamehe dhambi ya kuua na chuki?”

“**Ndio,**” Yesu alisema. “**Angeamini tu na kuja kwangu, ningelimsamehe dhambi zake zote, kubwa na ndogo. Badala yake aliendelea kutenda dhambi na alikuwa katika**

hizo. Ndio maana yupo hapa alipo leo. Alipewa fursa nyingi kunitumikia na kuiamini injili, lakini alikataa. Sasa amechelewa.

Selo tulioyiendea ilijaa harufu mbaya ajabu. Nilisikia vilio vy a wafu na manung'uniko ya kukata tamaa kila mahali. Nilikuwa na huzuni mno kiasi cha kuugua. Niliamua kwamba nitafanya kila linalowezekana kuuambia ulimwengu kuhusu mahali hapa.

Sauti ya mwanamke ilisema, “*Nisaidie.*” Niliyaona macho ya kweli, sio mashimo meusi ya macho ambayo ni ishara ya kuungua. Nilisikitika kiasi cha kutetemeka, niliona huruma na huzuni kwa roho hii. Nilitaka sana kumvuta kwenye selo na kukimbia naye. “*Inauma kweli.*” Alisema.

“*Bwana, sasa nitafanya yaliyo sahihi. Kuna wakati nilikuja, ulikuwa Mkombozi wangu.*” Mikono yake ilishikilia nondo za selo kwa nguvu.” *Kwanini usiwe Mkombozi wangu sasa?*” Mapande ya nyama iliyoungua yalidondoka toka mwilini mwake, na mifupa tu ndio iliyoshikilia nondo za selo.

“*Hata uliniponya ugonjwa wa kansa*”, alisema, “*Uliniambia nisitende dhambi tena jambo baya zaidi lisije likanitokea. Nilijaribu, Bwana, unajua nilijaribu. Hata nilijaribu kushudia kwa ajili yako. Lakini, Bwana, mara nilijifunza kwamba wanaohubiri neno lako hawapendwi. Nilitaka watu wanipende. Taratibu nilirejea katika dunia na tamaa ya mwili ilinimaliza. Majumba ya stare na vinywaji vikali vilikuwa muhimu kwangu kuliko wewe. Nilipoteza ukaribu namarafiki zangu Wakristo na mara nikajikuta nina hali mbaya mara saba kuliko nilivyokuwa mwanzoni.*

“*Ingawaje niliwapenda wote wanaume na wanawake, sikukusudia kupotea. Sikujua kwamba nilikuwa nimemilikiwa na Shetani. Bado kwenye moyo wangu nilisikia wito wako wa kutubu na kuokoka, lakini sikuweza. Niliendelea kuwaza kwamba muda ulikuwepo bado. Kesho nitamgeukia Yesu, ananisamehe na kuniokoa. Lakini nilisubiri muda mrefu mno, na sasa nimechelewa,*” alilia.

Macho yake ya huzuni yaliwaka moto na kutoweka. Nililia na kumwangukia Yesu. O Bwana, niliwaza, ni rahisi tu kuwa huyo angekuwa mimi au mmojawapo wa wapendwa! Mkosaji, tafadhalii, amka kungali nafasi.

Tulitembea hadi kwenye selo nyingine. Ndani yake alikuwemo mtu mwingine, skeleton yenyе roho ya rangi ya kikahawia ndani yake. Kilio cha uchungu mkubwa na majuto kilitoka kwa mtu huyu na nilijua kwamba nisingesahau kamwe.

Yesu alisema, “***Mwanangu,wengine watakaosoma kitabu hiki watakilinganisha na riwaya au picha ya sinema ambayo wame wahini kuiona. Watesema kwamba hii si kweli. Lakini wewe unajua kwamba mambo haya ni kweli. Unajua kwamba kuzimu ni***

halisi, kwa maana nimekuleta huku mara nyingi kwa Roho wangu. Nimekufunulia kweli ili ukaushuhudie.”

Ewe mpotevu, kama hutatubu na kubatizwa na kuiamnini injili ya Yesu Kristo, hakika huu ndio utakuwa mwisho wako.

“Huyu mtu yupo hapa,” Bwana alisema, **“kwa sababu ya uasi. Dhambi ya uasi ni kama dhambi ya uchawi. Wale wote ambao wanalijua Neno langu na njia zangu na wamesikia injili lakini hawataki kutubu wananiasi. Wengi wako kuzimu leo kwa sababu ya dhambi hii.”**

Mtu yule alizungumza na Yesu na kumwambia, “Kuna wakati nilitaka kukufanya wewe kuwa Bwana wa maisha yangu, lakini sikutaka kutembea njia yako nyembamba na ilisiyonyooka. Nilitaka njia pana. Ilikuwa rahisi zaidi kutumikia dhambi. Sikutaka kuwa mtakatifu. Nilipenda njia yangu ya dhambi. Nilipenda kunywa vinywaji vikali na kufanya mambo ya dunia hii kuliko kufuata amri zako. Sasa najuta kwamba sikuwasikia watu uliowatuma kwangu. Badala yake nilifanya uovu na sikutaka kutubu.”

Kilio cha kwiki kubwa kiliutikisa mwili wake alipokuwa analia kwa majuto. **“Nimeteswa mahali hapa kwa miaka mingi. Najua mimi ni nani, na najua kwamba sitatoka hapa kamwe. Ninateswa usiku na mchana katika moto huu na funza hawa. Ninaita, lakini hakuna anayekuja kenisaidia. Hapa hakuna anayejali juu ya roho yangu –hakuna anayejali juu ya roho yangu.”** Alianguka kwenye sakafu kama kifurushi na aliendelea kulia.

Tulikwenda kwenye selo nyingine. Mwanamke alikuwa anatoa mafunza kwenye mifupa yake. Alianza kulia alipomwona Yesu. **“Nisaidie “Bwana,”** alisema. **“Nitakuwa mtu mzuri, tafadhali nitoe.”** Nayeye alisimama na kushikilia nondo za selo. Nilimwonea huruma sana. Kilio kilitikisa mwili wake alipokuwa analia.

Alisema, **“Bwana, nilipokuwa duniani, niliabudu miungu ya Kihindu na miungu mingi. Sikuiamini injili ambayo wamisionari walinihubiri, ingawaje niliisikia mara nyingi. Siku moja nilikufa, niliililia miungu yangu iniokoe kuzimu, lakini haikuweza. Sasa bwana, nataka kutubu.”**

“Umechelewa.” Yesu alisema.

Moto ulimfunika tulipoendelea mbele, kilio chake kinaujaza moyo wangu hata sasa. Shetani alimdanganya.

Sauti yake ikiwa na huzuni, Yesu alisema, **“Twende, tutarudi kesho. Sasa ni saa ya kuondoka.”**

Sura ya 17

Vita Katika Mbingu

Roho wa Bwana alikuwa juu yangu, na tulikwenda tena kuzimu. Yesu alisema, “**Ninakuambia kweli, roho nydingi zipo hapa kwa sababu ya uchawi, ulozi, na kuabudu miungu mingine, kutokutii, kutokuamini, ulevi na uchafu wa mwili na roho. Njoo, nitakuonyesha siri na kukuambia mambo yaliyojificha. Nitakufundisha namna ya kuomba kupinga nguvu za uovu.**”

Tulitembea hadi sehemu ya kuzimu iliyo karibu na moyo mwovu wa kuzimu. Yesu alisema, “**Hivi karibuni tutaingia kwenye taya za kuzimu, lakini nataka kumwambia kila mtu kwamba kuzimu kumejipanua.**”

Tulisimama, na alisema, “**Tazama na amini.**” Niliangalia na kuona maono ya wazi. Katika maono Yesu na mimi tulikuwa juu sana juu ya dunia tukitazama angani. Niliona duara la kiroho juu ya dunia. Duara lilikuwa halionekani kwa macho ya kawaida, ila ya kiroho, niliweza kuliona vizuri. Nilifahamu kwamba maono hayo yalihusika na vita vyetu kupambana na wafalme na wakuu wa anga.

Nilipoendelea kuangali niliona kwamba, kumbe, kulikuwa na maduara mengi. Katika duara la kwanza kulikuwa na roho nydingi chafu na ovu. Niliona roho chafu zikichukua umbo la wachawi, na zilianza kuruka angani na kufanya uharibifu mwangi wa kiroho. Nilisikia sauti ya Yesu ikisema, “**Katika Jina langu, nawapa watoto wangu mamlaka juu ya wabaya hawa. Sikiliza na jifunze jinsi ya kuomba.**”

Niliona kitu kingine kikiinuka kutoka duara lingine na kuanza kuzunguka na kutawanywa uchawi. Kisha niliona pepo limeinuka, na lilikuwa likifanya mambo maovu duniani. Pepo lilikuwa na roho ya mchawi. Aliweza kugeuka na kucheka, na kutoka katika fimbo mkononi mwake, alimwaga roho wachafu kwa watu mbalimbali. Niliona roho nydingine chafu zikiungana na yule mchawi, na Shetani alimpa nguvu zaidi.

“**Angalia, mnayofunga duniani, nitayafunga mbinguni,**” Yesu alisema. “**Shetani lazima afungwe kama maombi ya watakatifu yanataka kuwa na nguvu katika siku hizi za mwisho.**”

Kutoka duara lingine niliona mazingaombwe akiinuka, na alinza kutoa amri. Mvua na moto vilianguka kutoka mbinguni alipokuwa anazungumza. Alizungumza mambo mabaya mengi, na aliwadanganya watu wa dunia. Nilipoendelea kutazama, niliona pepo

wengine wawili wakiungana na huyo mfanya mazingaombwe juu ya anga la dunia. Hawa wote walikuwa wafalme wabaya na nguvu za anga.

Hawa waliwapa nguvu wachawi waliojikusanya pamoja mahali fulani ili kufanya uovu. Watenda kazi wa giza waliwazunguka. Mapepo yaliingia na kutoka kama yalivyopenda.

“*Angalia kwa uangalifu*, “Yesu alisema, “*maana Roho Mtakatifu anakufunulia ukweli mkubwa.*”

Katika maono niliona mambo mabaya sana yakitokea duniani. Uovu ulikuzwa na dhambi ilitapakaa. Nguvu za uovu zilisababisha watu kuiba, kusema uongo, kudanganya, kuumizana, kusema uovu na kushindwa na tamaa ya mwili. Kila aina ya uovu ulimwagwa duniani.

Nilisema, “Yesu, haya ni vigumu mno kuendelea kutazama.”

Yesu alisema, “***Mwanangu, katika Jina langu, uovu lazima ukimbie. Vaeni silaha zote za Mungu ili muweze kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama.***”

Roho chafu zilipomwaga uovu wao na matusi juu ya dunia, niliona watu wa Mungu wakianza kuomba. Waliomba kwa Jina la Yesu na kwa imani. Walipokuwa wanaomba, Neno la Mungu lilipambana na mapepo, nayo yalianza kupoteza nguvu. Watakatifu walipoomba, nguvu za uovu zilianza kushindwa. Nguvu za uovu zilivunjika. Wale waliokuwa wamedhoofishwa na nguvu za kuzimu walipata nguvu.

Waliopoomba kwa sauti moja, malaika wa mbinguni waliingia katika mapambano. Niliwaona malaika watakatifu wakipigana na wafalme waovu na nguvu za anga, na malaika wa Mungu walikuwa wakiziharibu nguvu za uovu.

Niliangalia, tazama, kulikuwa na mstari juu ya mstari wa jeshi la malaika, kila mstari ukiwa na malaika kama 600. Watu walipokuwa wanamwamini Mungu, malaika walikuwa wanasogea mbele. Mungu ndiye alitoa amri, na nguvu yake ilikuwa kubwa sana. Aliwapa nguvu nyingi watu wake na malaika kuharibu kazi za Shetani. Mungu alikuwa akipigana na ouvu katika anga. Watu walipoomba na kumwamini Mungu, nguvu za uovu zilikuwa zikiharibiwa. Lakini kulipokuwa na kutokuamini, nguvu za uovu zilianza kushinda.

“*Watu wangu ni lazima waamini, na lazima wakubaliane wao kwa wao na mimi,* Bwana alisema, **“*mambo yote lazima yawekwe chini ya miguu ya Baba*”** Mbingu na dunia ni lazima zikubaliane kama tunataka kuwaangamiza maadui wetu.

Sifa za watu wa Mungu zilipoanza kupanda kutoka duniani, nguvu za uovu zilirudi nyuma. Niliwaona watakatifu wa Mungu wakiomba kwa moyo wao wote kupinga hila za mwovo. Walipofanya hivyo, nguvu za uchawi na laana zilivunjika, na watakatifu walipata ushindi.

Ilitokea namna hii. Malaika watakatifu walipopigana na mapepo na nguvu za kuzimu, watakatifu waliokolewa kwa njia ya maombi. Watu walipookolewa, sifa nyingi zilitolewa kwa Mungu, na sifa zililetu ushindi zaidi. Ni pale tu ambapo matokea ya maombi hayakuonekana mara moja ndipo sifa zilikoma na ouvu ulianza kushinda vita.

Nilimsikia malaika akisema kwa sauti kubwa, “O Bwana, imani ya watu wako ni dhaifu. Ni lazima wawe na imani kama unataka kuwaokoa kutoka majeshi ya Shetani. Bwana, uwe na rehema kwa warithi wa wokovu.”

Sauti ya Mwenyezi ilijibu, “***Bila imani haiwezekani kumpendeza Mungu. Lakini Bwana ni mwaminifu, atawasimamisha.***”

Tena katika maono niliona Bwana akimwaga Roho wake kwa wote wenye mwili, na watu waliamini kwamba angefanya yote waliyoomba kwa sababu walikuwa watu wake na walimpenda kweli. Walikuwa na imani kwa Mungu na waliliamini Neno lake, na Mungu aliwaokoa. Na Neno la Mungu lilikua katika nchi.

Bwana alisema, “***Yote yanawezekana kwa wao wanaoamini. Naliangalia Neno langu nipate kulitimiza. Fanyeni sehemu yenu, nanyi mnajua kwamba namimi nitafanya yangu. Kama watu wangu wasimamia kweli na kupigana vita njema, mambo mazuri ya ajabu yatatokea kama Siku ya Pentekoste. Niite nami nitakuitikia. Nitakuwa Mungu wenu nanyi mtakuwa watu wangu. Nitawathibitisha katika haki, kweli na uaminifu.***

Katika maono haya, niliwaona Wakristo wakizaliwa kama watoto wachanga. Niliwaona malaika wakisimama juu yao kuwalinda wasipatwe na mabaya. Nilimwona Bwana wa mabwana akipigana vita vyao na kushinda kwa ajili yao. Niliwaona watoto hao wakikua na kuvuna mashamba ya Bwana wa Utukufu. Walikuwa wanafanya kazi ya Bwana kwa moyo wa furaha na wa kumpenda Mungu, wakimwamini Mungu na kumtumikia. Niliona malaika na Neno la Mungu wakiungana kuteketeza ubaya kutoka uso wa dunia. Niliona amani duniani wakati hatimaye kila kitu kimewekwa chini ya miguu ya Mungu.

Sura ya 18

Maono ya Wazi Kutoka Kuzimu

Bwana alisema, “**Maono haya ni kwa ajili ya siku za baadaye, na yatatimia. Lakini nitarejea kumkomboa bibi harusi wangu, kanisa langu, na halitayaona haya. Amkeni, watu wangu. Napiga baragumu kona zate za dunia, maana nitakuja kama Neno langu linavyosema.**”

Nililiona joka kali lililokuwa mkono wa kulia wa kuzimu.

Yesu aliniambia, “**Njoo, uone mambo ambayo Roho auambia ulimwengu.**”

Niliziona pembe za joka kali zilipokuwa zinaingia kwenye miili ya watu duniani. Wengi walipagawa kabisa na joka. Nilipoangalia niliona mnyama mkubwa akiinuka mahali fulani pakubwa na kugeuka kuwa mtu. Wakazi wa dunia walimkimbia, wengine walikwenda nyikani, wengine katika mapango, wengine kwenye vituo vya treni na wengine kwenye mahandaki ya kujisetiri mabomu. Walitafuta sehemu yoyote ambayo ingewasetiri na macho ya mnyama. Hakuna aliyekuwa anamsifu Mungu au kuzungumza habari za Yesu.

Sauti iliniambia, “*Watu wangu wako wapi?*”

Niliangalia kwa karibu zaidi na kuona watu wakitembea kama watu waliokufa. Kulikuwa na huzuni nzito katika anga, na hakuna mtu aliyegeuka kulia au kushoto. Niliona kwamba watu walikuwa wanaongozwa na nguvu fulani isiyooonekana. Mara kwa mara sauti ilizungumza nao hewani, na waliitii sauti hiyo. Hawakuwa wanasemezana. Vile vile niliona kwamba namba “666” imeandikwa kwenye kipaji cha uso au mkono wa kila mtu. Niliona askari waliopanda farasi wakiwachunga watu kama kwamba walikuwa ng’ombe.

Bendera ya America, ikiwa imechanika vipande vipande, ilala chini. Hakukuwa na furaha, wala kicheko. Niliona mauti na ouvu kila mahali.

Watu walitembea kwenye mstari kwenda dukani. Walitembea kwa hatua kama askari waliokata tamaa na walivaa sare aina kama ya wafungwa. Uzio ulilizunguka duka, na walinzi waliwekwa hapa na pale. Kila nilipotazama, niliwaona askari sare za vita.

Niliwaona watu hawa kama misukule wakiingizwa kwenye maduka, ambapo waliweza kununua vitu muhimu tu. Kila mtu alipomaliza manuzi yake, alipandishwa kwenye gari la kijeshi la kijani kibichi. Gari hilo, ambalo lililindwa vizuri, lilielekea sehemu nyininge.

Hapa, kwenye aina fulani ya zahanati, watu hawa walichunguzwa kama wana magonjwa ya kuambukiza au ulemavu mkubwa. Wachache wao walitengwa pemberi kuwa hawafai.

Mara, wale walioshindwa kwenye uchunguzi walipelekwa kwenye chumba cha pemberi, swichi za aina mbalimbali zilijaza ukuta mzima. Mlango ulifunguliwa, na watalaaam mbalimbali waliingia. Mmoja wao alianza kuita majina ya watu waliokuwa chumbani mle. Bila ubishi, walioitwa waliinuka na kuingia ndani ya sanduku kubwa. Walipoingia mfanyakazi mwngine alifunga mlango na kubonyeza swichi iliyokuwa ukutani.

Dakika chache baadaye alifungua mlango alichukua fagio na chombo cha kuzolea taka, na kuzoa masalia yaliyokuwa kwenye sakafu. Hakukuwa na kitu ila vumbi kidogo badala ya watu waliokuwa wamejaa chumbani!

Niliwaona watu walikuwa wamefaulu mtihani wa kupimwa afya wakipandishwa kwenye malori yale yale na kundeshwa kupelekwa kwenye treni. Hakuna aliyezungumza au kugeuka na kumtazama mwenzake. Katika jengo lingine kila mmoja alipewa kazi ya kufanya. Wote walianza kufanya kazi bila ubishi wowote. Niliangalia walivyofanya kazi walizopewa kwa bidii, halafu, mwisho wa siku, walichukuliwa kwenye maghorofa yaliyokuwa yamezungushiwa uzio mrefu. Kila mmoja alivua nguo na kwenda kitandani kulala. Kesho yake wangeamka na kufanya kazi kwa nguvu tena.

Nilisikia sauti ikienea katika anga la usiku. Nilimwona mnyama mkubwa, alikaa kwenye kitu cha enzi kikubwa sana. Watu wote walimtii mnyama. Niliona pembe za kiroho zikiota kwenye kichwa chake. Zilikwenda kila mahali katika dunia. Mnyama alijichukulia vyeo vingi vyenye madaraka, na akawa na mamlaka kubwa.

Mnyama alijipenyeza sehemu nyingi na aliwadanganya watu wengi. Matajiri na watu maarufu walidanganywa kama vile maskini walivyodanganywa. Wakubwa na wadogo walimheshimu mnyama.

Mashine kubwa ililetwa ofisini. Mnyama aliweka alama juu yake, na sauti ilitoka kwenye mashine ile. Vile vile kulikuwa na mashine ingine kubwa ambayo iliweza kuona majumbani na mahali mbalimbali pa kazi. Kulikuwa na mashine moja tu ya aina hii, na alikuwa nayo mnyama peke yake. Sehemu ya mashine ambayo ilikuwa kwenye nyumba za watu ilikuwa haionekani kwa macho ya kawaida, lakini ilikuwa ikitoa taarifa kwa mnyama kila kitu kilichofanywa na watu. Niliangalia mnyama alipozungusha kitu chake cha enzi kuelekea kwangu. Kwenye kipaji cha uso wake kulikuwa na namba 666.

Nilipoendelea kuangali nilimwona mtu mwngine ofisini akiwa amemkasirikia sana mnyama. Alidai azungumze naye. Alikuwa akipiga kelele kwa nguvu. Mnyama alitokea na alionekana mnyenyeketu aliposema, “*Njoo, nitakusaidia kutoa suluhisho la tatizo lako.*”

Mnyama alimchua yule mtu hadi kwenye chumba kikubwa na alimwambia alale kwenye meza. Chumba kile na kitanda kile kilinikumbusha juu ya chumba cha dharura hospitalini. Yule mtu alipewa dawa ya nusu kaputi na kusukumwa akiwa amelala kwenye kitanda hadi kwenye mashine kubwa. Mnyama aliunganisha waya kwenye kichwa cha yule mtu na

akawasha machine. Juu ya ile mashine yalikuwa yameandikwa maneno haya: “Mashine hii ya kufuta kumbukumbu ni mali ya mnyama, 666.

Yule mtu alipoondolewa kwenye meza, macho yake yalipoteza uhai, na mwendo wake ulinikumbusha moja wapo ya sinema za misukule. Niliona shimo kubwa katika utosi wa kichwa chake, na nilijua kwamba akili yake ilikuwa imefanyiwa upasuaji ili atawaliwe na mnyama.

Mnyama alisema, “*Sasa bwana, si unajisikia vizuri? Si nilikwambia kwamba nitakupa suluhisho la tatizo lako? Nimekupa ubongo mpya. Sasa hatakuwa na kitu cha kujali au matatizo yoyote.*”

Mtu yule hakusema neno.

“*Utatii amri zangu zote,*” alisema yule mnyama huku akichukua kitu fulani kidogo na kukibandika wenye shati la mtu yule. Alizungumza tena na yule mtu na alijibu bila kuchezesha mdomo. Alitembea kama mtu mfu. “*Utafanya kazi bila kukasirika au kukata tamaa, hutalia wala hutaona huzuni. Utanifanya kazi mpaka utakapokufa. Ninao wengi kama wewe ninao wamiliki. Wengine wanadanganya, wengine wanaua, wengine wanaiba, wengine wanapigana vita, wengine wanazaa, wengine wanaendesha mitambo, na wengine wanafanya mambo mengine. Ndio, natawala kila kitu.*” Kicheko cha kebehi kilimtoka.

Mtu yule alipewa karatasi ili aweke sahihi. Kwa raha tu alimpa mnyama mali zake zote.

Katika maono nilimuona mtu yule akitoka kwenye ofisi ya mnyama, akiingia kwenye gari lake na kwenda nyumbani. Alipomkaribia mke wake, mke wake alijaribu kumbusu, lakini hakuthubutu kujibu. Hakuwa na hisia zozote kwa mke wake wala kwa mtu yoyote. Mnyama alimfanya asiwe na hisia za aina yoyote.

Mke wake alichukia sana na akampigia kelele mume wake, bila mafanikio. Hatimaye alisema, “*Sawa, nitamwambia mnyama. Atajua la kufanya.*” Mara baada ya kupiga simu, alitoka pale nyumbani na kwenda kwenye jumba lile lile ambalo mume wake aliquwa ametoka.

Mnyama alimkaribisha na kumwambia, “*Niambie matatizo yako. Nina uhakika naweza kukusaidia.*”

Mwanaume mmoja mzuri alimchukua na kumpeleka kwenye meza ile ile ambayo mume wake alikuwa ametoka muda si mrefu. Baada ya operesheni ile ile, naye aligeuka akawa mtumwa wa mnyama asiye na utashi.

Nilisikia mnyama akimuuliza, “*Unajisikiaje?*” Hakujibu mpaka kidude fulani kiliposhikizwa kwenye blauzi yake. Ndipo alipokiri kwamba yeze mnyama ni bwana na akaanza kumwabudu.

“*Utakuwa mzaaji,*” alisema. “*Utakuwa na watoto wazuri, nao wataniabudu na kunitumikia.*”

Mwanamke alijibu kwa sauti kama ya machine, “*Ndio bwana, nitakutii.*”

Nilimwona tena yule mwanamke. Safari hii alikuwa katika jengo lingine. Kulikuwa na wanawake wengi waja wazito katika jengo lile. Wanawake hawa walilala kwenye vitanda kama kwamba hawana uhai, wakiimba nyimbo za kurudia rudia wakimsifu mnyama. Wote walikuwa na alama ya 666 katika vipaji vya nyuso zao.

Watoto wao walipozaliwa, walipelekwa kwenye nyumba nyingine ambako manesi ambao fahamu zao zilikuwa zimevurugwa walikuwa na kazi ya kuwalea. Manesi nao walikuwa na alama ya 666 katika vipaji vya nyuso zao.

Nguvu za mnyama zilizidi kuongezeka mpaka ufalme wake ulifika ulimwenguni pote. Watoto nao walikua, na kwa wakati maalum, nao waliwekwa chini ya machine ya kubadili ufahamu. Walimwabudu mnyama na sanamu yake. Lakini mashine haikuwa na nguvu juu ya watoto wa Mungu.

Niliisikia sauti ya Bwana ikisema, “*Wale wanaomwabudu mnyama na sanamu yake wataangamia. Wengi watadanganywa na watapotea, lakini nitawaokoa watoto wangu na mnyama. Mambo haya yatafanyika katika siku za mwisho. Usipigwe alama ya mnyama. Tubu sasa kabla hujachelewa.*

“*Mnyama atajifanya mtu wa amani. Na ataleta amani kwa mataifa mengi katikati ya machafuko mengi. Ataweza kuupa ulimwengu vitu vingi kwa bei rahisi, na atahakikisha kwamba mshahara wa kila mtu unatosha. Atafanya mikataba ya ushirikiano na mataifa mengi, na wakuu wengi wa dunia watamfuata kwa ajili ya amani isiyo halisi.*

“*Kabla ya nyakati hizo nitaiunua jeshi la waumini ambalo litasimamia ukweli na haki. Jeshi kuu ambalo Yoeli alilizungumzia litasikia sauti yangu kutoka macheo hadi mawio ya juu.*

“*Hata wakati wa usiku watasikia sauti yangu, na wataitika. Watanitumikia, watakwendwa kama watu hodari wa vita. Watafanya makuu kwa ajili yangu, kwa sababu nitakuwa nao.*”

Haya yote yalifunuliwa kwangu na Bwana Yesu Kristo katika maono ya wazi. Ni maneno ya kinywa chake, na yanahu siku za mwisho.

Yesu na mimi tulirudi nyumbani, na nilikuwa natafakari mambo haya yote aliyoniambia na kunionyesha. Nilala usingiza nikiomba kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu.

Sura ya 19

Mdomo wa Kuzimu

Usiku uliofuata Yesu namimi tulitembea katika mdomo wa kuzimu.

Yesu alisema, “**Karibu tutamaliza kuzimu, mwanangu. Sitakuonyesha kuzimu nzima. Lakini niliyokuonyesha nataka uuambie ulimwengu. Waaambie kuzimu ni halisi. Waambie taarifa hii ni halisi.**”

Tulipokuwa tunakwenda, tulisimama juu ya mlipa uliokabiliana na bonde dogo. Kwa kadri ya upeo wa macho yangu kulikuwa na roho za watu pembezoni mote mwa mlipa. Nilisikia vilio vyao. Kelele zilijaa mahali hapa. Yesu alisema, “**Mwanangu, huu ni mdomo wa kuzimu. Kila wakati mdomo wa kuzimu unapofunguliwa, utasikia kelele hizo.**”

Roho zilikuwa zikijaribu kutoka lakini wapi, maana zilikuwa zimekandikwa kwenye kuta za kuzimu.

Yesu alipokuwa anasema, niliona vitu vyeusi vikianguka kutupita na kudondoka kwa kishindo chini ya mlipa. Mapepo yakiwa na minyororo mikubwa yalikuwa yakiziburiza roho. Yesu alisema, “**Hizo ni roho ambazo zimekufa duniani na zinafika kuzimu. Tukio hili linaendelea usiku na mchana.**”

Ghafla, ukimya mkubwa ulijaa mahali pale. Yesu alisema, “**Nakupenda, mwanangu, na nataka uwaambie watu wa dunia habari za kuzimu.**”

Nilitazama ndani kabisa mwa mdomo wa kuzimu kuitia kwenye matundu pembedi mwa mdomo. Vilio vyaa mateso na maumivu vilitoka mle. Mambo haya yatakwisha lini? Nilijiuliza. Nitafurahi sana nisipoyaona tena.

Halafu, ghafla, nilijikuta nimepotea. Siwezi kujua namna nilivyojua, lakini nilijua kwa moyo wangu wote kwamba Yesu ametoweka. Nilisikia huzuni kubwa. Niligeuka kuangalia alipokuwa amesimama. Kweli, Yesu hakuwepo! “*O hapana!*” Nililia. “*Sio mara hii tena, Yesu, Uko wapi?*”

Unayokwenda kusoma yatakutisha! Naomba yakutishe kiasi cha kutosha ili uwe muumini. Naomba utubu dhambi zako ili usiende mahali pale pa kutisha. Naomba uniamini, maana sitaki mambo haya yatokee kwa mtu yeoyote. Ninakupenda na nadhani utaamka bila kuchelewa.

Kama wewe ni Mkristo na unasoma haya, uwe na uhakika na wokovu wako. Uwe tayari kukutana na Bwana wakati wowote, kwa maana wakati mwingine hakuna nafasi ya kutubu. Wakati wote taa yako iwe inawaka na iwe na mafuta. Kaa tayari, maana hujui wakati gani atakuja. Kama hujazaliwa upya, soma [Yohana 3:16-19](#), na mwite Bwana, atakuokoa na mahali hapa pa mateso.

Nilipokuwa namlilia Yesu , nilianza kukimbia chini ya mlima nikimtafuta. Nilisimamishwa na pepo kubwa lenye mnyoro mkononi. Lilicheka na kusema, “*Huna mahali pa kukimbilia, mwanamke. Yesu hayupo hapa kukuokoa. Umefika kuzimu milele.*

“*O hapana, nililia, “niache niende!”* Nilipigana kwa nguvu zangu zote lakini mwishoni nilifungwa na mnyororo na kutupwa chini. Nilipolala pale, kitu kama gundi au uji kilianza kuufunika mwili wangu na harufu mbaya sana kiasi cha kutaka kutapika. Sikujua kitu gani kingetokea.

Halafu niliona nyama yangu na ngozi ikianguka kutoka kwenye mifupa yangu! Nilipiga kelele na kupiga kelele kwa taharuki kubwa. “*O Yesu, uko wapi?*” *Niliita, “Uko wapi?”*

Nilijitazama na kuona kwamba mashimo yalianza kutokea kila mahali kwenye nyama iliyosalia. Nilianza kugeuka rangi kuwa wa kijivu, na nyama ya kijivu ilidondoka kutoka mwilini mwangu. Kulikuwa na matundu kwenye mbavu zangu, kwenye miguu, na kwenye mikono. Nilipaza sauti, “*O hapana. Niko kuzimu milele, hapana!*”

Nilianza kuhisi mafunza yakitembea ndani yamwil wangu, na nilipoangalia, niliona kwamba mifupa yangu ilikuwa imeja mafunza. Hata kama nilikuwa siyaoni, nilijua yapo. Nilipojaribu kuyatoa, mengine mengi zaidi yalijitokeza. Nilikuwa nausikia uozo katika mwili wangu.

Ndio, nilikuwa najua kila kitu na nilikuwa na kumbukumbu halisi ya mambo yote ya duniani. Niliweza kuhisi, kuona, kunusa na kuonja mateso ya kuzimu. Niliweza kuona ndani yangu. Nilikuwa skeleton chafu, bado niliweza kuona yote yaliyokuwa yanatokea kwangu. Niliwaona wengine kama mimi. Kulikuwa na roho kwa kadri ya upeo wa macho yangu.

Nililia tena kwa maumivu makubwa, O Yesu, tafadhali nisaidie, Yesu. Nilitamani kufa, lakini sikuweza. Nilihisi moto ukiwashwa kwenye miguu yangu. Nilipiga kelele, “*Uko wapi, Yesu?*” niligalagala kwenye sakafu na kulia kama wengine walivyokuwa wanafanya. Tulilala kwenye mdomo wa kuzimu katika malundo , kama takataka zilizotupwa. Mateso yasiyovumilika yalizibana roho zetu.

Niliendelea kupiga kelele tena na tena, “*Uko wapi Yesu? Uko wapi Yesu!*”

Niliwaza kama nilikuwa naota au la. Je nitaamka katika ndoto? Ni kweli nilikuwa kuzimu? Nilifanya dhambi gani kubwa na kupoteza wokovu wangu? Nilimkosea Roho Mtakatifu? Nilikumbuka mafundisho yote ya biblia ambayo niliwahi kufundishwa. Nilijua kwamba familia yangu ilikuwa mahali fulani juu. Kwa taharuki kubwa nilijiona niko kuzimu sawa na roho nyingine ambazo nilikuwa nimeziona na kuzungumza nazo.

Niliona ajabu kuweza kujiona ndani ya mwili. Mafunza yalianza kunitembea tena. Niliyahisi yakitembea mwilini. Nilipiga kelele kwa woga na maumivu.

Mara lile pepo liliema, “*Yesu wako amekuangusha, au sio? Sasa wewe ni mali ya Shetani?*” kicheko cha kebehi kilimtoka aliponiinua na kuniweka juu ya kitu fulani.

Mara niligundua kwamba nilikuwa juu ya mnyama-mfu fulani. Mnyama yule, kama mimi, alikuwa na rangi ya kijivu, akiwa na uchafu mwingi na uozo. Hewa mbaya sana ilijaa hewani. Mnyama yule alinichukua juu sana kwenye ngazi. Niliwaza, “*O Bwana, uko wapi?*”

Tulizipita roho nyingi zikiomba kuokolewa. Nilisikia mlio wa mdomo wa kuzimu ukifunguliwa na roho nyingi nyingine zikiangukia mle. Mikono yangu ilifungwa nyuma.

Maumivu hayakuwa yanakuja kwa utaratibu- yaliuju ghafla na kutoweka ghafla. Nilipiga kelele kila wakati mateso yalipokuja na kusubiri kwa hofu yalipotoweka.

Niliwaza, Nitatokaje humu? Huko mbele kuna nini? Huu ndio mwisho? Nimekosa nini kustahili kuzimu? “*O Bwana, uko wapi?*” Nililia kwa uchungu.

Nililia, lakini machozi hayakutoka. Kilio kikavu kiliutikisa mwili wangu. Mnyama alisimama juu ya kitu fulani. Nilitazama na kuona chumba kizuri kimeshehezwa utajiri mwingi na vidani vinavyong’ara. Katika achumba hiki alikuwepo mwanamke mrembo amevaa nguo za kimalkia. Nilishangaa katika hali yangu ya kukata tamaa kwamba hii ni nini tena.

Nilisema, “**Mwanamke, tafadhali nisaidie**” alikuja karibu na kunitemea mate kwenye ule uso niliokuwa nao. Alinilaani na kunitukana matusi mengi. “*O Bwana, nini zaidi?*” nililia. Kicheko cha kebehi kilimtoka.

Mbele ya macho yangu yule mwanamke aligeuka na kuwa mwanaume, paka, farasi, nyoka, panya, na kijana wa kiume. Alivyotaka kuwa ndivyo alivyokuwa. Alikuwa na nguvu za giza nyingi. Juu ya chumba chake paliandikwa, “*Malkia wa Shetani.*”

Yule mnyama alitembea kwa muda ambao ulionekana kuwa ni mrefu, halafu alisimama. Nilitupwa na kudondoka chini. Nilipoinua macho yangu niliona jeshi la watu wamepanda farasi wanakuja kwangu. Nilisogezwa upande kulipisha. Nalo lilikuwa watu skeleton ya rangi ya mauti, rangi ya kijivu.

Baada ya jeshi lile kupita, niliinuliwa kutoka chini na kuwewa kwenye selo. Mtu fulani alipofunga mlango, niliangalia mazingira na kulia. Niliomba, lakini bila matumaini. Nililia na kutubu dhambi zangu mara elfu. Nilifikiria mambo mengi sana ambayo ningeliyafanya ili kuwaongoza wengine kwa Kristo na kuwasaidia watu pale waliponihitaji. Nilitubu juu ya mambo ambayo nilifanya na ambayo niliacha kuyafanya.

“O *Bwana, niokoe,* “ nililia. Mara nyingi sana nilimwita Mungu anisaidie. Sikuweza kumuona wala kumhisi. Nilikuwa kuzimu sawa tu na wengine ambao nilikuwa nimewaona. Nilianguka chini na kulia. Niliona kuwa nilikuwa nimepotea milele.

Masaa yalipita, na mara kwa mara ile sauti ilirudi tena, na roho nyingine ziliangukia kuzimu. Nilizidi kuita, “*Yesu, uko wapi?*” Masaa yalizidi kwenda. Mafunza yalianza kutembea tena kwenye mwili wangu wa roho. Niliwasikia ndani ya mwili wangu.

Mauti ilikuwa kila mahali. Sikuwa na nyama, sikuwa na viungo, sikuwa na damu, sikuwa na mwili, sikuwa na matumaini. Nilizidi kuvuta mafunza kutoka kwenye mwili wangu wa mifupa mitupu. Nilikuwa na ufahamu wa kila kitu kilichokuwa kinafanyika, na nilitamani kufa likini sikuweza. Roho yangu ingeishi milele.

Nilianza kuimba juu ya maisha na nguvu ya damu ya Yesu, ambayo ina uwezo wa kuokoa katika dhambi. Nilipokuwa naimba, mapepo makubwa yenyе mikuki yalikuja yaki坑ga kelele, “*Nyamaza!*” Yalinichoma na mikuki, na nilisikia moto ukiniingia kupita ncha za mikuki. Walinichoma mikuki tena na tena.

Waliimba, “*Hapa Shetani ni mungu. Tunamchukia Yesu na yote anayosimamia.*”

Walipoona siachi kuimba walinitoa kwenye selo na kuniburuza hadi kwenye uwazi mkubwa na kuniambia, “*Kama hunyamazi mateso yako yatakuwa makubwa zaidi.*”

Nilinyamaza kuimba, na hatimaye walimirudisha kwenye selo. Nilikumbuka vifungu vya Biblia juu ya malaika walioanguka ambao wamefungwa minyororo hadi kukumu ya mwisho. Niliwaza kama hii ndio iliyokuwa hukumu yangu. “*Bwana, waokoe watu wa dunia, nililia. “waamshe kabla hawajachelewa.*” Vifungu vingi vya Biblia vilinijia lakini niliogopa kuvisema mbele ya mapepo.

Vilio na mayowe vilijaza hewa chafu. Panya alipita karibu nami. Nilimpiga teke. Nilimuwa na watoto wangu. “*O Mungu wasije huku*”, nililia, kwa maana nilijua kwa uhakika kwamba nilikuwa kuzimu.

Mungu hakuweza kunisikia. Masikio ya Mwenyezi hayasikii vilio vya kuzimu, niliwaza. Heri kama vilio hivi vingesikika.

Panya mkubwa alipanda kwenye mguu wangu na kuniuma. Nilipiga kelele na kumtoa kwa nguvu. Kulikuwa na maumivu makubwa.

Moto ulianzia mahali fulani na kuanza kuwaka kuelekea kwangu. Nukta, dakika saa zilipita. Nilikuwa mwenye dhambi, aliye kwenda kuzimu. “*O mauti, tafadhali njoo*”. Nililia. Kilio changu kilikuwa kama kimejaza mdomo wote wa kuzimu. Wengine waliungana nami katika kilio hiki, nao walikuwa wamepotea milele, hakuna pa kutokea. Nilitaka kufa, lakini sikuweza.

Nilidondoka kwenye sakafu, nikiyasikia mateso yote. Niliona mdomo wa kuzimu ukifunguka tena, na roho nyingine ziliingia. Sasa moto ulianza kuniunguza, na maumivu mapya yalikuja. Nilikuwa na uelewa wa kila kitu. Nilikuwa na akili timamu. Mambo haya yote niliyajua, na nilijua kwamba watu wakifa duniani na hawajaokolewa kwenye dhambi zao, wanakuja huku.

“*O Mungu wangu*,” nililia. “*Tafadhali tuokoe sisi wote*.”

Niliyakumbuka maisha yangu yote na wale walionishuhudia habari za Yesu. Nilikumbuka namna ambavyo nilikuwa nawaombea wagonjwa na jinsi Yesu alivyokuwa anawaponya. Nilikumbuka maneno yake ya upendo na uaminifu wake.

Ningelikuwa kama Yesu nisingekuwa hapa, niliwaza. Niliwaza juu ya vitu vyote vizuri ambavyo Mungu alikuwa amenipa – jinsi alivyokuwa amenipa hewa niliyokuwa navuta, chakula, watoto, nyumba, na vitu vingi vizuri vya kuvifurahia. Lakini, kama Mungu ni mwema, kwanini nipo hapa? Sikuwa na nguvu ya kuinuka, lakini roho yangu ilikuwa inapiga kelele, “*Nitoe humu!*”

Nilijua kwamba huko juu kulikuwa na maisha na kwamba mahali fulani marafiki zangu na familia yangu ilikuwa inaendelea na maisha yao ya kawaida. Nilijua kwamba mahali fulani huko juu kulikuwa na vicheko, upendo, na upole. Lakini hata mawazo haya yalianza kufifia shauri ya mateso makubwa. Giza giza na ukungu mchafu ulijaza sehemu hii ya kuzimu. Mwanga dhaifu wa manjano ulikuwa kila mahali, na harufu ya nyama inayooza na uozo ulikuwa mwingi kiasi cha kushindwa kuvumilia. Dakika zilikuwa kama masaa, na masaa yalifika mpaka umilele. O mambo haya yatakwisha lini?

Sikuweza kulala, wala kupumzika, hakukuwa na maji, hakukuwa na chakula. Nilikuwa na njaa kubwa na aina ya kiu ambayo sijawahi kuifikiria katika maisha yangu. Nilichoka kweli na usingizi ulikuwa mwingi, lakini mateso yaliendelea tu. Kila mdomo wakati ulipofunguka mzigo mwingine wa roho zilizopotea ulimwagwa kuzimu. Nilijiuliwa kama baadhi ya watu niliokuwa nawafahamu walikuwemo mle. Je mume wangu watamleta huku?

Masaa yalikuwa yamepita tangu nilipokuwa nimeletwa kwenye mdomo wa kuzimu. Sasa niliona kwamba mwanga ulianza kujaa kwenye chumba. Mara moto uliacha kuwaka, panya alikimbia, na maumivu kwenye mwili wangu yalikoma. Niliangalia mpenyo wa kutokea, sikuona.

Nilishangaa. Niliangalia kwenye vlipenyo vya kuzimu, nikitazamia jambo baya kutokea. Halafu kuzimu kulianza kutetemeka, na moto ulitokea tena. Kwa mara nyingine, majoka, na mafunza na panya walitokea tena. Mateso yasiyovumilika yalijaza roho yangu tena.

“*O Mungu acha nife*,” nililia huku nikigonga sakafu ya selo yangu na mikono yangu ya mifupa mitupu. Nilipiga kelele na kulia, lakini hakuna mtu aliyejewa ananijali.

Mara niliinuliwa kutoka kwenye selo na nguvu isiyonekana. Nilipopata ufahamu, Bwana na mimi tulikuwa tumesimama pembeni mwa nyumba yangu. Nililia, “*Kwanini, Bwana, kwanini?*” na nilijiangusha kwenye miguu yake kwa kukuta tamaa.

Yesu alisema, “**Amani, tulia**.” Mara nilipata amani. Aliniinua kwa upole, na nililala usingizi nikiwa kwenye mikono yake.

Nilipoamka kesho yake, nilikuwa mgonjwa sana. Kwa siku kadhaa kumbukumbiu ya mateso ya kuzimu ilinitesa. Usiku ningeweza kuamka na kupiga kelele na kusema mafunza yanatembea kwenye mwili wangu. Nilikuwa na woga sana wa kuzimu

Sura ya 20

Mbinguni

Nilikuwa mgonjwa kwa siku nyingi baada ya kutoka mdomo wa kuzimu. Ilibidi nisizime taa usiku wakati wa kulala. Nilihitaji kuwa na Biblia karibu nami wakati wote, na niliisoma kila wakati. Roho yangu ilikuwa katika hali ya mshituko mkubwa. Sasa nilikuwa najua mambo yanayozipata roho zilizopotea zinapokwenda kuishi kuzimu.

Yesu alikuwa ananiambia, “**Amani, tulia.**” Na amani ingelikuja na kuujaza moyo wangu. Lakini dakika chache baadaye ningeliama na kupiga kelele kwa woga.

Katika nyakati hizo nilijua kwamba sikuwa peke yangu – wakati wote Yesu alikuwa pamoja nami. Pamoja na ufahamu huo, wakati mwingine nilikuwa sioni uwepo wake. Nilikuwa naogopa mno kwenda kuzimu tena kiasi kwamba mara nyingine nilikuwa naogopa hata kuwa karibu na Yesu.

Nilijaribu kuwaeleza wengine juu ya kwenda kwangu kuzimu. Hawakutaka kunisikiliza. Niliwasihi, “*Tafadhali tubu dhambi zenu muda ungalipo.*” Ilikuwa vigumu kwa mtu yeoyote kuamini mateso niliyokuwa nimeyapitia na jinsi Yesu alivyoniagiza kuandika juu ya kuzimu.

Bwana alinihakikishia kwamba alikuwa ni Bwana aliyeniponya. Ingawaje niliamini kwamba nisingepona kabisa, uponyaji ulikuja.

Halafu ilitokea tena. Kwa mara nyingine nilikuwa katika roho nikiwa na Bwana Yesu, na tulikuwa tunapaa juu kwenye mawingu.

Yesu alisema, “**Nataka kukuonyesha upendo na uzuri wa Mungu na sehemu za mbinguni. Nataka nikuonyeshe kazi nzuri za ajabu za Bwana, ambazo ni nzuri mno kuzitazama.**”

Mbele yetu niliona sayari mbili kubwa, nzuri za kupendeza katika utukufu wake. Mungu mwenyewe alikuwa ni nuru yake.

Malaika alitulaki na aliniambia, “*Angalia upendo na ukarimu wa Bwana Mungu wenu. Huruma zake zinadumu milele.*” Kulikuwa na hali ya juu ya upendo na upole kwa yule malaika kiasi cha kwamba nilitaka kulia aliposema tena, “*Angalia nguvu na uwezo na utukufu wa Mungu. Ebu nikuonyeshe mahali ambapo amepatengeneza kwa ajili ya wanawe.*”

Mara kulikuwa na sayari kubwa mbele yetu, kubwa kama dunia. Halafu nilisikia sauti ya Baba akisema, “**Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu ni wamoja. Baba na Mwana ni wamoja, na Baba n a Roho Mtakatifu ni wamoja. Nilimtuma Mwanangu kufa msalabani ili asiwepo mtu wa kupotea.**

“**Lakini**”, alisema kwa tabasamu, “**nilitaka kukuonyesha mahali ambapo nimeandaa kwa ajili ya watoto wangu. Nawajali sana watoto wote. Najali mama anapompoteza mtoto wake, angali mbegu, mtoto anayeuawa kabla ya wakati wake. Unaona, nayajua mambo yote, na najali.**

“**Tangu kunapokuwa na maisha katika tumbo, najua. Najua juu ya watoto wanaouawa wangali kwenye matumbo ya mama zao-mimba zinazotolewa kwa sababu hazitakiwi. Nawajua watoto wanaozaliwa wakiwa wamekufa na wale wanaozaliwa na ulemavu. Kutoka siku mimba inapotungwa, hiyo ni roho hai.**

“**Malaika zangu wanakwenda chini na kuniletea watoto wanapokufa. Ninapo mahali ambapo wanakaa na kukua, wanajifunza na wanapendwa. Nawapa miili mizima na kuwarejeshea viungo vilivyopungua. Nawapa miili ya utukufu.**”

Katika sayari yote kulikuwa na hali ya kupendwa, hali ya ukamilifu. Kila kitu kilikuwa kikamilifu. Hapa na pale katika majani mabichi na mabwawa ya maji maangavu kulikuwa na viwanja vya burudani na viti vya marumaru na viti vya kukalia vya mbaa vilivyong’arishwa vizuri.

Na kulikuwa na watoto. Kila nilikotazama kulikuwa na watoto wakiendelea kufanya shughuli mbalimbali. Kila mtoto alivaa kanzu nyeupe isiyo na madoa na kanda mbili. Kanzu nyeupe zilikuwa angavu kiasi cha kumeremeta kwenye mwanga wa sayari. Rangi mbalimbali zilijitokeza kila mahali na kuzidisha wangavu wa kanzu za watoto. Malaika walikuwa walini wa malango, na majina ya watoto wote yalikuwa yameandikwa katika kitabu.

Niliwaona watoto wakijifunza neno la Mungu na wakifundishwa muziki kutoka kitabu cha dhahabu. Nilishangaa kuona wanyama wa kila aina wakija kwa watoto au wakikaa pemberi mwa watoto wakiwa katika shule hii ya malaika

Hakukuwa na machozi wala huzuni. Kila kitu kilikuwa kizuri mno, furaha ilienea kila mahali.

Kisha malaika alinionyesha sayari nyingine ambayo iliwaka kama mwanga mkubwa mbele yangu. Mwanga wake ulikuwa kama mwanga wa nyota milioni moja, na kila kitu kwenye sayari kilikuwa kizuri na chakupendeza.

Kwa mbali niliona milima miwili imetengenezwa kwa dhahabu safi, na karibu nami kulikuwa na malango mawili yamepambwa kwa almasi na vito vingine vyatmanu. Nilijua kwamba hii ilikuwa ni nchi mpya na mji uliokuwa mbele yangu ambao ulikuwa umejaa uzuri wa ajabu ulikuwa Yerusalemu Mpya-mji wa Mungu ulioshuka duniani.

Halafu tena nilirejea kwenye dunia ya zamani-dunia kabla ya moto wa mwisho utakaoisafisha kwa ajili ya kusudi la Mungu. Hapa napo palikuwa na Yerusalem mpya, mji mkuu wa kipindi cha miaka 1000. Niliwaona watu wakitoka kwenye mapango na kutoka kenyé milima wakielekea kwenye mji huu.

Hapa Yesu alikuwa Mfalme, na mataifa yote ya dunia yalimletea zawadi na kumpa heshima.

Yesu alinipa tafsiri ya maono yangu. Alisema, “***Hivi karibuni nitarudi na kuwachukua mbinguni, kwanza wafu watakatifu, na baada ya hayo walio hai watanyakuliwa na kuungana nami angani. Baada ya hayo Mpinga Kristo atatawala duniani kwa muda uliowekwa, na kutakuwa na dhiki ambayo haijawahi kutokea, wala haitatokea tena.***

“Ndipo nitakapokuja na watakatifu wangu, na Shetani atatupwa kenyé shimo la kuzimu, ambako atabaki kwa miaka elfu moja. Katika miaka hiyo elfu moja nitatawala duniani kutoka Yerusalemu. Miaka elfu moja ikipita Shetani ataachiliwa kwa muda, na nitamshinda kwa mng’ao wa ujio wangu. Dunia ya zamani itapita.

“Angalia, kutakuwa na dunia mpya na Yerusalemu mpya itashuka kutoka juu_nitatawala milele na milele.”

Sura ya 21

Dini ya Uongo

Bwana alisema, “**Kama watu wa dunia watanisikiliza na kutubu dhambi zao, nitazuia kazi za Mpinga Kristo na za mnyama mpaka zitokee nyakati za kuburudisha. Je watu wa Ninawi hawakutubu kutokana na mahubiri ya Yona? Mimi ni yule yule jana, leo na milele. Tubu, nami nitatuma nyakati za baraka.**”

Tena nilimsikia Yesu akisema, “**Watu wangu wapendane na kusaidiana. Lazima wachukie dhambi na kumpenda mwenye dhambi. Kwa upendo wa namna hii watu wote watajua kwamba ninyi ni wanafunzi wangu.**”

Yesu alipokuwa anasema dunia ilifunguka na tulikwenda tena kuzimu. Niliona upande wa mlima umejaa miti iliyokufa, na kuzunguka kulikuwa na uchafu wa kijivu. Vile vile niliona mashimo madogo kwenye kuta za mlima, na taswira za kimajivu za watu wakitembea na kuzungumza.

Nilimfuata Yesu kwenye kinjia kichafu na kilichopinda pinda kilichoelekea kwenye kilima cha kijivu. Tulipokaribia, niliona kwamba watu walikuwapo, lakini walikuwa wafu. Walikuwa na miili ya kijivu iliyokufa, na walikuwa wamefungwa pamoja kwa kamba, kamba ya kijivu iliyowafunganisha pamoja watu wote kwenye kilima kile. Ingawaje sikuona moto, nilijua kwamba hapa palikuwa sehemu ya kuzimu, kwa sababu nyama zilidondoka kutoka kwenye miili ya watu hawa na kukua tena kwa haraka. Mauti ilikuwa kila mahali, lakini watu walikuwa hawaoni-walikuwa wamezama kwenye mazungumzo.

Yesu alisema, “**Ebu tusikilize wanayosema.**”

Mmoja alimwabia mwenzake, “*Ulisikia habari za mtu huyu Yesu ambaye alikuja kuchukua dhambi za dunia?*”

Mwingine alijibu, “*Nilimjua Yesu, alisafisha dhambi zangu. Kwa kweli, sijui kwanini nipo hapa.*”

“*Hata mimi sijui.*” Mtu wa kwanza alijibu.

Mwingine alisema, “*Nilijaribu kumshuhudia jirani yangu habari za Yesu, lakini hakutaka hata kusikia. Mke wake alipokufa, alikuja kwangu kukopa fedha kwa ajili ya mazishi, lakini nakumbuka kwamba Yesu alisema kwamba tuwe werevu kama nyoka na wapole kama*

hua. Kwa hiyo nilimkatalia. Nilijua kwamba angetumia fedha hizo kwa mambo mengine. Unajua, inabidi tuwe mawakili wazuri wa mali zetu.

Yule aliyesema kwanza alisema tena, “Ndio ndugu,” alisema, “Mtu mmoja kanisani kwetu alisema kwamba anahitaji nguo na viatu, lakini baba yake ni mlevi, kwa hiyo nilikataa kununua chochote kwa ajili ya mtoto wake-tulimfunza kitu yule bwana.”

“Sawa sawa,” Alijibu, huku akishika ile kamba iliyomshika mikononi mwake na kuichezea kwa kuviriringisha viringisha. “lazima niwafundishe watu kuishi kama Yesu. Mtu yule hakuwa na sababu ya kuwa mlevi. Acha ateseke.”

Yesu alisema, “**Enyi watu wajinga na wagumu kuelewa, amka muone ukweli, pendaneni kwa upendo wa kweli. Wasaidie wasiojiweza. Wasaidieni wahitaji bila kutegemea kupata malipo yoyote.**

“**Ukitubu, ee dunia, nitakubariki wala sitakulaani. Amka usingizini, na njoo kwangu. Jinyenyekesheni na inamisha mioyo yenu kwangu, nami nitakuja na kuishi pamoja nanyi. Mtakuwa watu wangu nami nitakuwa Mungu wenu**”

Sura ya 22

Alama ya Mnyama

Nilimsikia Bwana akisema, “**Roho yangu haitashindana na mwanadamu wakati wote. Njoo umwone mnyama.**”

“**Katika siku za mwisho mnyama mkali atainuka kutoka katika dunia na kuwadanganya wengi katika kila taifa duniani. Atadai kila mtu apokee alama yake, namba 666, imegongwa kwenye mkono au kwenye kipaji cha uso. Kila mtu atakayepokea alama hiyo atakuwa wa mnyama na atatupwa kwenye ziwa la moto ambalo linawaka kwa kiberiti moto na kiberiti.**

“**Mnyama atainuka na kushangiliwa na dunia nzima, kwa maana ataleta amani na maendeleo ambayo hayajawahi kuwako. Atakapokuwa amepata utawala wa dunia nzima, wale wasio na alama katika vipaji vya nyuso zao au katika mikono hawataweza kununua chakula, nguo, magari, nyumba au kitu chochote kinachouzwa. Wala hawataweza kuuza kitu chochote walichonacho kwa mtu ye yeyote mpaka kwanza wawe na alama.**

“Bwana Mungu amesema waziwazi kuwa wale watakaokubali kuwekwa alama watakuwa wamekubali kuwa watii kwa mnyama na watakatiliwa mbali na Bwana milele. Nafasi yao ni pamoja na wasioamini na watenda maovu. Alama hii inasema waziwazi kuwa walioipokea wamemkataa Mungu na wamemgeukia mnyama kwa mahitaji yao.

“Mnyama na wafuasi wake watawatesa wale watakaokataa kupokea alama na watawaua wengi wao. Watafanya kila namna kuwalazimisha waumini wa Mungu wa kweli kopokea alama. Watoto na vichanga vitauawa mbele ya macho ya wazazi wanaokataa kupokea alama. Kutakuwa na wakati wa maombolezo makubwa.

“Wale watakaokuwa wamepokea alama watalazimishwa kumpa mnyama vitu vyao vyote kwa ahadi kwamba mnyama atawatimizia mahitaji yao yote.

“Baadhi yenu mtadhoofishwa na kukubali kupokea alama yake katika mkono au kipaji cha uso. Mtasema, ‘Mungu atasamehe, Mungu ataelewa’. Lakini sitalibadilisha neno langu. Nimewaonya mara nyingi kupitia midomo ya manabii wangu na watumishi wa injili. Tubuni sasa kungali mchana, maana usiku waja ambapo hukumu ya milele itatolewa.

“Kama hamtamti mnyama na kukataa kuwekwa alama yake, nitawatunza. Sisemi kwamba hawatakuwa kwa ajili ya imani yao katika nyakati hizi, maana wengi watakatwa vichwa kwa ajili ya kumwamini Bwana Mungu. Lakini heri watakokufa katika Bwana, maana thawabu yao ni kubwa.

“Kweli, kutakuwa na kipindi cha amani na maendeleo ambapo mnyama atatukuka. Atafanya matatizo ya dunia yaonekane si kitu-lakini amani itaishia katika umwagaji wa damu na maendeleo yataishia katika njaa kubwa duniani pote.

“Usiogope utakalotendewa na mtu,mwogope atayeweza kutupa roho yako na mwili wako kuzimu. Maana kuna mateso makubwa na ingawaje mateso yataongezeka sana, nitakuokoa katika hayo yote.

“Lakini kabla ya ile siku mbaya,nitainua jeshi kubwa litakaloniamini katika roho na kweli. Jeshi la Bwana litafanya mambo makubwa na ya ajabu kwa ajili yangu. Kwa hiyo njooni, kusanyikeni, na mniamini katika roho na kweli. Leteni matunda ya utakatifu, na nipeni kilicho halali yangu, na nitawalinda na ile saa mbaya. Tubuni sasa na muokolewe kutokana na mambo mabaya yatakayowapata waasi na wasiookoka.

“Mshahara wa dhambi ni mauti, bali thawabu ya Mungu ni uzima wa milele. Niite wakati ungalipo, nami nitakukubali na kukusamehe. Nakupenda na sitaki upotee.

Sura ya 23

Kurudi kwa Kristo

Niliona kurudi kwa Bwana. Nilisikia mwito wake kama sauti ya matarumbeta na sauti ya malaika mkuu. Dunia nzima ilitikisika, na kutoka katika makaburi walitoka watakatifu waliokufa na kukutana na Bwana hewani. Ilikuwa kama kwa masaa kadhaa, nilisikia baragumu ikilia, na dunia na bahari vikatoa wafu wao. Bwana Yesu Kristo alisimama juu ya mawingun katika mavazi ya moto akiiangalia hali hii ya utukufu.

Nilisikia tena sauti ya matarumbeta. Niliona, wale waliokuwa hai na kubaki duniani wakipaa kwenda kukutana nao. Niliwaona mamilioni ya waliookolewa wakiwa kama miali ya moto ikukusanyika mahali fulani mawinguni. Kule malaika waliwapa mavazi meupe sana. Kulikuwa na furaha kubwa.

Ilikuwa ni kazi ya malaika kusimamia mambo, na walionekana kuwa kila mahali wakiwahudumia walionyakuliwa. Waliokombolewa walipewa miili mipya, na walibadilishwa walipokuwa wanapita hewani. Furaha kuu ilijaza mbingu, na malaika waliimba, “*Utukufu kwa Mtalme wa wafalme*”

Juu ya mbingu niliuona mwili mkubwa wa kiroho- ulikuwa mwili wa Kristo. Na mwili ulikuwa umelala chali kwenye kitanda, na damu ilichirizika hadi duniani. Nilijua kwamba huu ulikuwa na mwili uliochinjwa wa Bwana wetu. Halafu mwili ulizidi kuwa mkubwa na mkubwa hadi ukazijaza mbingu. Na mamilioni ya watu waliokombolewa walikuwa wanatoka na kuingia kwenye mwili ule.

Niliangalia kwa mshangao wakati mamilioni ya watu walipanda kwenye ngazi na kuujaza mwili ule, kuanzia kwenye miguu, kwenye mkono, kwenda kweye tumbo, kisha kwenye moyo na kichwa. Na ulipokuwa umejaa, niliona kwamba umejazwa na wanaume na wanawake wa kila taifa, kabilia na lugha duniani. Na kwa sauti kubwa walimsifu Bwana.

Watu mamilioni walikaa mbele ya kiti cha enzi, na niliwaona malaika wakileta vitabu ambavyo kutoka humo hukumu zilisomwa. Kulikuwa na kiti cha rehema, na wengi walipewa tuzo.

Halafu niliona, giza limefunika uso wa dunia. Na nguvu za mapepo zilikuwa kila mahali. Mapepo yasiyo na idadi yalifunguliwa katika vifungo vyao na kumwagwa duniani. Nilimsikia Bwana akisema, “**Ole kwa wakazi wa dunia, kwa kuwa Shetani amekuja kukaa pamoja nanyi.**”

Nilimwona mnyama amechukia, na alimwaga sumu yake juu ya uso wa nchi. Kuzimu kulitikisika kwa hasira, na kutoka shimo la kuzimu yalikuja majeshi ya viumbe viovu

waliotia giza juu ya nchi kwa vile walivyokuwa wengi. Wanaume na wanawake walikimbilia milimani na kwenye mapango. Na kulikuwa na vita juu ya dunia, njaa na vifo.

Mwishihi niliona farasi wa moto na magari ya vita mbinguni. Dunia ilitetemeka, na jua liligeuka jekundu kama damu. *Malaika alipiga kelele, “Sikiliza, ee Dunia, Mfalme anakuja!”*

Na katika anga alionekana Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, na pamoja naye walikuwepo watakatifu wa nyakati zote, wakiwa katika nguo nyeupe sana. Na nilikumbuka kwamba kila jicho litamwona na kwake kila goti litapigwa.

Ndipo malaika walipochukua visu vya kuvunia na kuvuna ngano iliyokauka-ambao ni mwisho wa dunia

Yesu alisema, “**Tubuni na mkaokolewe, kwa maana ufalme wa Mungu u karibu. Mapenzi yangu na neno langu litatimia. Itengenezeni njia ya Bwana.**”

Niliwaza, Ni lazima tupendane. Ni lazima tuwe imara katika kweli na tuwarekebishe watoto wetu kufuatana na ufunuo wa kuja kwa Kristo. Ni kweli Mfalme anakuja.

Sura ya 24

Ombi la Mwisho la Mungu

Yesu alisema, “**Waambie watu walio duniani kwamba wasiweke tumaini lao katika utajiri usio wa kuaminika, lakini waweke tumaini lao katika Mungu aishiye, anayetupa kwa ukarimu vitu vyote tunavyovifurahia. Tambea katika roho, na hutatimiza mapenzi ya mwili.**”

“**Usidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Kwa maana apandacho mtu ndicho atakachovuna. Panda katika mwili, utavuna uharibifu, pand katika Roho utavuna maisha ya milele. Kazi za mwili ni uasherati, uzinzi, uchafu, ibada ya sanamu, uchawi, hasira, wivu, ulevi, anasa na mengine yanayofanana na hayo. Wanaofanya mambo haya hawataingia ufalme wa Mungu.**

“**Matunda ya roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, utu wema, uaminifu, kujishusha, na kiasi. Wale ambao ni wa Kristo wameusulubisha mwili na tamaa zake.**

“**Neno la Mungu likitimia, ndipo mwisho utakuja. Hakuna ajuaye siku wala saa Mwana wa Mungu atakaporejea duniani. Hata Mwana hajui, kwa maana anayejua ni Baba tu. Neno linatimia haraka. Njoo kama mtoto mdogo, njoo nikutakase na matendo ya mwili. Niambie, ‘Bwana Yesu, njoo katika moyo wangu na nisamehe dhambi zangu. Najua kwamba mimi ni mwenye dhambi, na natubu dhambi zangu. Nioshe katika damu yako, na nifanye kuwa msafi. Nimeikosea mbingu na nimekosea Wewe na sistahili kuitwa mwana. Ninakupokea kwa imani kuwa Mwokozi wangu’.**

“**Nitawapa wachungaji wanaotoka katika kifua changu, na nitakuwa Mchungaji wako wa kondoo. Mtakuwa watu wangu, na nitakuwa Mungu wenu. Soma Neno, na msiache kukusanyika pamoja. Toeni maisha yenu yote kwangu, nami nitawalinda. Sitawaacha kamwe.”**

Jamani kwa Roho mmoja, tuna njia ya kwenda kwa Baba. Naomba kwamba nyie wote mje na mumpe Bwana roho zenu.

Sura ya 25

Maono ya Mbinguni

Baadhi ya maono haya nilipewa kabla Yesu hajanipeleka kuzimu. Mengine yalikuja karibu na mwisho wa safari zangu za kuzimu.

Kufanana na Mungu

Nilipokea maono haya ya kimbingu nikiwa kwenye maombi mazito, na kuabudu.

Utukufu wa Bwana ulishuka mahali pale nilipokuwa naomba. Miali mikubwa ya moto, taa angavu sana, na nguvu yenye utukufu ilikuja machoni pangu. Katikati ya moto na zile taa kulikuwa na kiti cha enzi cha Mungu. Katika kiti cha enzi kulikuwa na kitu kama Mungu. Furaha, amani na upendo ulifurika kutoka kwa Bwana Mungu.

Hewa kuzunguka kiti cha enzi ilijazwa na makerubi watoto, wakiimba na kubusu uso wa Bwana na mikono yake na miguu yake. Wimbo walioimba ni, Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana wa majeshi. Ndimi za moto zilikuwa juu ya vichwa vyta makerubi na kwenye ncha ya mabawa yao madogo. Mwenendo wa mabaya yao ulionekana kuaonishwa na mwenendo wa nguvu na utukufu wa Bwana.

Kerubi aliruka na kuja kwangu na kunigusa macho.

Milima ya Dhahabu

Katika maono nilitazama mbali juu ya uso wa dunia. Niliona kwamba kwa kitambo cha maili nyingi ardhi ilikuwa na kiu ya mvua. Ardhi ilikuwa imepasuka, kavu na tupu. Miti wala mimea ya aina yoyote haikuonekana popote.

Halafu niliruhusiwa kuangalia mbele kupita nchi kavu, hadi mbinguni. Pale palikuwa na milima miwili ikikabiliana, na vitako vyake vikigusana. Sijui urefu wake, lakini ilikuwa mirefu, mirefu sana. Niliisogelea karibu nikaona kwamba milima ile ilikuwa ya dhahabu _ dhahabu safi sana kiasi cha kwamba ilikuwa kama kioo.

Mbele ya milima ile niliona mwanga mweupe, na mwanga ulipanuka kufunika mbingu yote. Nilihisi moyoni mwangu kwamba huu ulikuwa ni msingi ambapo mbingu inakaa.

Watu wanapigania pete ndogo ya dhahabu, lakini Mungu ndiye mwenye dhahabu yote.

Kujengwa kwa Nyumba

Nilipokuwa katika maombi nilipokea maono. Niliwaona malaika wakisoma taarifa ya mambo tunayofanya hapa duniani. Malaika wengine walikuwa na mabawa, na wengine hawakuwa nayo. Wengine walikuwa wakubwa, wengine walikuwa wadogo, lakini kila sura ilikuwa tofauti. Kama ilivyo kwa wanadamu hapa duniani, malaika waliweza kutambulika kwa sura zao.

Niliwaona malaika wakishughulika kukata vipande vikubwa sana vyta almasi na kuviweka kwenye misingi ya nyumba. Vipande hivyo vyta almasi vilikuwa na upana wa futi moja na urefu wa futi mbili na vilikuwa vizuri sana. Kila wakati ambapo roho inaokolewa, almasi inawekwa kwenye nyumba ya mtu aliyesababisha roho ile kuokoka. Hakuna kazi ya bure inayofanywa kwa ajili ya Mungu.

Malango ya Mbinguni

Siku nyingine nilipokuwa katika maombi, niliona maono ya mbinguni. Nilikuwa katika roho na Roho wa Bwana na malaika alikuja na kunichukua kunipeleka mbinguni. Kwa mara nyingine kulikuwa na mwangaza mzuri na utukufu kama ule niliyouona nyuma ya milima ya dhahabu. Lilikuwa ni jambo la kushangaza kuona utukufu wa Mungu ukijidhihirisha kwa namna ile. Malaika na mimi tulipokaribia malango mawili makubwa katika ukuta mkubwa, tuliwaona malaika wawili wakubwa mno wakiwa na mapanga. Walikuwa na urefu wa futi arobaini, na mywele zao zilikuwa dhahabu iliyosukwa. Malango yalikuwa marefu sana wala sikuweza kuona mwisho wake kwenda juu. Ilikuwa ni kazi nzuri ya kisanifu ambayo sijawahi kuona. Yalikiwa yamenakishiwa kwa mkono, yakiwa na mikunjo ya aina mbalimbali, na kunakishiwa kwa vito, almasi na madini nyingine za thamani. Kila kitu kwenye malango kilikuwa na mlingano mzuri, na malango yalifunguka kuelekea nje. Baada ya kuangalila kwenye kitabu, malaika aliashira kwa kichwa, akiruhusu niingie.

Msomaji, huwezi kuingia mbinguni kama jina lako kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana Kondoo

Chumba cha Mafaili

Katika maono, malaika alinichukua hadi kwenye chumba kikubwa sana chenyе kuta za dhahabu. Herufi za dhahabu zilichorwa sehemu sehemu katika kuta. Ilikuwa kama maktaba kubwa, lakini vitabu vilisilibwa ukutani badala ya kuwekwa kwenye makabati.

Malika katika makanzu marefu walikuwa wanachukua vitabu na kuvichunguza kwa makini. Kulikuwa na mpangilio dhabiti wa mambo waliyokuwa wanafanya. Niliona kwamba vitabu vilikuwa na magamba makubwa ya dhahabu na baadhi ya karatasi zake ziliwu nyekundu. Vitabu vilikuwa vizuri sana.

Malaika niliyekuwa naye alisema kwamba vitabu vile vilikuwa ni kumbukumbu ya kila mtu aliyewahi kuzaliwa duniani. Niliambiwa kwamba kulikuwa na vyumba vingine mahali pengine vikuwa na kumbukumbu nyingine. Mara kwa mara malaika wakuu walileta kumbukumbu hizi mbele za Mungu kwa ajili ya Yeye kukubali au kukataa. Vitabu vilikuwa na kumbukumbu ya maombi, nabii, mwelekeo, kukua katika Bwana, roho zilizomgeukia Bwana, tunda la roho na mengine mengi. Kila kitu tunachofanya hapa duniani kinawekwa kwenye kumbukumbu na malaika katika mojawapo ya vitabu.

Mara kwa mara malaika huchukua kitabu na kusafisha kurasa zake kwa kitambaa laini. Kurasa zilizosafishwa hugeuka kuwa nyekundu.

Ngazi ya Mbinguni

Roho wa Bwana aliniletea maono yafuatayo. Niliona ngazi kubwa ya kiroho ikishuka kutoka mbinguni kwenda duniani. Upande mmoja wa ngazi malaika walikuwa wanateremka kuja duniani, wakati upande wa pili walikuwa wanapanda.

Malaika waliokuwa kwenye ngazi hawakuwa na mabawa, lakini kila malaika alikuwa na kitabu kilichoandikwa gamba la mbele. Baadhi ya malaika walikuwa kama wanatoa maelekezo na kujibu maswali yaliyoelekezwa kwao na malaika wengine. Walipopokea maelekezo na maswali yao kujibiwa waliondoka.

Vile vile niliona ngazi katika sehemu nyingine za duania. Malaika walikuwa katika hali ya kutembea wakati wote, wakishuka na kupanda. Malaika walikuwa wakitembea kwa ujasiri na mamlaka, kwa maana walikuwa wajumbe wenye maagizo kutoka kwa Mungu.

Sura ya 26

Unabii Kutoka kwa Yesu

Yesu aliponitokea kwa mara ya kwanza alisema, “*Kathryn, umechaguliwa na Baba kwenda nami katika vilindi vya kuzimu. Nitakuonyesha mambo mengi ambayo nataka dunia ijue kuhusu kuzimu na mbinguni. Nitakuambia mambo ya kuandika ili kitabu hiki kiwe kumbukumbu ya kweli ya jinsi mahali kusikojulikana kulivyo. Roho wangu atakufunulia siri kusuhu umilele, hukumu, upendo, kifo na maisha ya baada ya kufa.*”

Ujumbe wa Bwana kwa dunia iliyopotea ni huu, “*Sipendi muende kuzimu. Niliwaumba kwa ajili ya furaha yangu mwenyewe na ushirikiano wa milele. Ni viumbe vyangu, na nawapenda. Niite ningali karibu, nitasikia na kukujibu. Nataka kukusamehe na kukubariki.*”

Kwa wale waliozaliwa mara ya pili Bwana anasema, “*Msisahau kukutanika pamoja. Kusanyikeni, ombo na soma Neno langu. Mniabudu katika roho ya utakatifu.*”

Bwana anasema kwa makanisa na kwa mataifa, “*Wakati wote malaika wanapigana kwa ajili ya warithi wa wokovu na kwa wale watakaokuwa warithi. Sibadiliki. Mimi ni yule yule jana, na leo na milele. Nitafuteni, nami nitawamwagieni Roho wangu juu yenu. Watoto wenu na binti zenu watatabiri. Nitafanya mambo makubwa kati yenu.*

Kama hujaokoka, tafadhali piga magoti sasa hivi mbele ya Bwana na muombe akusamehe makosa yako na akufanye mtoto wake. Kwa gharama yoyote ile, amua sasa kufanya mbinguni nyumbani kwako kwa milele. Kuzimu kunatisha, kuzimu ni halisi.

Maneno ya Mwisho

Nataka kukuhakikishia tena kwamba mambo uliyoyasoma katika kitabu hiki ni ya kweli. Kuzimu ni mahali halisi kwenye mateso ya moto. Lakini vile vile nikuambie kwamba mbinguni ni mahali halisi na panaweza kuwa nyumbani kwako milele.

Kama mtumishi wa Mungu, nimejitoa kwa kuongozwa na Yesu Kristo na nimeandika kwa uangalifu mambo yote aliyonionyesha na aliyoniambia.

Ni vizuri zaidi kama utasoma kitabu hiki ukiwa na Biblia ili uweze kulinganisha yaliyoandikwa humu na yaliyoandikwa kwenya Maandiko Matakatifu. Naomba Mungu akitumie kitabu hiki kwa ajili ya utukufu wake.

Mary Kathryn Baxter

Ufunuo 20:13-15 Matthayo 10:28 Luka 12:5 Luka 16:20-31 Zaburi 9: 17
Mithali 7:27 Mithali 9: 18 Isaya 5:14
Isaya14:12-15 Mathayo 5:22
Mathayo 23:33 Marko 9:43-48 Warumi 10:9-10 1 Yohana 1:9

Kuhusu Mary Baxter

Mary Kathryn Baxter alizaliwa Chattanooga, Tennessee. Alikulia katika nyumba ya Bwana. Alipokuwa mdogo mama yake alimfundisha juu ya Yesu Kristo na ukombozi wake. Kathryn alizaliwa upya akiwa na umri wa miaka kumi na tisa. Baada ya kumtumikia Bwana kwa miaka kadhaa, alirudi nyuma kwa muda. Roho wa Bwana hakuweza kumwachia, alirejea na kutoa upya maisha yake kwa Yesu. Bado anamtumikia kwa uaminifu.

Katikati miaka ya 1960 alihama na familia yake kwenda Detroit, Michigan, ambako aliishi kwa muda. Baadaye alihamia Belleville, Michigan, ambako alianza kupokea maono toka kwa Mungu.

Mwaka 1976, akiwa anaishi Bellville, Yesu alimtokea katika mwili wa binadamu, katika ndoto, na katika maono. Tangu wakati huo ametembelewa mara nyingi na Bwana. Katika safari hizo amemwonyesha kina, upana, ngazi na mateso ya roho kuzimu. Vile vile amepokea maono mengi ya mbinguni, Dhiki Kuu, na mwisho wa nyakati.

Katika kipindi fulani katika maisha yake, Yesu alimtokea kila usiku kwa siku arobaini. Alimfunulia mambo ya kutisha ya kuzimu na uzuri wa mbinguni. Alimwambia kwamba ujumbe huu ni kwa ajili ya ulimwengu wote.

Wachungaji, viongozi na watakatifu wa Bwana wanenena mema juu yake na juu ya huduma yake. Uwepo wa Roho Mtakatifu unasisitizwa katika huduma zake zote, na miujiza mingi imefanyika katika huduma hizo. Vipawa vya Roho Mtakatifu na uthibitisho wa nguvu umeonekana katika mikutano yake kwa jinsi Roho wa Mungu anavyomwongoza

na kumuwezesha. Anampenda Bwana kwa moyo wake wote, akili, roho na nguvu zote na jambo analolitamani kuliko yote ni kuwa mvunaji wa roho za watu kwa ajili ya Yesu Kristo. Huyu kweli ni mjakazi wa Bwana aliyejitoa. Kipaji chake ni katika nyanja za ndoto, maono, na mafunuo. Alibarikiwa kuwa mchungaji mwaka 1983 katika Full Gospel Church kule Taylor, Michigan. Sasa anahudumu na National Church of God kule Washington, DC.

Mialiko ya huduma

Kwa mialiko ya huduma, mwandikie: Mary K. Baxter
Lowery Ministries International
P.O. Box 2550
Cleveland, TN 37320-2550